



HEKAYA ZA ABUNUWASI NA HADITHI ZINGINE



HEKAYA ZA ABUNUWASI NA HADITHI ZINGINE



HEKAYA ZA ABUNUWASI NA HADITHI ZINGINE

Bombay; London: Macmillan, 1942.

pictuspublishers@gmail.com

Pictuss, 2021

KISA CHA I

Abunuwasi alikuwa anapendwa sana na Harun Rashid. Hata ikawa Harun Radhid hawezi kushinda siku moja asimuone Abunuwasi.

Siku moja Abunuwasi akawa anataka kununua punda, na fedha hana. Akatoka akaenda nyumbani kwa Harun Radhid, na wakati si muda wa watu kwenda kwa Harun Rashid. Akafika mlangoni na kuwakuta mabawabu, akataka idhini ya kupanda juu. Mabawabu wakamwambia watu hawana ruhusa ya kwenda juu kwa muda huo. Akatokea bawabu mkubwa na kusema, nitakupa ruhusa upande lakini utakachopata tugawane sawasawa. Abunuwasi akasema, vema! Nimekubali.

Wakaandikiana shahada kwamba atakachopata wagawane sawasawa. Hati ya bawabau akachukua Abunuwasi, na hati ya Abunuwasi akachukua bawabu. Abunuwasi akapanda hata kwa Harun Rashid. Alipofika mbele ta Harun Rashid hakuamkia, akakaa kitako kimya. Harun Rashid adipendezwe na habari ile ya kunyamaza Abunuwasi na kukaa bila kuamkia. Akamuuliza, “Ya! Abunuwasi, una nini leo? Abunuwasi akasema, “nataka unipige fimbo mia moja. Basi Harun Rashid alimpenda Abunuwasi asiweze kumpiga. Akamwambia, “Huachi maneno haya Abunuwasi!”

Abunuwasi akajibu, “La! Lazima utanipiga.”

Harun Rashid akatwaa fimbo na kumpiga, lakini kidogo kidogo. Akampiga hata zikatimia hamsini. Hapo Abunuwasi akatwaa hati ya bawabu na kumuonyesha Harun Rashid na kumwambia, “Yuko mwenzangu tumepatana kadiri nitakachopata kwako tugawane nusu kwa nusu. Na sasa mimi nimepata fimbo hamsini na yeye lazima apate hamsini.”

Harun Rashid akaamrisha aende akaletwe mkubwa wa mabawabu. Akaletwa, kaamrisha achapwe fimbo hamsini. Akaambiwa hii ni adhabu yako, usirudie tena siku nyingine. Bawabu akajuta kufanya makubaliano na Abunuwasi.

KISA CHA II

Abunuwasi alijenga nyumba yake ya orofa moja. Ilipokuwa tayari, akatafuta mshitiri anunue asipate. Lakini kwa bahati akapata tajiri mmoja aliyekuwa tayari kununua, lakini Abunuwasi akamuuzia orofa ya juu tu, na ngazi yake akamuwekea nje, akitaka kupanda juu sharti apite kwa nje. Mambo yakawa hivi siku nyingi.

Hata siku moja akataka akataka kumalizia kuuza na sehemu ya chini kwa yule tajiri. Yule tajiri akakataa kununua. Abunuwasi akatafuta mshitiri mwingine asipate. Akafanya hila nyingine, akatafuta vibarua wengi sana, akaja nao pale nyumbani pake akamwita yule tajiri aliyekuwa juu, “Bwana, bwana!” Yule tajiri akaitika, “Naam!” Abunuwasi akamwambia, “Mimi nataka kuvunja nyumba yangu hii ya chini, wewe shikilia sana nyumba yako huko juu usije ukasema sikukuambia.

Yule tajiri akashindwa na hila za Abunuwasi, akainunua ile nyumba kwa bei aliyotaka Abunuwasi.

KISA CHA III

Siku moja Abunuwasi alipata dinari zake mia. Akaenda sokoni akanunua punda mzuri, akampanda. Akaenda naye mpaka nyumbani kwake. Hata siku moja akaja mtu kuazima punda wa Abunuwasi. Abunuwasi akamwambia, “Punda hayuko.” Mara kidogo punda akalia.

Yule mtu akasema, “Punda si huyo analia na wewe wasema hayuko!” Abunuwasi akajibu, “Sasa wewe umekuja kuazima punda ams umekuja kuazima mlio? Kama umekuja kuazima mlio na mimi nitalia.” Abunuwasi akalia, “Ho! Ho! Ho!” Kisha akamwambia, “Haya panda uende zako.”

KISA CHA IV

Siku moja punda wa Abunuwasi alikuwa na kiu. Lakini Abunuwasi hakuwa na chombo cha kumuwekea maji. Akaenda kwa jirani yake, akamwambia, “Naomba uniazime sufuria nimnyweshee punda wangu maji.” Alipopewa akaenda zake. Akakaa na sufuria ile kwa siku tatu. Siku ya nne, akatwaa ile sufuria, akatia na sufuria ndogo ndani yake na kumpelekea jirani yake.

Alipofika akamwambia, “Sufuria yako hii hapa.” Jirani yale alipoitwaa akaona dani yake kuna sufuria ndogo. Akasema, “Hii sufuria ndogo si yangu.” Abunuwasi akasema, “Mimi si mwizi, siwezi kuiba mali ya watu. Sufuria yako imezaa ikiwa kwangu, na hiyo ndogo ni mtoto wake.” Yule mwenye sufuria akafurahi sana, akasema, “Nyumba ya Abunuwasi ina baraka sana, hata sufuria inazaa!”

Baada ya siku tatu Abunuwasi akaenda kuazima sufuria ileile, akapewa. Safari hii Abunuwasi akakaa nayo hata asiirudishe. Mwenye sufuria akaamua kwenda kwa Abunuwasi kuulizia sufuria yake.

Abunuwasi akamwambia, “Sufuria yako imekufa.”

Yule bwana akasema, “Shaba hufa?” Abunuwasi akajibu, “Haikuzaa?”

Yule bwana akajibu, “Ilizaa.”

“Kila kitu kinachozaa hatima yake hufa.” Akasema Abunuwasi.

Yule bwana akashindwa la kumjibu. Akawauliza wanazuoni habari hii nao wakamjibu vilevile.

Kinachozaa na kufa hakina budi. Abunuwasi akahodhi sufuria.

KISA CHA V

Abunuwasi alikuwa anachukiwa sana katika mji wa Baghdad. Siku moja watu wenye vyeo wakamfanyia fitina kwa Sultani, wakataka wamuue kwa hila.

Sultani akamwambia, Abunuwasi, “Nataka ujenge nyumba ya juu angani ikiwa inaelea, kama ukishindwa kuijenga utauwawa. Abunuwasi akasema, “Semaan wataan(nimesikia, nimekubali).”

Akaambiwa kuwa anatakiwa kuijenga nyumba hiyo ndani ya siku tatu. Abunuwasi akasema, “Inshallah.” Akaenda nje ya mji na akatengeneza karatasi. Akaunga pamoja kwa wanga, akafabta portangi moja kubwa, akalifunga na kengele na kamba ndefu. Akangoja hata wakati wa upepo mwingi na kulirusha, likaruka juu sana kisha akaifunga kamba panapo mti.

Watu wa mjini wakaona kitu kipo angani na kusikia kengele zikilia. Walistaajabu sana maana hawakuwahi kuona kitu kama kile. Abunuwasi alipoona kazi yake imekamilika akatoka akaenda kwa kwa sultani. Akataka idhini ya kupanda juu ili akaonane na Sultani, akapata.

Alipomuona Sultani akamwambia, ile nyumba imekwisha jengwa maulana. Fungua dirisha utazame. Sultani akafungua dirisha na Abunuwasi akamuonyesha akimwambia, “unaona ileee? Unasikia vitu vinalia?” Sultani akajibu, “Naam, nasikia.”

Abunuwasi akamwambia, “Hao ni mafundi wakitengeneza sakafu, na hivyo vinavyolia ni nyundo na misumari. Walakini bwana zimepungua mbao kidogo, nataka ufanye jamala inipatie mbao na watu wapeleke.”

Sultan akasema, “watu hao watapita wapi?”

“Njia niliyopita mimi,” akajibu Abunuwasi.

Basi sultani akatoa mbao na kuwapa watu. Akawaambia, “pelekeni mbao hizi, mfuateni Abunuwasi.

Abunuwasi akawachukua mpaka pale alipofunga kamba. Akwaambia, “njia ni hii, piteni.”

Wakamjibu, “hatuwezi kupita juu ya kamba.”

Abunuwasi akawaambia, “sharti mtapita.”

Lakini wao wakasema hawawezi. Wakarudi kwa sultani na kumwaambia kuwa hawawezi kupita juu ya kamba.

Sultani akasema, “Kwa kweli hakuna mtu awezaye kupita juu ya kamba.”

“Kumbe unajua! Mbona badi ukaniambia nijenge nyumba hewani?”
Akasema Abunuwasi.

Sultani hakuweza kumjibu, akanyamaa kimya. Abunuwasi akaenda kukata ile kamba aliyofungia portangi nalo likaruka likaenda zake. Hiyo ndiyo asili ya maportangi.

KISA CHA VI

Hapo zamani alikuwako mwanamke mmoja mzee na mwanawe. Nao walikuwa ni madikini sana. Siku moja alitokea tajiri mmoja na kumwambia yule kijana kuwa akiweza kukaa ndani ya ziwa la barafu usiku kucha atampatia dinari elfu kumi.

Yule kijana kwa umaskini akajasirika kwenda kukaa katika ziwa la barafu usiku kucha. Na mama yake kwa uchungu wa mwana akawa akimgojea huku akimmulika. Kulipokucha yule kijana akamwambia tajiri, “nipe pesa yangu.”

Tajiri akamjibu, “Sikupi! Mama yangu alikufanyizia moto usiku kucha.”

Yule kijana akasema, “La, alikuwa ananimulika tu.”

“La, uongo! Amekufanyizia moto.” Akasisitiza yule tajiri.

Yule kijana alaenda kushtaki kwa Abunuwasi.

Abunuwasi akamwambia, “vema, nimekubali lakini utanipa kiasi gani utakapopata mali yako?”

“Nitakupa dinari elfu mbili,” alijibu yule kijana.

“La, utanipatia dinari elfu tatu,” akasema Abunuwasi.

Basi yule kijana akakubali. Abaunuwasi akamwambia, “nenda kadhtaki kwanza kwa sultani.” Yule kijana akaenda kwa sultani. Akaeleza mabo yake yote. Alipo maliza sultani akasema, “tajiri yupo sahihi, wewe huna haki.”

Yule kijana akarudi kwa Abunuwadi na kumwambia hukumu ya sultani. Abunuwasi akamwambia, “kwa fadhili ya Mungu, kesho utapata haki yako.

Abunuwasi akanunua mbuzi, mchele samli, bizari na vitu vyote vya karamu. Akamchinja mbuzi na kumchuna kisha nyama akaitia ndani ya sufuria. Na mchele pia akautia ndani ya sufuria. Akawasha moto lakini ukawa mbali na vyakula akaviweka mbali. Akawaalika watu kuja karamuni, sultani na mawaziri wake pia. Wakaja wakabarizi mlangoni pa Abunuwasi. Wakakaa hata jioni wasipate hata kahawa. Watu wakachukizwa sana. Wakaenda jikoni wakakuta moto uko mbali na vyakula viko mbali.

Sultani akamwambia Abunuwasi, “Abunuwas una wazimu?”

Abunuwasi akajibu, “kwanini maulana?”

“Tokea asubuhi tumekuja hapa. Hatujatia kitu tumboni na karamu hatuioni?”

Abunuwasi akajibu, “watu wanapika bwana, ila nyama haijaiva.” Sultani akaenda akatazama jikoni, akaona nyama iko mbali, mchele mbali na moto uko mbali.

“Vyakula hivi havitaiva hata kwa miaka kumi.” Akasema sultani.

Abunuwasi akasema, “vitaiva tu.”

“Najua havitaiva, mimi nakwenda zangu, tena na watu nitawaambia waende zao.”

Abunuwasi akamwambia, “Maulana usikasirike. Kumbuka yule kijana aliyelala usiku kucha katika ziwa la barafu alikuja kwako kushtaki. Nawe ukanena kuwa tajiri yuko sahihi, na kuwa kijana yule alipata moto kwa kumulikwa na mama yake! Atapataje moto naye alikuwa anammulika kwa uchungu wa mwana tu?. Basi tafadhali bwana, mpe yule kijana haki yake. Maana kama yeye alipata moto, na hivi vyakula vitaiva.”

Sultani akasema, “ulisiosema ni kweli tupu.” Kisha akamuagiza yule tajiri ampe yule kijana haki yake naye akampa. Baada ya hayo, Abunuwasi akaagiza vyakula vipapikwe, watu wakala karamu. Na Abunuwasi akapata haki yake.

KISA CHA VII

Siku moja Abunuwasi alikuwa mhitaji sana, basi akamwambia mkewe, “leo mhitaji sana mimi, nipe shauri.”

Mkewe akamwambia, “mimi sina shauri, shauri kwako.”

Abunuwasi akamwambia, “vema, mimi nitakwenda kwa sultani nitamwambia mke wangu amekufa na wewe nenda kwa mkewe na kumwambia mume wangu amekufa. Najua tutapata pesa ya kutumia.”

Basi wakaondoka na kwenda kutekeleza huo mpango. Abunuwasi akaenda kwa sultani akamwambia, “mke wangu amekufa.” Sultani akampatia sanda na fedha za maziko.

Na mkewe akaenda kwa mke wa sultani na kumwambia, “mume wangu amekufa.” Naye akapewa fedha na sanda. Basi wakatoka na kwenda kutumia pesa zile.

Sultani alipoingia kwa mkewe akamwambia, “mke wa Abunuwasi amekufa.” Mkewe naye akamwambia, “Abunuwasi amekufa.” Wote wakacheka.

Sultani akatuma watu kwenda kwa Abunuwasi kutazama. Wakaenda na wakamkuta mkewe anamuosha mumewe naye amevaa sanda. Akawaambia, “mume wangu amekufa.” Walipotaka kumtia ndani ya sanda, Abunuwasi akapiga chafya na kusema, “Alhamdulillah, Mungu kadiri, hukifanya hai kilichokufa, na kilicho hai kikafa.”

KISA CHA VIII

Ilikuwa siku moja Abunuwasi alisema, “Pindi mwenyezi Mungu akinijalia kupata reale mia tisa tisini na tisa, sitazipokea mpaka zitimie elfu kabisa. Nami niwe kama watu.” Watu wakamuona ana wazimu, apate reale elfu kadoro moja asipokee! Maneno haya yakaenea katika mji.

Hata tajiri mmoja akasema, “Ela nijaribu Abunuwasi, hivyo kweli akipata reale elfu kasoro moja ataacha?”

Akatwaa mfuko akatoa reale mia tisa tisini na tisa. Akaenda akaweka barazani pa abunuwasi. Alipotoka nje Abunuwasi akaona mfuko wa fedha. Akachukua ndani akahesabu akaona ni reale elfu kasoro moja

Akashukuru akanena, “Alhamdulillah, Mwenyezi Mungu amesikia dua yangu niliomba anipe reale elfu.

Na sasa kanipa tisa mia na tisini na tisa, haidhuru, hii moja namkopesha Mungu, najua atanipa siku nyingine zitimie hesabu nitakayo.”

Yule tajiri mwenye fedha akaja kwa Abunuwasi akamwambia, “Umeona mfuko wa fedha hapa?” Akanena, “Naam.”

“Zimo ngapi?”

Aka mwambia, “Reale elfu kasoro moja.”

Akamwambia, “Basi nipe mwenyewe.”

Abunuwasi akanena, “Kwa nini?”

Akasema, “Kwa kuwa ulisema pindi Mungu akupapo reale elfu kasoro moja hutazichukua sharti zitimie elfu.”

Abunuwasi akasema, “La hii ni riziki yangu kwa Mungu, naliomba, amenipa. Basi kama amenipa reale tisa mia na tisini na tisa atashindwa

kunipa moja?”

Yule taitri alipoona Abunuwas anafitini, akasema, “Twende zetu kwa Harun Rashid.”

Abunuwas akasema, “Kama ni hivyo, Mimi siwezi kwenda vivi hivi, na mimi nipe joho na kilemba na punda kama wewe. Tena ndipo twende barazani, maana sina nguo.” Yule tajiri akakubali akampa punda, joho, na kilemba ili kumwazima kuendea mashtakani Wakaenda

Walipofika yule tajiri akasema maneno yake kumshitaki Abunuwasi. Halafu Harun Rashid akamuuliza Abunuwasi habari

yake. Abunuwasi akasema, “Hawa Watu Wananionea sanaa mimi. Hivi ananisingizia habari za fedha hiyo, hakosi atasema na huyu Punda wake, na joho lake na kilemba chake.”

Tajiri akasema, “Nipe basi! Si Vyangu?”

Abunuwasi akasema, “Mnaona basi?”

Hata Harun Rashid akaona kweli wanamsingizia. Akaamuru achukue vyote abunuwasi.

KISA CHA IX

Siku moja Abunuwasi alikuwa anakata mti akawa amekaa kunako ncha ya tawi anakata shinan. Akapita mtu akamwambia, “Umekaa vibaya, hili tawi litakapoanguka na wewe utaanguka, maana umekaa nchani, unakata shinani.” Abunuwasi akasema, “Sianguki, hii ndiyo namna ya kukata miti mimi kuanzia leo.”

Yule mtu akaenda zake. Abunuwasi akawa anakata ule mti, ulipoanguka, na yeye akaanguka. Akaondoka upesi akamkimbilia Yule mtu aliyemwambia utaanguka. Akamwambia, “Ee bwana, nataka uniambie na siku ya kufa kwangu.”

Akamwambia, “Kwa nini?”

Akasema, “Sababu umeniambia, nitaanguka, na mimi nimeanguka kweli.”

Akamwambia, “Nalikuonya umekaa vibaya, lakini siku ya kufa sijui.”

Aka mwambia, “Sharti utaniambia.”

Yule mtu akataka salama yake, akamwambia. “Siku utakapopanda punda wako akajikwaa mara tatu, hujafika unakokwenda. Siku hiyo ndiyo mauti yako.

Abunuwasi akakaa, siku moja akapanda punda wake akaenda shamba. Zamani za kurejea aka mpiga

sana punda wake akaenda shoti. Punda akajikwaa kwa kule kwenda mbio. Akaenda tena mbio tena, akajikwaa ya pili, Abunuwas akasema, “Kufa kwangu karibu sasa.”

Akaenda mbele akajikwaa ya tatu. Abunuwas akashuka juu ya punda, akajifunika shuka, akajilaza twaaa kama mtu aliyekufa. Na yeye kulala

huku asema kafa, maana aliambiwa punda akijikwaa mara tatu ndiyo kufa kwake.

Basi akalala namna ile siku tatu, watu mjini wanamtafuta.

Hata siku ya tatu akapita mtu mmoja akamuona Abunuwasi, akamwuliza, akamwambia, “ile njia ya kwenda mjini kwa Harun Rashid iko wapi hapa.”

Abunuwas akaamka, akamwambia, “Mimi nafahamu nilipokua hai ukipita mwembe ule hata upandie pale; utakapofika mjini.”

Yule akamwambia, “mbona unasema ulipokuwa hai?” akamwambia, “naam, sasa nimekufa mimi.”

Akalala tena. Mara wakapita mabedui wamepanda ngamia. Walipofika pale alipokuwa Abunuwasi wale ngamia Wakashtuka, wakafanya machachari. Wale mabedui wakaudhika walipofahamu kama

Abunuwas ndiye aliyewashtua ngamia, Wakampiga sana kwa bakora, na Abunuwas akanyamaza kimya, maana kafa. kisha Mabedui wakaenda zao.

Yule mtu aliyeuliza njia, alipofika barazani kwa Harun Rashid akawasikia watu wanaulizana habari ya Abunuwas. Yule mtu akasema, “Abunuwas yuko hapo kalala, asema kafa.”

Harun Rashid akasema, “Mimi namjua Abunuwas mkienda kumwita tu haji. Chukueni baragumu mpaka alipo mkapige, kisha mwambieni Abunuwasi, Ondoka, amri ya kiyama imekwisha kuwako.”

Wakaenda watu wakapiga baragumu. Wakamwambia,

“Abunuwas ondoka amri ya kiyama imekuwako.”

Abunuwas akaondoka akajipangusa, akavaa nguo, akafuatana nao kwenda mjini.

Alipofika mjini watu wakamzunguka, wakamfanyizia mzaha, “Abunuwas kafufuka!”

Wengine wakamwuliza habari za ahera. Abunuwas akawaambia, “Ahera hakuna lolote. Watu wanatutisha tu kutuambia ahera hivi, ahera hivi, lakini hakuna lolote. Neno moja lipo, njaa, hapana kula huko.”

Nayo kweli, maana alikaa siku tatu hakula. “

Tena neno la pii akawaambia, “Neno baya nililoona huko kuwa baya sana ni hili. Kuna Mabedui huko wamepanda ngamia, ukipambana na hao watakupiga sana.”

Nayo kweli maana yeye ndiye waliyempiga

Harun Rashid akamwuliza habari za kufa kwake, Ilikwendaje?
Akamweleza yote.

Haruni Rashidi akamwambia, “Mtu huyo amekusmbua sana.”

Akanena, “La, hakunisumbua amenifaa sana. Sasa mimi najua habari zote za ahera.”

KISA CHA X

Abunuwasi alikuwa anachukiwa sana na watu wa Baghdad kwa mambo yake ya kuudhi watu. Wakaenda wakamfitini kwa Harun Rashid, Harun Rashid akaamuru atupwe katika kisima, na ndani ya kisima hiki alikuwamo simba. Abunuwasi akafanya hekima, Alipofika chini kazi yake ikawa kumkunakuna yule simba asimle, hata mwisho wakazoeana.

Chakula cha Abunuwas ikawa nyama aliyokuwa akitupiwa simba kila siku.

Abunuwas akakaa mle kisimani jumla ya siku nyingi. Hata watu wakafanya kumsahau mjini. Siku moja ikatokea ibra kubwa katika mji. Walipoamka asubuhi wakaona umetokeza mkono wa mtu baharini, umenyosha vidole vitatu.

Watu wakastaajabu. Wakampa habari mfalme. Akatoka kwenda kutazama, yeye na mawaziri wake, wakauona mkono wa mtu kweli, umetokeza baharini umenyosha vidole vitatu. Wakatafuta kujua maana yake wasijue. Wakaitwa wanachuoni wote wakaulizwa maana yake asitambue mtu.

Walipoona wameshindwa kutambua maana yake, wakataka kuuondoa ule mkono. Wakaisha kufanyiza uganga na uganguzi mkono haukutoka. Hata mwisho watu wengine wakamkumbuka Abunuwasi, wakasema, “Angekuwapo Abunuwasi angetuambia maana yake mkono huu.”

Wakampa habari Harun Rashid. Na yeye akaona kweli maneno yao.

Basi akatuma watu kwenda kumtazama Abunuwas kisimani.

Walipofika wakaita, “Abunuwas!” Akaitika, “Naam!”

Wakanena, “Mfalme anakutaka utoke.”

Akanena, “Siwezi kutoka sina nguo.”

Wakaenda kwa mfalme wakamwambia, “Abunuwasi kasema hawezi kutoka, hana nguo.”

Mfalme akawapa shuka kwenda kumpa Abunuwasi. Abunuwasi alipopata shuka pa kuvaa chini akaipiga kilemba.

Wakamwambia, “Fanyaa sasa toka.”

Akanena, “Siwezi kutoka sina nguo bado.”

Wakamwambia, “Nguo hatukukupa sasa hivi?”

Akanena, “La, nimepiga kilemba.” Wakampelekea nyingine akavaa. Halafu wakamwambia, “Sasa toka.”

Akanena, “Nitatoka namna gani nami sina fulana, wala kanzu, wala joho?”

Wakatafuta vitu hivi waka mtupia, akavaa, akawaambia, “Sasa tayari nitupieni kamba,” wakamtupia. Akaishika

ile kamba akawaambia, “Haya vuteni.” Wale juu wakawa wanavuta, na, yeye akatwaa fimbo anamkuna yule simba, na huku anapandishwa juu.

Alipofika juu akapelekwa kwa Haruni Rashid.

Mfalme akamwambia habari za ule mkono wa mtu. Abunuwas akanena, “Nina njaa, nipeni chakula kwanza.” Wakamfanyizia chakula Wakampa. Alipokwisha

kula akawaambia, “Haya twendeni kunako mkono.” Akatoka mfalme na jumla ya watu wakafuatana na Abunuwasi mpaka pwani. Abunuwasi akasimama kuukabili mkono. Na yeye akanyoosha mkono Wake akapunga kama vile anakaidi kitu. Mkono Ukafunga kidole kimoja Abunuwasi akapunga tena mkono, mkono ukafunga kidole cha pili. Halafu ukabaki mkono umenyosha kidole kimoja,

Abunuwas akatikisa mkono ukaondoka. Watu wakastaajabu wakamuuliza Abunuwasi tafsiri yake. Abunuwas akanena, “Mkono ule umekuja kuuliza kama katika dunia ipo siri ya watu watatu? Mimi hupunga mkono, hunena

la, hapana siri ya watu watatu. Vikabaki vidole viwili, maana yake, Je siri ya watu wawili ipo? Nikanena la, haipo.

Hapo kikabaki kimoja, maana yake, Ya mmoja je? nikanena, Naam siri ya mtu mmoja, ndiyo Maana mkono ukaondoka.”

Watu wakamsifu Abunuwas kwa akili zake.

Harun Rashid akampa abunuwasi nyumba na zawadi nyingi. Akawa mtu mkubwa katika mji.

Hata baada ya siku kupita mfalme akaota ndoto kama katika nyumba aliyompa Abunuwasi, upande wa kushoto kuna makasiki ya fedha chini. Asubuhi akapeleka watu kwenda kuchimba nyumba ya Abunuwasi ghairi ya kumpa habari mwenyewe. Wakaichimba ile nyumba wasipate kitu. Habari hii ikamuudhii sana Abunuwasi. Akanena, “haidhuru nitalipa kisasi.”

Akamwambia mkewe, “Mke wangu pika wali mzuri; kitoweo kuku.”

Mkewe akapika wali akaisha. Akamwambia, “Haya sasa wewe toka nenda katembe.” Abunuwasi akatwaa sahani na bakuli ya mchuzi akatia ndani ya sinia, akaweka chini ya meza, akafunika kwa kitambaa cheupe.

Kisha akafunga nyumba, na ufunguo akaweka juu ya mlango, akaenda zake. Njiani akakutana na vijana watatu. Akawaambia, “Najua ninyi vijana wa siku hizi jeuri sana, hivi nakuoneni mnakwenda upande wa nyumbani kwangu, msiende mkatwaa ufunguo ulio juu ya mlango, mkafungua nyumba, mkatazama chini ya meza, mkaona sahani ya wali kitoweo kuku, mkala na sahani na bakuli mkafunika ndani ya sinia bila kuosha.”

Wale vijana wakaona ajabu maneno ya Abunuwas. Wakanena, “huyu anatutuma nini tukale huu wali?”

Wengine wakanena, “Kwanza wali wenyewe upo? Twendeni tukatazame.”

Wakaenda wakafanyiza kama alivyosema Abunuwasi. Wakatwaa ufunguo juu ya mlango, wakafungua nyumba, wakatazama chini ya meza, wakaona

upo wali kweli.

Wakautwaa wakala. Sahani wakazifunika ndani ya sinia bila kuosha, wakatoka wakaenda zao. Abunuwas akapima kiasi cha wale vijana kula wali hata kwisha akarudi kwake. Alipofungua nyumba akaona wamekula wali. Basi akachukua sahani na sinia zimefunikwa vile vile mpaka kwa Haruni Rashid, akanena, “kuna watu nawashtaki wamekula wali wangu.”

Rashid kanena, “Wako wapi?”

Akanena, “Hawa nimewafunika ndani ya sahani.”

Akaambiwa, “Funua tuwaone basi.”

Akafunua, wakatoka inzi wakaruka. Akanena, “hawa ndio ninaowashitaki.”

Sultani akamwambia Abunuwasi, “unashtaki hata inzi?”

Akanena, “wao ndio walionikosa, asiyenikosa siwezi kumshitaki nami nataka unihukumie kama sheria.”

Sultani akamwambia, “nimekupa ruhusa kila utakapomwona nzi ametua mpige.”

Akampa na hati ya mkono wake.

Abunuwasi akachonga rungu kubwa. Ikawa hupita madukani akiona inzi wametua juu ya tende huzipiga zile tende akazitawanya tawanya. Akikuta juu ya papa huwapiga akawaponda.

Na watu wakipiga kelele kwa ajili ya kuharibiwa vitu vyao. Abuiiwas husema, “Mimi sipigi vitu nawapiga inzi.”

Hata siku moja Abunuwas akamwambia mkewe, nitakwenda lipa kisasi cha kuchimbiwa nyumba yangu. Akaenda barazani

kwa Sultani na fimbo yake. Akakaa karibu na Sultani. Hata mazungumzo yaliposhika sana, akaja inzi akamrukia Sultani kipajini. Abunuwasi akatwaa

fimbo ke akampiga Sultani e fimbo ya kipajini, kisasi cha kuchimbiwa nyumba yake!

Watu wakamkamata Abunuwasi wakataka kumfunga.

Abunuwas akanena, “Kama mtanifunga, mwanifunga kwa kunionea, mimi sikumpiga

Sultani, nimepiga inzi aliyemtua Sultani. Na ruhusa ya kupiga inzi amenipa yeye mwenyewe nimpige nitakapomwona ametua. Na hii hati ya mkono wake.” Ikatazamwa hati ikaonekana kweli akaachiwa Akaenda zake nyumbani kwake.

KISA CHA XI

Mtu mmoja alisafiri, naye alikuwa na ng'ombe jike mmoja. Kabla hajaondoka alimpeleka ng'ombe wake kwa mtu mmoja katika mji. Na yule mtu ana ng'ombe wake dume mmoja. Alipokuwa safarini yule mtu ng'ombe wake kazaa, wakatimia watoto saba. Aliporudi akaenda kwa yule mzee kuchukua ng'ombe wake. Naye anazo habari kuwa ng'ombe wake kazaa.

Alipofika akanena, “nataka ng'ombe wangu na watoto wake.” Yule mzee akanena, “nenda zizini kamchukue ngo'mbe wako Yule yule uliyeniachia.”

Yule mtu akanena, “itakuaje na ng'ombe wangu kazaa.”

Akanena, “la, ng'ombe wangu dume ndiye aliyezaa. Wewe wako alipokuj, alikuja hana mtoto na sasa mchukue mwenyewe.”

Yule mtu akaenda akisikitika, akafika kwa Abunuwasi. Akamueleza habari iliyompata. Abunuwasi akakubali kumsaidia. Abunuwasi akaingia ndani akatwaa nguo za kimaskini akavaa akaenda kwa yule mzee kwa masikitko sana, akasema “mzee nikopeshe rupia

tatu , nikamfae baba yangu ndiyo kwanza amezaa.”

Yule mzee akasema, “usifanye mzaha na mimi, kama amezaa mama yako nitakupa.” Abunuwasi akasema, “la, hapana bwana baba yangu ndiye aliyezaa.”

Yule mzee akanena, “sijapata kusikia kama mwanamume huzaa.”

Abunuwasi akamwambia kama, “hujasikia leo ndio kwanza.”

Basi mzee asikubali.

Abunuwasi akasema, “kama mwanamume hazai imekwendaje basi ukanyang'anya ng'ombe wa huyu kijana? Unasema ngo'mbe wako ndiye aliyezaa naye dume! Afadhali ungesema unataka uchungaji wako.”

Yule mtu asiweze kumjibu Abunuwasi akawatoa wote saba akampa mwenyewe.

KISA CHA XII

Siku moja palikuwa palikuwa na tajiri akachinja mbuzi wake. Wakati wa kupika mbuzi huyu, akaja maskini mmoja na chakula chake akakaa upande unakoendea upepo akala chakula chake kwa kutowelea harufu ya mbuzi. Asubuhi Yule maskini akakutana na Yule tajiri akamwambia, “bwana umenifaa sana jana, nimetowelea harufu ya mbuzi wako hata nikashiba.”

Tajiri akasema, “kumbe! Ndiyo maana mbuzi wangu hakuwa na ladha kwa sababu tamu yote umechukuwa wewe.”

Akaenda akamshitaki kwa Haruni Rashid na yeye alikuwa anapendelea saba matajairi. Basi yule maskini akalazimishwa kutoa rupia thenashara. Maskini akaenda zake akilia, maana fedha hana. Akakutana na Abunuwasi, alipomuuliza akamueleza yote

Abunuwasi akamwambia maskini, “usilie.”

Akatwaa Abunuwasi rupia zake thenashara akampa, akamwambia, “nakupa hizi nenda kalipe lakini usitoe mpaka nitakapokuja mimi.”

Asubuhi wakakutana wote kwa sultani maskini akasema amekuja kulipa zile fedha lakini akasikitika sana akasema yeye hakula nyama, katowelea harufu tu. Mara akatokea Abunuwasi wakamweleza yalivyokuwa.

Kisha abunuwasi akamwuliza maskini, “unazo rupia thenashara?”

Akajibu, “ninazo.”

Abunuwasi akazitwaa zile fedha akazishika, akamwita tajiri atwae fedha yake. Alipotaka kupokea, akamwambia, “ngoja.”

Akazitupa chini akamwambia, “haya chukua huo mlio wa hizo rupia. Maana maskini naye hakula nyama amekula harufu tu.”

tajiri akashangaa kwa visa vya Abunuwasi, akashindwa,

Abunuwasi akamwachia maskini zile rupia akaenda zake

SULTANI NA MVUVI

Alikuwako Sultani katika nchi ya Uajemi. Siku moja akaenda kutembea pwani pamoja na waziri wake. Wakamkuta mvuvi anatengeneza mishiپی yake tayari kwenda baharini, na siku hiyo bahari imechafuka vikubwa na upepo unavuma mtindo mmoja. Sultani akamwita mvuvi, “ya” mvuvi akaitikia, “naam maulana.”

Akanena, “palipo wanne na wanne hawakifu wanne?”

Mvuvi akajibu hawakifu wanne.”

Mvuvi akajibu, hawakifu wanne bwana.”

Sultani akamuuliza, “unamtumikia mtu au unatumikia nafsi?”

Mvuvi akajibu, “naitumikia nafsi.”

Sultani akanena, “ya mvuvi hallah! Hallah!”

Mvuvi akasema, “mimi mchokozi bwana namjua pweza alipo.”

Sultani na waziri wakashika njia kurudi mjini. Njiani sultani akamuuliza waziri, “umefahamu maneno yale niliyosema mimi na mvuvi?”

Waziri akasema, “la sikufahamu.”

Akamwambia, “wewe waziri mzima usifahamu maneno

yale, akayafahamu mvuvi! Sharti unifahamishe.”

Akamshika waziri hata asiwe na raha.

Waziri akaona hana njia ila amtafute yule mvuvi amuulize, akamwita kwake akamwambia, “nataka maana ya maneno yale uliyosema na sultani pwani?”

Mvuvi akamwambia, “sijui maana yake, mimi nilijiseme tu.”

Waziri akamwambia, “tafadhali niambie nitakupa reale miteen.”

Mvuvi akasema, “sijui.” Akamwambia, “nitakupa reale hamsi mia.”

Mvuvi akasema, “bwana wangu sijui fasiri yake.”

Akamwambia, “nitakupa shamba langu la mahali fulani.”

Akanena, “bwana sijui.”

Hata mwisho akamwambia, “nitakupa hii nyumba yangu ninayokaa.”

Mvuvi akamwambia, “niandikie hati ya mkono wako bwana,”
akamwandikia.

Akamwambia, “sasa nitakueleza, Sultani aliniambia palipo wanne na wanne hawakifu wanne.

Maana yake Sultani aliona ile dhoruba iliokuwako akaona ajabu kuniona mimi natengeneza nyavu kwenda baharini, ndipo akaniambia, ‘wewe katika mwaka kuna miezi minne ya kaskazi ndio wakati wa uvuvi wa samaki kuna miezi minne ya maleleji ndio wakati wa bahari kuwa shwari, basi miezi hiii nane huwezi pata samaki wa kutosha kuweka miezi hii minne ya kusi?’ Na mimi nikamwambia akiba ya miezi minane haitoshi kuwa akiba ya miezi hii minne ya kusi.”

Waziri alipopata tafasiri hii akatoka akaenda kwa sultani. Akamwambia, “nimekwisha pata fasiri ya maneno yako na mvuvi.” Sultani akamwambia umefahamu mwenyewe?”

Akanena, “naam.”

Sultani akafurahi akampa zawadi. Baada ya siku si nyingi, sultani akapata habari kama mvuvi anakaa katika nyumba ya

waziri. Maneno haya yakaenea katika mji hata sultani akataka kujua maana yake. Akamwita mvuvi akamuuliza, “amepataje kuwamo katika nyumba ya

waziri?”

Akamwambia, “nyumba ni yangu sasa ya waziri.”

Sultani akamuuliza, “imepataje kuwa yako.”

Akanena, “bwana unafahamu siku ile pwani uliponiambia Hallah! Hallah!? Nalifahamu kuwa umeniambia usimpe rahisi. nami nikakwambia mimi mchokozi namjua pweza alipo maana yake mimi maskini najua njia ya kupata pesa, sitamwambia ila kwa kupata faida kubwa na sasa nimepata faida nakaa nyumba ya waziri.”

Sultani alipoona kama waziri wake amemdanganya akakasirika sana akamwita akamwambia, “umenidanganya ya kuwa umetambua kwa akili zako kumbe umeambiwa! Basi sasa hufai wewe kuwa waziri. Umekuwa mwongo na mjinga. Huyu mvuvi ndiye atakayekuwa waziri wangu.”

Mvuvi akawa waziri, akastarehe siku zake zote.

SULTANI NA MKWEWE

Palikuwa na Sultani aliyekuwa na binti mmoja naye alikuwa akimpenda sana. Akampeleka chuoni akapata kuwa hodari sana katika elimu. Na katika mji ule alikuwako kijana mmoja wa kimaskini, lakini naye alikuwa amesoma vyema sana. Basi ikawa wakitokea watu wa kumposa yule mwanamke binti Sultani mtoto mwenyewe hukataa. Akamwambia baba yake, “Mimi sitaki kuolewa na mtu ila na Sefu,” ndiye Yule mtoto wa maskini. Baba yake akamhoji sana, “kwa nini kutaka Sharti akuoe huyu?”

Akanena, “moyo wangu ndivyo ulivyopenda.”

Sultani alipoona mwanawe ameshika, akakubali. Lakini akasema, “Sina budi kumtazama ili nijue kama ni kijana mwenye akili.” Akamwita yule kijana, akamwambia, “nakwenda, kutazama watu mahali fulani, name sitaki kufatana na mtu ila wewe.”

Yule kijana akanena, “vema.”

Wakaondoka wakaenda. Njiani wakaona mpunga umepandwa, umekwisha ota, una kimo chema, tena umezungushiwa uzio. Yule kijana akamuuliza Sultani, “nini hiki?”

Sultani akanena, “si mpunga huu!”

“Na hiki kilichozungushiwa ni nini?”

Akamwambia, “si uzio huu?”

Kijana akasema, “hivyo?”

Wakaenda mbele wakakuta watu wanalinda ndege mnamo mpunga. Wanapiga kelele, “Hao! Hao! Hao!”

Sultani anapita kati ya makonde ya mpunga wao wamekazana tu “Hao! Hao! Hao!”

Yule kijana akamuuliza, “wanafanyaje hawa?”

Sultani akamwambia, “si watu hawa wanalinda ndege? Na hao wanaofukuzwa ni ndege.”

Moyoni mwake mwake Sultani anamuona yule kijana kuwa mpumbavu. Maana maswali yote anayouliza ni ya kijinga. Wakazidi kwenda mbele.

Wakaona visima vingine viko kwa juu na vingine kwa chini. Wakaona watu wanakoga vile vya juu, na wengine wanateka maji ya kunywa hivi vya chini. Yule kijana akauliza, “nini hivi?”

Sultani akasema, “Si visima hivi?” “Na wale watu je?”

Sultani akanena, “wale wanakoga. na hawa wanateka maji ya kunywa.”

Kijana akaitikia, “Eh-e-e.” Wakaenda zao wakafika walikokuwa wakienda. wakakaribishwa vyema wakamletea sultani maziwa ndani ya kalasia. Akapokea yule kijana akayanywa kwanza kisha akampa Sultani. Halafu ikaja kahawa, naye kafanya vile vile. Sultani akaudhika na habari ile. Akaona kijana huyu mjinga, na bado hana adabu.

Hata walipokuwa wanarejea hawakuwa na mazungumzo mema. Maana Sultani alikuwa ameudhika sana. Akafika nyumbani kwake, binti yake akamwuliza, “je, baba umemuonaje mkweo?” Sultani akajibu, n”isikusikie tena unamtaja kijana yule. Kaniudhi namna gani! Mjinga na bado hana adabu.”

Binti yake akamuuliza, “nini ujinga wake baba?”

Akamwambia, “kwanza tulikuta mpunga umezungushiwa uzio. Akauliza nini hiki?”

Basi binti yake akamwambia, “baba hujui kwa nini ameuliza?”

Akamwambia, “sijui.” Akamwambia, “baba, mpunga ni majani tu, waweza kuanguka kwa upepo, na watu wanatwaa miti mikubwa wanazungusha. Ile miti ikianguka haitavunja mpunga?

Miti haina akili haiwezi kuzuia mpunga.”

Sultani akaona kweli.

Akamwuliza ujinga wa pili, Sultani akanena, “Aliuliza watu waliokuwa wakilinda ndege, kwa kupiga kelele, ‘Hao, Hao, Hao!’” Binti yake akamwambia, “waona ajabu huyo kuuliza? Alistaajabu kwa kuwa watu hawa wanamuona Sultani anapita nao wasinyamaze kidogo. Ndege hao watakula mpunga gani? Tena kule kusema Hao! Hao! Hao! Wakati Sultani anapita watu wengine hawatadhani ni ndege, watadhani hao ni Sultani na mkwewe.”

Sultani akaona kweli.

Akamwuliza ujinga wa tatu, akamwambia habari ya vile visima, na watu kuoga juu na kunywa vya chini. Binti yake akanena, “Baba basi hayo si dhairi? Kuwaje watu kuoga vya juu na kunywa vya chini?

Yale maji wanayokoga ndiyo yanayokuja hivi visima vya chini.”

Sultani akaona kweli. Binti yake akauliza, “nini tena?” Akamwambia, “sasa nikuelezee ukosefu wake wa adabu.” Akamweleza habari ile ya kutangulia kunywa maziwa na kahawa. Binti yake akamwambia, “yeye kafanya hayo kwa akili yake .Wewe Sultani wanakuhasimu watu wengi. Aliona huyu kijana huenda wakatia sumu, au kitu cha dhara yoyote katika vitu hivi, ndipo akanywa yeye mbele.” Sultani akaona yakuwa binti yake amesoma elimu vema, na yule kijana anamtaka kwa ajili ya akili zake. Akakubali kumwoza.

MVUVI NA JINI

Alikuwako mvuvi mmoja maskini, naye mcha Mungu sana. Alikuwa na kawaida akienda kuvua mshipi wake hutupa mara tatu tu atakachovua ndio chake na asipopata huwa basi.

Siku moja akaenda kuvua akatupa mshipi wake majini, akavua mzoga wa punda. Akanena, “ya Rabi mambo gani tena haya? Sasa imebaki mshipi miwili tu. Akatupa mwingine akavua vigae vya nyungu! Akanena, “Hayo mambo gani tena! Sasa umebaki mshipi mmoja sijui nitavua nini?” Akatupa mshipi wa mwisho akavua chupa ya shaba, alipoona ya kuwa ni shaba akasema, “haidhuru nitakwenda uza hii shaba nitapata pesa za kutosha kununua chakula.” Akatikisa, akasikia kinalia kitu ndani. Akasema, Ebu nijaribu kufungua nitazame kilichomo ndani.

Alipofungua akatokea jini mrefu, akasimama karibu yake, akamwambia, “ukitaka umekufa, usitake umekufa. Mimi nilifungwa na nabii Sulemani ndani ya chupa hii, nikatupwa baharini nimekaa baharini karne kadha wa kadha, Nikaweka nadhiri kama mtu akinivua kunitoa humu nitamjaza mema mengi. Hata nilipoona miaka imepindukia nikasema hapana, kwa ghadhabu zangu nikanena, ‘mtu atakayenivua nitamuua’ wala hapana vingine, basi na wewe ukitaka umekufa, usitake umekufa.”

Binadamu akamwambia, “basi bwana mkubwa ijazi yako ya kukuvua ndiyo hii, kutaka kuniua mtu niliyakutendea mema?”

Jini akasema, “mimi sifahamu hayo, nataka uchague unataka kufa namna gani, lakini kufa huna budi.”

Basi wakashindana hata wakasema twende tukashitakiane, wakashika safari kwenda zao mjini njiani wakamkuta ng'ombe, binadamu akamsimamisha na kumwuliza ng'ombe, “Ati bwana mtu akikutendea wema humlipa maovu?”

Ng'ombe akauliza, “kulikoni?” Akaelezwa kile kisa chote cha jini na binadamu, Ng'ombe akanena, “kweli mtu halipwi maovu kwa mema, lakini

si ninyi binadamu. Binadamu astahili kutendewa hayo maana si kitu Mimi nawapeni maziwa ya kunywa, na nyama yangu mnakula, na ngozi yangu mwaifanya viatu, na nyingine mwaiwamba ngoma, basi huu wema?”

Jinni akasema, “Je! Binadamu unasikia, akamwambia nasikia lakini twende zetu.” Wakaenda mbele wakakuta mnazi wakauliza kama walivyo muuliza Ng'ombe, Mnazi ukasema, “Binadamu astahili kutendewa kama hayo maana si kitu. Mimi mnazi nawafaa sana, nazi zangu wanapikia, kifuu wanakoka moto, makumbi wanafanya kamba, makuti wanaezekea, wakiwa na kiu nawapa maji, na ijazi yangu ni kunikata na kunifanya kizingiti!”

Jini akanena, “je binadamu unaskia? Akanena, Naskia lakini ushahidi ni mara tatu, twende mbele. Walipokwenda mbele wakakuta watu watatu, Yule binadamu akawauliza wale watu swali lile lile. Yule jini akasema, Maneno ni yale yale ya ng'ombe na mnazi, hawa binadamu haikosi watacupendelea wewe binadamu mwenzao.

Wale watu wakanena, “sisi hatuwezi kusema maana habari yenyewe hatusadiki. Ilikwendaje bwana mkubwa kama wewe kukaa ndani ya chupa hii?”

Jini akasema, “kama hamsadiki ngojeni niwaoneshe. Akaingia ndani ya chupa akasema nalikaa hivi. Wale wakafunga chupa hodari. Wakamwambia, kaitupe baharini akaenda akaitupa ukawa ndio mwisho wa uvuvi.

KISA CHA MAJUHA WAWILI WANAWAKE

Hapo zamani za kale palikuwa na maskini katika mji mmoja. Maskini huyo alioa mke na akazaa naye mtoto mmoja wa kike. Alikuwa na ng'ombe mmoja jike na ndiyo ilikuwa rasilimali yake pekee. Na kazi yake ilikuwa ni kulima makonde uko nje ya mji.

Kila siku wakati wa kuingia mjini huchukua majani ya ukoka kama chakula cha ng'ombe wake. Bibi na mtoto hubaki nyumbani. Hata siku moja alipokuwa yule mtoto ametimia miaka saba umri wake, aliota ndoto usiku.

Na ndoto yake ilikuwa ameota kaolewa tena amezaa mtoto mwanamke mzuri sana. Asubuhi baba yake akaamka akaenda kondeni kwake. Yule mtoto alipoamka akaangua kilio akalia, “mama wee! Mama wee mtoto wangu yuko wapi?”

Hata mama mtu akasikia kilio akaenda chumbani akamwuliza, “je mwanangu walilia nini asubuhi yote hii?”

Mtoto akamjibu mama yake kuwa, “nimeota ndoto usiku mmenioza mume, kisha nikazaa mtoto mwanamke mzuri, sasa naamka simwoni, ndiyo maana nalia, umemchukua wewe mama.” Akasema hivi na huku analia.

Mama mtoto aliposikia habari ya mtoto aliyezaliwa usiku na kumwona mwanaye analia, naye akaangua kilio akalia. Ikawa kelele moja kwa moja, hata majirani mtaani wakasikia vilio wakaja nao kusikiliza kuna nini? Mama mtu akawaelezea watu mambo yote ya ndoto, majirani wakacheka sana wakanena, “Haya mambo! Hatujapata kuona sisi watu kulia kwa sababu ya ndoto.” Lakini wale wenyewe wamekazana kulia,

Jirani mmoja mzee alipoona hawa ni wapumbavu, na kelele zikazidi akataka kuwanyamazisha akaenda kumwambia yule mama, “bibi hapana maana kukaa kitako ukilia, kama mtoto aliyezaliwa usiku amekufa, iliyobaki ni kuweka matanga nakuondoa.

Lakini aliyekufa kwa kuwa ni mtoto mdogo fanyeni chakula tu mpate kuondoa msiba.”

Yule mke wa maskini akasema, “hayo ni mashauri mazuri lakini nitaifanyaje mume wangu hayupo, naye ndiye mwenye mashauri ya mapesa.”

Yule jirani akamwambia, “huna hata kikuku ukachinja?”

Akajibu, “nyumbani hamna kitu ila ngombe wa bwana naye anampenda sana. Akaambiwa, “utafanyaje basi, nawe una sharti ya kuondoa msiba huu, usipoondoa itakua uchimvi utakufa wewe au mume wako.”

Yule mwanamke aliposikia vile akafanyiza hofu, akaona afadhali amchinje huyu ng'ombe maana sina kitu kingine. Akaita watu akagiza wamchinje ng'ombe.

Watu wakachekelea sana wakajua leo ndio kufaidi. Wakamchukua ng'ombe wakamchinja, wakamchuna upesi upesi. Wakatwaa mguu wakaenda wakabadili kwa mchele, wakatwaa nyama nyingine wakabadili na vitakataka vingine vya kupikia, Mara upishi ukasimama ukapikwa wali hata ikipata saa saba chakula tayari

Akaitwa mwalimu kuja kusoma hitima. Watu wengi wakaja kula chakula ikawa tena kila aliiyesikia akaja na wote waliokuwa wakija wakapata chakula. Hata habari ikaenea mji mzima kwa maskini kuna hitima, na wakisifu chakula kwa wingi wakati huu wote mume yupo shamba analima hana habari za hitima nyumbani kwake, Kasikia kwa watu waliokuwa wakitoka mjini kwenda shamba lakini hakutia moyoni maana hali ya nyumbani kwake anajua mwenyewe. Akakaa hata saa zake za desturi akang'oa ukoka wake, akashika safari taratiibu kwenda zake mjini.

Wakati huu kule nyumbani wale watu wamekwisha ondoka, maskini akafika nyumbani kwake mkewe akamlaki juu kwa juu, karibu bwana karibu. Yule maskini kimya akaongoza njia moja kwa moja mpaka zizini, akatua mzigo wake aingie ndani ya zizi ng'ombe hayumo!

Akashangaa, “ng'ombe wangu yuko wapi?”

Mara mkewe akaja akamwambia, “Mume wangu twende ndani nikakupe habari za mkasa ulionipata, na nikuelezee ng'ombe wako yupo wapi.”

Yule maskini akasema, “siendi popote mpaka nimwone ng'ombe wangu kwanza, Mkewe akamwambia, Bwana twende ndani nikakueleze.”

Lakini yule madjini akasisitiza, “nieleze hapa hapa.” Yule mkewe tena akaona hana budi kumweleza mambo yaliyopita akamweleza yote. Maskini aliposikia kuwa ng'ombe wake amechinjwa kwa ajili ya ndoto, akaduwaa, asijue la kutenda, akaingia ndani akakaa kimya, mkewe akamletea chakula asiweze kula.

Hata usiku Yule maskini akamwambia mkewe, “tangu kuzaliwa sijapata kuona juha kama wewe. Ilikwendaje wewe kusikiliza maneno ya ndoto? Basi sasa nifanyizie mikate nataka nisafiri nataka niende mbali nitafute mtu mwingine aliye juha kama wewe. Nikimwona utakuwa mke wangu hivi hivi. La sikumwona nitakuacha.”

Asubuhi mkewe akamtengenezea mikate akafunga akachukua na karatasi na bahasha na wino. Akaondoka akaenda zake msitu na nyika hata zikatimia siku saba akafika katika mji mmoja mkubwa. Na yeye kwa kuwa alikuwa na mashauri yake moyoni hakingia mjini, akafika katika kibanda cha kizee mmoja mwanamke. Yule mwanamke hakukasirika akamkaribisha, akamfanyizia na chakula.

Yule mgeni akauliza sana habari za mjini, na habari za wakubwa wa mji, kizee mwanamke akamwambia, “mwanangu, je, una haja nao hata ukawauliza hivyo?”

Akanena, “naam, shughuli kubwa.” Hata ilipofika usiku kizee akamwuliza, “je utakwenda mjini leo au utalala hapa leo?” Akanena, “Ningependa nilale hapa, asubuhi niingie mjini.”

Yule kizee akamwambia, “karibu mwanangu, ipo nafasi tele hapa.” Akapewa chumba cha pili katika kibanda chake. Yule mgeni akafurahi sana alipoingia chumbani kwake akafunga mlango wake akatoa karatasi zake, akakaa kitako akaandika barua zake, moja kwa Sultani, moja kwa binti Sultani moja kwa waziri, moja kwa mke wa waziri.

Akazifunga katika bahasha kila barua bahasha ya peke yake.

Asubuhi akamwuliza Yule kizee nyumba za watu hawa aliowaandikia barua ziko wapi?

Yule kizee akajibu, “Nyumba za watu hawa wote zipo pwani forodhani, ila nyumba ya Binti Sultani iko nje ya mji si mbali kwa kutoka hapa.”

Akauliza namna ilivyokaa, na alama zake akaambiwa zote, basi alipokwisha pata habari zote alizozitaka akaaga akasema, “kwa hapa mama sina budi kwenda mapema nikamuwahi kila mtu nyumbani kwake niwape barua zao.”

Akaondoka akaenda akishika njia akaingia mjini akafika panapo ile nyumba ya binti Sultani. Akatazama huku na huko akaona tanuru ya chokaa na ile tanuru inaelekea penye dirisha la binti Sultani. Akachimba chini ya ile chokaa. Akangoja mpaka alipoona sasa ni sa tatu akajifukiza pale penye chokaa kwa kichwa chake, na huku anapiga kelele, “Eeh! Jamani nifaeni mwenzenu natoka, mbali mimi, shime jamaa.” Mara akachungulia mtumishi dirishani akaona chokaa inatutumuka na kichwa cha mtu kinatokeza, akaenda akamwita bibi yake akamwambia tazama chini, “Kitu gani kile?”

Akachungulia chini akaona mtu anaotokeza penye chokaa na huku akipiga kelele. Mara binti sultani akamwita mtumishi mwana mume akamwambia, “Uledi nenda upesi ukamtazame mtu yule ana nini?”

Mara Uledi akaenda akamwuliza, “wewe ni shetani au binadamu?”

Yule mgeni akasema, “mimi ni mtu lakini natoka ahera nimetumwa kuja kuleta barua za watu hapa mjini. Je sasa mimi nipo wapi hapa?”

Uledi akamwambia, “hii nyumba inayokukabili ni nyumba ya binti Sultani.” Yule mgeni akasema, “ooh! vema sana ninayo barua yake hapa.”

Uledi akamshika mkono akatoka katika ile chokaa, akampeleka uani, akapewa maji akaoga, akapewa na chakula, na wakati wa kula akistaajabu. “Hivi ndiyo chakula cha ulimwenguni wa siku hizi?” Anafanya kasahau maana yake katoka ahera. Alipokiwsha wakampeleka kwa bibi, kufika tu

yule mtu akamwamkia bibi, akatoa barua akampa, akamwambia, “barua yako hii yatoka ahera kwa mjomba wako, naye anakusalimu pamoja na bwana.”

Binti sultani akafungua barua akasoma nayo imeandikwa hivi:

“Saalam mjomba, mimi huku ahera sijambo, na jamaa wote waliopo wazima ila mimi nina dhiki ya deni, nilikopa fedha za watu nami sina cha kuwalipa, basi tafadhali mpe huyu niliyemtuma rupia elfeeni aniletee nilipe deni za watu. Salaam Wakatabahu Mjomba wako.”

Yule binti Sultani aliposoma ile barua alisikitika sana akaenda zake moja kwa moja mpaka chumbani akafungua bweta akatoa rupia elfeeni ndani ya mifuko miwili akaenda. Kwenye sanduku la nguo akatoa kanzu ya hudhurungi safi na kanzu melimeli iliyo safi, na kanzu ya doria iliyo safi. Akatoa na buraa Muskati moja, na kitambi cha debwani iliyo njema, na kofia nyeupe ya kazi nzuri.

Akatwaa na vitu vingine vidogo vidogo kama miski, na halundi akatafuta kilesio kikubwa cha Hariri akafunga pamoja na vitu hivi vyote. Kisha akaandika barua kwa mjomba wake ahera akaandika hivi:

Salaam mjomba, waama baada ya salam barua yako imewasili. Nami nimefurahi kuniletea huyu mtu wa kunipasha habari ya kuwa wewe mzima, na vitu ulivyoagiza nimempa huyu mtu, nimempa rupia elfeeni, na nguo maana nasikia nguo adimu sana huko.

Salaam, mimi Binti Sultani.

Akampa bahasha Yule mtu wa ahera na barua hii. Akamwambia, “mchukulie mjomba mwambie bwana hukumkuta, ungepewa zaidi ya hivi.” Binti Sultani akaendelea kusema, “je nikupe mtu akuchukulie mizigo?”

Yule maskini akanena, “itanilazimu kuchukua mwenyewe maana ahera haendi mtu ila aliyekufa. Basi kwa heri, bibi sina budi kwenda upesi maana jua linapanda na sisi watu wa ahera jua linaatuathiri.”

Yule mgeni wa ahera alipotoka nje akaona haina haja ya kupeleka zile barua nyingine.

Akatazama huko na huko akaona mahali njia inapita kwenda vichakani akachagua njia hii, akashika njia kwenda zake. Njiani akapita akasema kimoyo moyo, “Ah! Kumbe majuha wapo wengi nikadhani ni mke wangu tu Kumbe hata katika watu wakubwa wamo majuha!”

Akashika njia akaenda zake upesi upesi, akaviisha vile vichaka akatokea katika mashamba. Alikua anakwenda hivi upesi kwa kuwa alishuku kuwa atafuatwa. Alipofika mle shambani akamkuta mzee mmoja analima, akamwambia, “eeh baba umepta habari za mjini leo?”

Yule baba akasema, “la! Sina habari, kumetokea nini?”

Yule mtu wa ahera akajibu, “imetoka amri kwa Sultani watafutwe vizee vya shamba wote wauawe iwe kafara ya

nyumba moja ya Sultani inayojengwa, basi mimi kwa hisani yangu napenda uvae hii kanzu yangu, na mimi unipe nguo zako za kulimia unipe na jembe lako nilimie, na wewe panda juu ya mnazi huu utazame juu njia ya mjini utaona mtu anakuja.”

Sasa turudi kwa binti Sultani baada ya kuondoka huyu mtu wa ahera mara bwana mume wa binti sultani akarudi nyumbani, akamkuta mkewe ana majonzi akamwuliza, “je bibi una nini?”

Yule bibi asiseme neno akatwaa ile barua akampa mumewe akaisoma. Alipokwisha soma akamwuliza mkewe jinsi yalivyokwenda mambo haya, mkewe akaleza yote jinsi alivyokuja mtu wa ahera akaleta barua hii, na yakuwa amempa mjomba wake wa ahera haja aliyotaka na zawadi nyingine.

Yule mume akakasirika sana akamwuliza mkewe, “wewe una wazimu! Sasa niambie huyu mtu kaenda njia gani?” Akaambiwa kapita ile njia ya vichakani, mara akaagizwa atandikwe farasi akavaa nguo zake, joho, kilemba na upanga mkononi. Akapanda farasi ili kumfuata huyu mwizi mkubwa lakini akamwambia mkewe, “fhamu mimi namfuata huyu mtu

maneno yake yakinielea vema utakuwa mke wangu lakini ukiwa ni upuuzi wako na wazimu nitakuacha.”

Akatoka akaenda zake kwa kasi. Basi alipokuwa anakuja mbio, Yule mjumbe wa ahera akasema, “je sikukwambia miye?” Mara yule mpanda farasi akafika pale akamkuta Yule hasimu wake analima. Akadhani huyu ni baba shamba tu, akamuuliza, “hukumwona mtu anapita hapa na bahasha?”

Akamjibu, “sikumwona bwana lakini tazama huko juu mnazini, kuna mtu: huyo ndiye aliyekuja kutoka huko mjini, alipofika hapa akapanda juu ya mnazi, nilipomwuliza akasema anaogopa basi sijui kama ndiye unayemtafuta.”

Yule bwana akamwuliza yule mtu kama anajua kupanda mnazi, yule akasema, “la bwana sijui.” Yule mwarabu akawa ameshikwa na uchungu, akawa anataka kumwua yule aliyekuwa juu ya mnazi, basi akavua nguo zake kanzu na joho na kilemba na jambia akampa yule mgeni wa ahera amshikie pamoja na farasi. Yeye akapanda juu ya mnazi. Alipokuwa akipanda akawa anasema, “utanitambua leo mwizi mkubwa wewe, leo kutoka yangu au yako.”

Na yule aliyekuwa juu akaona kuwa maneno ya yule mgeni wa ahera kuwa ya kweli. Akadhani huyu anakuja kuniua kwa habari ya amri iliyotoka. Basi naye akamwambia, “haya njoo nami nikuoneshe kazi kama sikukupiga na mundu wangu, yule mwarabu akawa anapanda tu, wala hatazami chini.

Yule mjumbe wa ahera kule chini akaenda akatwaa bahasha yake akafunga juu ya farasi. Akatwaa na zile nguo za mwarabu akazifunga juu ya farasi akampanda, Huyooo! Akaenda zake. Yule mkulima aliye juu ya mnazi akamwambia mwarabu, “Ela! Ebu tazama chini yuko wapi farasi wako?”

Akatehemu, kwenda juu hawezi, kushuka chini hawezi. Kisha akaona hana hila ila kushuka apate hakika ya maneno yale. Akamwambia yule mzee, “shuka chini tupate kuulizana vema. Yule mzee akakataa kushuka mpaka mwarabu alipomwapia kuwa hatamuua. Basi wakadhuka wote. Walipofika chini mwarabu akamwambia, “nipe habari ya yule habithi.” Mkulima akampa habari yote tangu mwanzo, alivyokuja na aliyosema, na kumtisha

kwa amri ya mfalme iliyoko mjini. Hata ikajiri kubadilishana nguo na yeye kupanda juu ya mnazi, hata kutokea yeye mwarabu.

Yule mwarabu aliposikia kisa hiki, badala ya kukasirika akacheke sana. Na yule mkulima naye akanwambia mwarabu, “Ela na mimi nieleze ilivyokwenda huko mjini.” Mwarabu akamweleza habari zote za barua ya ahera, na vitu alivyopewa. Wote wawili wakakauka kwa vicheko.

Yule mkulima akamuuliza mwarabu, “sasa ukienda nyumbani, Utakwenda kusemaje?”

Yule mwarabu akasema, “Sina la kusema ila nitakwenda kumwambia bibi kuwa nimemkuta yule mtu, nami

niliposika habari za ahera moyo wangu ukaingia huzuni sana, hata sikuweza kustahimili nikampa farasi wangu na nguo zangu zote awachukulie watu wa ahera. Je! waonaje kizee?”

Kizee akasema, “Kwell maneno yako. Mana ukisema kuwa umenyang’anywa utachekwa sana. Mwarabu akarudi mjini na kikoi chake na Jambia lake mkononi. Kisha akafika kwa mkewe.

Mkewe akamuuliza, “jinsi gani bwana nguo zako na farasi viko wapi?”

Akamwambia, “kweli maneno yako bibi. Habari za ahera nilizosikia kwa yule mjumbe wa ahera zimenitia huzuni sana, hata nimempa farasi na vitu vyangu vyote kuongezea vile uilivyompa wewe.”

“Bai sasa Bibi na tukae. Lakini pamoja na hayo akija mtu mwingine kutoka ahera usimpe kitu mpaka unishauri.”

Sasa tumrejee yule mjumbe wa ahera. Baada ya kupata farasi akamwendesha kasi, akaenda mwendo Wa siku chache kuliko alivyokuja maana sasa kapanda farasi. Akafika hata kwa mkewe, amechoka kwa kwenda mbio. Akamfungua farasi mzigo wake akaimweka katika lile zizi la ng'ombe wake. Na mzigo akauweka ndani.

Aiipokwisha pumzika na kula chakula akamweleza mkewe mambo yote ya safari yake. Akamwonyesha na fedha. Akanena Sasa na tukae kitako mke wangu nimekwisha muona aliye juha kuliko wewe. Lakini Pamoja na hayo ukitokea tena Upuzi wa ndoto wajibu uningoje unieleze tufanye shauri pamoja. Wakakaa raha mustarehe.

JOGOO NA SUNGURA

Hapo kale paliondokea sungura akafanya urafiki mkubwa mno

na jogoo, ikawa jogoo hali kitu asipomuona sungura kwanza. Wala Sungura hali asipomuona Jogoo kwanza.

Wakakaa katika hali hii kwa muda wa siku nyingi sana, pasipo hitilafu iwayo yoyote.

Hata siku moja Jogoo akawaza moyoni mwake, “Ah! Hivi huyu rafiki yangu anapokuja kwangu na tukizungumza maneno yetu ya siri huyachukua na kwenda kumwambia mkewe nini? Ela safari hii nitamjaribu kumpa neno moja la upuzi tu, nione mwisho wake.”

Desturi moja waliyoafikiana wao kwa wao tangu awali ya urafiki wao, ndiyo, mtu akija kwa mwenziwe kutembea, hana ruhusa kulala ndani ya nyumba ya mwenziwe, ila ni kulala upenuni tu, hata ikiwa ni siku ngapi, bora malazi mazuri ya upenuni wala si ndani ya nyumba. Hayo ndio maafikiano yao walioyokuwa nao. Walidumu daima. Wala hapana mmoja aliyenung'unika, maana kwa kila mmoja alitengeneza kipenu kizuri akatia kitanda na matandiko mazuri. Ikawa kwa kila mmoja aendapo kwa mwenziwe huja kulala mahali pake, upenuni.

Hata siku hiyo, mzee Sungura alipokuja kwa Jogoo kwa matembezi na malazi pia, Jogoo katika yale mazungumzo yao, akamwambia Sungura, “Je! rafiki yangu hizi siku unazokuja hapa na ukalala, je! usiku hunisikia nikisema nini au huweweseka na kubwetabweta kwa namna gani?”

Sungura akamjibu, “La, hata siku moja sijakusikia ukisema wala ukibwetabweta neno,

ila karibu na asubuhi tu, pale unapotuamsha sisi sote. Nakusikia ukisema, ‘Kucha kucheree. Mamiye Mwali Kamie ndege reeee.’ Hivi tunakusikia ukihimiza. Watu waende kazini kwao.”

Lakini zaidi sifahamu. Ndipo Jogoo akamwambia Sungura, “rafiki yangu, basi tangu leo nakupa siri ya mimi na wewe tu, na siri hii shika moyoni mwako tu wala usimwambie mtu, hata akiwa ni mkeo wa nyumbani haifai kumwambia. Wasikia rafiki yangu? Halahala shika hayo yangu wala usidanganyike na neno liwalo lote.”

Sungura akajibu, “Vema, rafiki yangu, mimi sithubutu kutoa neno lako nje.” “Wakakaa

Hata siku moja Jogoo akamwita mkewe ampendaye akamwambia. “Mke wangu, siku moja rafiki yangu Sungura atakuja kula na kulala hapa. Basi mtandikie pale pale upenuni pake pa siku zote, na tena, sikia sana mke wangu mimi usiku. Nitakuamsha nitakuambia, mke wangu. Huachi wee. Mtu wajua kazi yako ya siku zote, ya kukata kichwa changu ndipo nipate usingizi, leo umeniacha kulala na kichwa changu. Nitapataje usingizi?”

Ndipo wewe unijibu, ‘Ah! Mume wangu, nisamehe sana usingizi ulinishika upesi nikalala pasipo kukata kichwa chako, haya basi lete kisu nikukate niweke kule, ili upate usingizi.’

Ukisha, useme tena, ‘Haya lala sasa nimekwisha kata kichwa chako usinisumbue tena.’ Na vile vile kadhalika, asubuhi mimi nitaamka nitatikisa mbawa zangu. Nitakuita, Mke wangu, lete kichwa changu nataka kutoka nje sasa, wewe nawe ujipurukushe.

‘Ah! Bwana wee saa, udhia gani huu, watu wote hulala na vichwa vyao wewe ni kunisumbua tu kukata na kukiunga siku zote, mambo gani haya?’”

Maarifa haya yote jogoo akamwelekeza mkewe tangu siku ya kwanza hata siku alipokuja rafiki yake Sungura.

Siku zikipita Sungura akaja kwa Jogoo, wakaamkiana kwa namna zote, wakakaa, wakazungumza sana. Hata katika mazungumzo yao, Jogoo akamwambia Sungura, “je! juzi nilikuambiaje rafiki yangu?”

Sungura akajibu, “Uliniambia ya kuwa siri yangu usimwambie mtu au sivyo?” Jogoo akamjibu, “Ndivyo, ila leo nakupa neno moja tena, ndiyo, La upenuni na halisimuliwi nje; Wakasikia rafiki yangu?”

Sungura akajibu, “nasikia sana.” Wakazungumza sana, hata wakati wa kulala, jogoo akaingia ndani na mkewe na sungura akaenda upenuni pake kwenda kulala. Hata kupita muda kidogo tu sungura ndo kwanza usingizi ukaanza kumshika, mara jogoo akaanza kuita.

“Mke wangu! Huachi wee, mtu Wajua Kazi yako ya siku zote kazi yako ya kukata kichwa changu ndipo nipate usingizi leo

umeniacha kulala na kichwa changu, nitaupataje usingizi?”

Mara hiyo hiyo mke wa jogoo akajibu, “Ah! Mume wangu, nisamehe bwana, usingizi ulinishika upesi, halala pasipo kukata kwanza kichwa chako, haya basi, lete kisu nikikate, nikiweke kule upate kulala.”

Mke wa Jogoo akaenda kwa Jogoo akakitwaa kichwa cha mumewe akakitia ndani ya bawa, akasema. “Haya lala, nimekwisha fanya kazi yangu.”

Wakati huu Sungura amekwisha amka asikiliza tu maneno ya Jogoo na mkewe jinsi wapeanavyo mashauri. Wakalala hata karibu na asubuhi Jogoo akaita tena, “Mke wangu! Mke wangu! Ah! Mambo gani hayo?

Huku atikisa mbawa zake, Ela nipe kichwa changu nipate amsha watu watoke nje.”

Mara mkewe yule Jogoo akafanya kama alivyoambiwa na mumewe, akaenda huko na huko, mara huyu, “haya bwana, lete shingo niweke kichwa chako, udhia gani huu, watu wote hulala na vichwa vyao, wewe ni kunisumbua tu.”

Mara Jogoo akaanza kuwika.

“Kucha kuchereee. Mamiye Mwali Kaimie ndege-reee.” Mara mbili tatu, hata asubuhi kweupee. Watu watoka na kwenda kazini kwao. Yote haya Sungura asikiliza tu na kuona kwa macho jinsi watu watokavyo na kwenda kazini kwao.

Asubuhi kulipokucha, Sungura na Jogoo wakanawa, wakala chakula chao wakaisha. Wakakaa vile vile hata usiku, mambo ya Jogoo yakawa vile vile

kama juzi na jana na Sungura ni kusikiliza tu pale upenuni alipolala.

Hata siku za kukaa Sungura kwa rafiki yake Jogoo zikaisha. Sungura akaaga kurudi kwake Jogoo akamuaga vizuri na kumpa zawadi nyingi, zake na za bibi yake pia, akaenda zake.

Sungura njia nzima ni kuwaza tu mambo na maneno yaliyotendeka kwa jogoo mara akawaza moyoni mwake, “Ah! Jogoo ana maarifa gani ya kunishinda? Mimi sungura nina maarifa mangapi yote kwa ajili ya ujanja wangu.”

Sungura kufika kwake akamwita mkewe kuzungumza yote aliyoyasikia na kuyaona nyumbani kwa jogoo, hata akamwambia, “kesho kutwa rafiki yangu jogoo anakuja basi nawe nitendee kama hayo ambayo jogoo anatendewa na mke wake.”

Lakini mke wa sungura akamjibu, “vema bwana lakini sijawahi kuona mtu akakatwa kichwa akaishi.”

Sungura akamjibu mkewe, “mbona rafiki yangu jogoo yupo hata leo! Na kesho kutwa yuaja utamwona akija mzima na kichwa chake.”

Wakakaa hata siku ya tatu Jogoo huyu akawasili, Sungura akashughulika sana kumkaribisha rafiki yake. Wakakaa wakamkiana kwa njema zote na kuulizana habari zote. Wakati wa chakula wakafurahi sana hata jionii Jogoo akatandikiwa vile vile upenuni na Sungura na mkewe wakaingia ndani kulala. Jogoo halali, asikiliza tu kuona kama Sungura hakumwambia mkewe siri yao.

Mara akasikia, “Mke wangu! Mke wangu! Mbona hivi? Mtu kazi yako uijuayo sikuzote, leo waniacha kulala na kichwa changu, ela usingizi nitaupataje? Haya upesi, fanya kazi yako kama sikuzote, lete kisu upesi unikate kichwa changu ukiweke. Jogoo aliposikia maneno yale akashtuka, lakini asiseme neno akakaa kimya tu akisikiliza mwisho wa maneno yao.

Mara mke wa Sungura akaenda akatwaa kisu kikubwa na Kikali nakumkata mumewe shingo yote akaiondoa. Sungura akaruka huko na huko

anapapatika mkewe akashangaa tu, hajui la kufanya, aona ni ajabu tu hii ya mtu kukatwa kichwa akaishi.

Mzee sungura alipoisha kupapatika akafa kabisa foo pale pale, mke wa Sungura akaenda akalala. Hata asubuhi mke wa sungura akaamka, akaenda kukichukua kile kichwa cha mume wake akaenda kukiumanisha penye shingo, akaanza kumtikisa mume wangu, “mume wangu amka ati, kumekucha rafiki yako anakungoja,” kimya hapana sauti wala kuamka, aona nzi tu wanaanza kukusanyika. Akamshukuru Mungu, “Lillahi hamdu. Mume wangu amekwisha kufa hapana zaidi tena.”

Akatwaa nguo akamfunika. Muda ule ule mke wa sungura akafungua mlango amkuta shemeji yake jogoo kaisha amka zamani anamngoja yeye tu.

Jogoo akamwuliza mke wa sungura. “Je! bwana yuko wapi? mbona hata sasa hajaamka anaumwa nini? au kaenda wapi?”

Mke wa sungura akamjibu Jogoo, “Bwana kaisha kufa, ela njoo uone huyu hapa, sijui kama kalala, lakini mimi naona kama amekufa.” Jogoo akaenda kufunua nguo na kumwangalia mzee Sungura. Amekwisha kufa.

Jogoo akamwuliza mke wa Sungura, “Umemfanyaje mumeo?”

Mke wa Sungura akamwambia Jogoo, akasema. “Tangu siku alipokuja kwako na kurudi hapa, akanieleza yakuwa rafiki yangu Jogoo halali na kichwa, mkewe humkata kichwa usiku na hata asubuhi hukiunga mahali pake, na jogoo, (wewe ati), huwa mzima vile vile! Basi tangu arejee kutoka kwako, bwana wangu akanifundisha sana maneno na matendo aliyoyaona na kuyasikia kwako, ukitendwa na mwenzangu. Na sasa nami nimemtenda vile vile kama alivyonihamuru, na kumbe mume wangu kafa. Jogoo akamjibu mke wa Sungura, akamwambia. “Nasikitika sana sana kwa kuwa rafiki yangu hakutambua maana ya maneno yangu.”

“Maana, mimi nalimwambia wakati nilalapo huimwambia mke wangu, Haya upesi nikate kichwa nilale. Maana yake ni kusema, Je! mke wangu, hapana hata ukoko unipakulie nipate kulala? ndipo mke wangu huvumbulia kidogo ukoko aliouficha na kunipa. Na kadhalika kwa asubuhi,

humwambia, Mke wangu nipe kichwa changu maana yake, haya fanya upesi chakula, Kidogo angalau nipate nguvu za kutoka nje ndipo mke wangu hufanya chakula kwa upesi na kunipa nikala, ndipo hutoka nje na kuwaamsha watu.”

Lakini sasa rafiki yangu kajidhulumu nafsi yake, ndipo jogoo akawaita watu kwao kina Sungura wakamzika. Tangu siku hiyo urafiki wa jogoo na sungura ukakatika kwa kutokusikilizana.

KISA CHA PAKA KUPENDA MEKONI

Zamani za wahenga, paliondokea paka akapeleleza sana jinsi viumbe walivyoumbwa na nguvu na kuwa kila mmoja humpita mwenziwe kwa nguvu. Basi katika kupeleleza kwake akaona na akadhani ya kuwa hapana kiumbe mwenye nguvu kupita simba.

Akashika njia akaenda kwa simba akafanya urafiki mkubwa, ukasitawi kwa siku nyingi, Wakapatana sana. Hata siku moja simba akatoka kwenda kutembea mahali pa mbali, yeye na rafiki yake paka, kule matembezini wakakutana na tembo. Tembo waliipomwona simba wakamfukuza sana, hata wakamkamata, wakamtwa na kumpachika kwenye panda ya mtini sawia.

Paka alipoona vile akashangaa sana, akasema moyoni mwake, “Ah! Mimi huwaza ya kuwa simba ni bora kumbe kuna aliyemzidi!” Akatoka kwenda kumtafuta tembo, akamwona, akamwambia nataka urafiki, Tembo asikatae, kamwambia vema. Wakakaa, siku zikapita nyingi katika hali ya kupendana na kusikilizana.

Lakini ikatukia siku walipokuwa wakitembea tembea msituni mwao, mara wakamwona mtu mwindi nyama, mara yule mwindaji akaelekeza bunduki yake kwa tembo, akampiga tembo risasi moja tu akaanguka chini akafa. Paka akazidi kushangaa, “Ah! Huyu ndiye mwenye nguvu kupita wote, yaani kaniulia rafiki yangu mpenzi! Paka akafanya majonzi sana sana. Hata mwindi alipoondoka kwenda zake nyumbani, paka akamkimbilia akamwambia, “Ee bwana nataka kukufuata uendako.”

Mwindi akiona ni Paka tu, akamjibu, “Vema, haya, twende zetu kwangu. Walipofika nyumbani, mara paka akaona mke wa mwindaji akija mbio akipokea silaha zote za mwindaji, tangu bunduki hata risasi na baruti pia. Paka kwa ujinga wake akazidi kushangaa, akawaza katika moyo wake. “Hakika, huyu ndiye mwenye nguvu kuliko wote, maana kaweza kunyang'anya silaha zote kutoka mkononi mwa mwindaji. Na mwindaji

hakutoa neno lolote ila ni kukaa kitako na kupumzika tu. Huyu ndiye wa kumfuata mimi.”

Basi papo hapo Paka akamfuata mwanamke ndani, hata jikoni, akakaa karibu na mwanamke jikoni wakati akiandaa chakula cha mumewe. Paka akawa mzoefu sana kukaa jikoni, hata ikambidi yule mwanamke kumtuma Paka kukamata panya na kumlindia vyombo vyake visiharibiwe na Panya. Tangu siku hiyo ndiyo maana ukaona Paka hatoki jikoni hata leo.

KISA CHA KUKU NA MWEWE

Hapo zamani za kale Mwewe alikuwa na mtoto mmoja tu wa pekee, na jina la mtoto huyo alikuwa akiitwa Rahisi. Basi ikatukia yule mtoto wa pekee wa Mwewe akawa mgonjwa sana, hata ikajulikana ya kuwa Rahisi bin Mwewe yu katika hatari ya kufa. Baba wa Rahisi akawaita watu kadha wa kadha awajuao kuwa hawa ni waganga na wenye akiliili kuja kwake kumtibu na wamponye mwanawe. Katika wale walioitwa pasitokee hata mtu mmoja aliyeweza kuuponya ugonjwa wa Rahisi bin Mwewe. Mama Mwewe na Baba Mwewe wakaona majonzi makuu mno hata hawajui la kutenda wameduwaa tu.

Hata siku kupita, akaja mmoja. Akamwambia Mwewe kuwa yeye ana mganga mmoja, ajuaye sana dawa na awezaye kuuponya ugonjwa wa Rahisi maana mganga huyo hutibu magonjwa yaliyo makubwa kupita huo wa mtoto wa Mwewe. Lakini kabla ya kwenda kumwita huyo mganga, sharti nipe fungu kwanza ndipo niweze kwenda kumwita.

Mwewe akamjibu yule mtu, “Vema mimi tayari kutoa fungu lako kukupa, lakini mtoto wangu asipopona? ni vipi?”

Yule mtu akamwambia Mwewe, “ikiwa huyo mganga kaja, na kakupa dawa yake, na mtoto wako Rahisi bin Mwewe kainywa, naye asipone fahamu, ya kuwa nitakurudishia mali yako yote uliyotoa kunipa, huu wahadi nakupa.”

Mwewe akaona furaha sana kusikia maneno hayo, akamjibu, “vyema haya, fungu lako kiasi gani wataka?”

“Reale hamsini, bwana.” Akajibu yule mtu.

Mwewe akamwamuru mkewe kutoa reale hamsini za Sham. Akampa yule mtu, akamwambia, “Haya tafadhali nenda upesi sana sana maana mtoto wangu yu katika hatari ya kifo.”

Yule mtu akatoka mbio, akaenda hata kwa Buibui, akabisha, “Hodi! hodi!”

Akajibiwa, “Karibu! karibu.”

Yule mtu akamwambia Buibui, “Ee bwana, nimejua kuwa wewe ni mganga sana, na huko nje mtoto wa bwana Mwewe ni mgonjwa sana sana, basi tafadhali fanya shime, uende upesi ukamponye, maana utapata fungu kubwa sana la mali, kwa kuwa waganga wengi wameshindwa kuuponya ugonjwa wa Rahisi bin Mwewe.”

Buibui akamjibu yule mtu, “Vema, mimi ni tayari kwenda, lakini itakulazimu wewe unichukue mimi, kwa maana, wajua sana ya kuwa mzee kuku akiniona tu njiani, atanidonoa hata nife.”

Yule mtu akamuuliza Buibui, “Wewe na kuku mna ugomvi gani hata akuue bure bila kisa?”

Buibui akamjibu binadamu, “Hukusikia jana mbiu ya mgambo aliyotangaza mzee Kuku, ya kuwa Kuku akiona mdudu awaye yote machoni pake, na awe chakula kufa afe tu pasipo huruma, basi je! Mimi mdudu mdogo tu machoni pa kuku?”

Lakini yule mtu hakumsadiki, buibui akadhani labda ni uvivu Wake tu, akazidi kumshurutisha ili aende peke yake na mikoba yake tu buibui akaona imembidi kwenda, hana la kutenda.

Akashika njia safarini na mkoba wake wa dawa kwapani. Hata kufika nusu ya njia wala si mbali tena kufika kwa Mwewe, akafika kwa kuku akajiepusha upande wa nyasini ili kujificha lakini kuku akiangalia chini aona nyayo za buibui zaendelea nyasini, akazifuuata huko huko. Akagundua kajificha na mkoba wake nyasini, mara akamkamata na kumpiga mdomo mmoja tu na kumwua sawia.

Akawaita watoto wake akawatupia, watoto walipoona ni nyama wakafurahi na kunyang’anyana kila mmoja ili apate kidogo kidogo hata wakamwisha pasi hata unyayo wake kuonekana. Wakautwaa mkoba wa dawa wakauchanachana. Wakazivunja chupa na kuzimwaga dawa huko na huko wakaenda zao.

Mwewe alikuwa katika hali ya kungoja siku ile waliyoagana na binadamu akakaa hata adhuhuri, aona saa zapita na mtoto wake tena yu katika kutapia roho.

Mwewe akaona binadarnu amemdhihaki na mara akachukua gongo lake akashika njia nakumfuatia binadamu, kumwuliza habari. Alipofika njiani, wala si mbali na kwake mara aona vigae chekwaa vya chupa za dawa zilizovunjika na vitambaa vimepasuliwa na kutupwa huko na huko. Akizidi kuangalia sana akaona barua, akaiokota, akaipasua, akaisoma, akaona imeandikwa hivi;

“Binadamu kaja niita, asema, Rahisi bin Mwewe mgonjwa sana, upesi ukamwahi. Basi nia yangu na lazima yangu, ilikuwa kwenda nyumbani kwa Mwewe.”

Yule Mwewe alipokwisha soma ile barua, na kutazama mgaragazo ulitokea pale njiani hakuwa na neno ila kurejea nyumbani kwake kumwuguza mtoto wake. Hazikupata siku mbili tena mtoto wa Mwewe akafa, akapumzika.

Waiipoisha ondoa matanga Mwewe akawaza sasa ndio wakati wa kulipiza kisasi cha mtoto wangu Rahisi bin Mwewe kati ya mimi na Kuku. Akapiga mbiu ya mgambo kwa binadamu na kwa wote wenye miguu minne, ya kuwa, Kwa kila amwonaye Kuku, au mtoto wa Kuku, awe chakula kwake, amwue tu, asiwe na huruma. Na yeye Mwewe akajiapia kiapo kusema, nitamlilia mwana wangu Rahisi mpaka kufa.

Basi tangu siku hiyo ukawa uhasama mkubwa mno kati ya Kuku na Mwewe, na ndiyo manaa ukaona hata leo kuku hana msamaha kwa mwanadamu wala kwa Mwewe, na ndiyo ukamsikia Mwewe alia huko juu “Rahisi, Rahisii.” Yaani awakumbusha sababu ya ugomvi wao, ya kuwa kwa kumzuia Buibui kuja mponya Rahisi bin Mwewe ndiyo maana vita hiyo ikawapo wala haitakwisha.

Na tena ndiyo rnaana ukamsikia Kuku akishikwa na mwanadamu alia, “Siye, siye Si mimi, Si mimi.” Yaani ajaribu kukataa kuwa yeye hakuwapo katika vita hiyo. Lakini Mwewe amekataa kupambanua, hukamata na kuwala tu hata leo.

KISA CHA MAJUHA WATATU

(MAANA YA MAJUHA NI WATU WAPUMBAVU)

Hapo zamani paliondokea mtu, akaenda kutembea. Akafika njiani akawakuta watu watatu wamekaa kitako, yule mtu akawaamkia, “Salaam aleikum!

Majuha.” Wakaitikia, “Aleikum salaam.” Yule mtu akapita akaenda zake.

Wale Majuha huku nyuma wakabishana wao kwa wao, mmoja akasema, Salamu hizi ni zangu mimi, wa pili akasema juha ni mimi, wa tatu akasema vile vile. Basi wakawa katika hali ya kubishana mmoja akasema, “sisi hatuna haja ya kubishana kutwa maana yule mtu bado kufika mbali, twende tukamwulize, katika sisi watatu juha ni nani?”

Wakakubali wakaenda wote watatu huku wanapiga kelele za kumwita yule mtu, “Ee Bwana weee, simama! Ee Bwana, simama!” Yule mtu akawaza, “Nimefanya nini huko nyuma nilipowapita wale watu?” Akasimama.

Hata walipomfikia karibu mmoja wao akasema, “Ati bwana, ile salamu uliyotoa Si yangu mimi? Juha si mimi?”

Wa pili akamwuliza vile vile, “Je! ile salaam si yangu! Juha si mimi?” Watatu naye akauliza, “Juha si mimi, Bwana?” Yule mtu akawaza rohani mwake ya kuwa nitawauliza watu hawa. Akamwuliza yule mmoja, “Lete habari za Ujuha kweli!”

Akasema, “Bwana mimi ni juha kweli. Jana nalikwenda sokoni, nikaenda nikanunua nyama, nikampelekea mke wangu akapika, kabla nyama haijaisha kuiva bado, yule mke wangu akatoka, akaenda kuomba chumvi. Huku nyuma nikatwaa vipande viwili vya nyama nikatia mdomoni nikatafuna, kabla sijameza, mke wangu akaja nami kutafuna nikaona haya, ile nyama nikaitia katika shavu moja likajaa fututuu, mke wangu aliporejea akaniona ni hali ile, akasema, ‘Alhamdu Lillahi Rabbi-l-alamina, Mwenyezi Mungu ni mkubwa. Mara hii natoka kwenda omba chumvi, naja ndani

mume wangu amevimba shavu! Bahati! lete uma na moto.’ Akaleta ule uma, ukawashwa moto nikachomwa katika shavu, nikaona shavu hili linaungua, nikageuza nyama katika shavu la pili, nalo likachomwa, nikaona sina mahali pa kugeuzia tena nikaitema ile nyama, nikaiangusha pale chini pu! Mke wangu akaniambia, ‘Ah! Mume wangu, mke ni mkeo, nyama ni nyama yako, umefanya upumbavu kama huu, hata nimekutia vidonda katika mashavu?’ Je! Bwana, wasemaje mimi si juha?”

Akasema, Kweli juha ni wewe. Naam, yule wa pili akasema, “juha ni mimi, jana nilikwenda sokoni nikanunua nyama, na mchele, na nazi, na bizari na kunipia nikaja nikampa mke wangu akapika akaisha. Na mji huu una amri ikifika saa nne mlango hufungwa, lakini ikifika sa nne kama hukufunga mlango hukamatwa ukalazwa korokoroni, asubuhi huzungushwa mji mzima kisha hupelekwa kuchinjwa.

Basi nyumbani petu tumekaa hata ikapita saa nne bado hatujafunga mlango, wala chakula hakijapakuliwa.

Nikamwambia mke wangu, Pakua chakula! Akapakua akaisha akaweka juu ya meza, tukitaka kula nikamwambia mke wangu Tusile, nchi hii ina amri na wewe unaijua, basi kafunge mlango kwanza ndiyo tuje tule; mke wangu akaniambia, ‘Kafunge wewe,’ nikamwambia, Kafunge wewe, akaniambia, ‘Kafunge wewe.’

Nikamwambia mke wangu, Hatuna haja ya kubishana, basi na tukae hivi hivi tu, na chakula tusile, atakayekula, na akafunge mlango, na atakaye sema, na akafunge miango.

Basi tukakaa mimi na mke wangu kimya tukatazamana tu. Tukakaa hata akaja punda mle nyumbani, akala mtama hata ukaisha, punda akatoka, hapana asemaye, atakayesema na akafunge mlango. Akaja mbwa akaingia nyumbani, akaramba vyombo vyote akaja pale mezani akala ule wali wote, sahani akazivunja akaenda zake, hapana asemaye kama Mbwa amekula wali wote,

Atakayesema na akafunge mlango. Tukakaa hata saa saba. akaja askari, akatuuliza, ‘sababu gani hamkufunga mlango?’

Tusiseme, tukanyamaza askari akatuchua akatupeleka korokoroni hata asubuhi tukapelekwa kwa Sultani. Sultani akasema, ‘Wazungusheni mji mzima kisha mkawachinje.’ Mimi na mke wangu tukazungushwa

mji mzima hatusemi, hata tulipofika karibu na nyumba yetu, mke wangu akasema, ‘Mume wangu, si ile nyumba

yetu mbona twaipita?’ Mimi nikamzomea mke wangu, Woooo! Mke wangu amesema, Eeeee Woooo! Mke wangu amesema!’

Yule askari akasema, ‘Ah! Watu hawa wana ninii? Sultani ameniambia niwazungushe, nikifika pwani niwachinje, sasa wanasema hivi! watu hawa nitawarudisha kwa Sultani.’ Askari akaturudisha, akamweleza Sultani, Sultani akatuuliza, nasi tukamjibu, akatupa ruhusa tukarudi kwetu nyumbani.

Je! Waonaje? Wali wangu, mke wangu, nyumba yangu ikitaka kuniua, Je! Bwana mimi si Juha?”

Akamwambia, “wewe ni Juha zaidi ya yule wa kwanza.”

Watatu akasema, “Bwana, Juha ni mimi, mimi jino langu liliniuma, nikauliza. Humu mjini hamna mganga wa jino? Nikaambiwa, ‘yupo hapa anaitwa Ali.’ Nikaenda kwa Ali, nikamwambia, jino langu laniuma, unajua kutoa jino?

Akasema, anajua. Nikamwuliza, Unatoa kwa pesa ngapi Akaniambia, Nusu rupia tu. Nami nina nusu rupia yangu ya dhahabu, sawa na reale tano. Nikampa akanitoa jino moja.

Nikarudi nyumbani kwangu, mke wangu akaniuliza, ‘umekwisha tolewa jino?’ Nikamwambia, Nimekwisha kutolewa.”

“Akaniuliza, ‘umempa fungule?’

Nikamwambia, ile rupia yangu ya reale tano. Akaniambia, ‘Ah! Mume wangu, wenzio watolewa jino moja kwa robo ya reale, pesa 32, wewe umetolewa jino moja, umetoa reale 5!”

“Nikarudi kwa Ali, nikamwambia, Kumbe! Wenzangu unawatoa jino moja kwa pesa 32 mimi umenitoa jino moja kwa reale zangu 5! Basi afadhali unitoe yote! Ali akanitoa yote nikarudi nyumbani. Mke wangu akaniuliza umepata rupia zako? Nikamwambja, Ohooooho: na miye nimemkopa, akaniuliza, ‘Kwanini?’ Nikamwambia

Amenitoa meno yote kwa robo moja ya dhahabu, je waonaje mke wangu, sikumkopa Ali?

Mke wangu akaniambia, ‘ndiyo wewe juha.’”

Yule mtu akamwambia, “Ah! Wewe juha sana, hata salamu zile ni zako wewe.”

Wakarudi wakiambiana huyu ameshinda wenzake kwa ujuha

SIMBA NA SUNGURA

Zamani za kale aliondokea simba akaenda mwituni kuwinda

wanyama ili apate chakula. Hata siku moja alipokuwa akitembea alisikia mashindo, akitazama aona kundi la nyati, akashangaa kwanza, lakini akawaza kuwa, Miye sikuzote hutafuta wanyama na wanyama ni hawa, nitabahatisha. Akajibanza mahali kimya. Mara walipokaribia akamchagua mmoja akamrukia. Vikaanguka vishindo, patashika. Mzee nyati akaangushwa chini. Huku na huku, akapigwa ukucha wa shingo akafa.

Lakini kwa jinsi vita ilivyokuwa kubwa hata mzee simba naye akajeruhiwa mkono. Lakini maadam amepata chakula basi, akamkokota hata chini ya mti mkubwa penye kivuli kizuri, akakaa akitweta. Mara akatokea Sungura, naye alikuwa anapita tu katika matembezi yake hakujua kama mzee simba yupo pale.

Hata alipomwona akamtambua kuwa ni Bwana mkubwa, akamwambja, “Sabalheri mjomba, mbona upo hapa, tena

una nini? Mbona nakuona hali hiyo?” Kumbe Sungura kaisha ng'amu kama mzee simba ana nyama pale. Basi simba akamwita akamwambia, “Njoo mwanangu, hali yangu mgonjwa kidogo.”

Sungura akaenda, simba akamwambia, “sungura unaiona nyama hiyo?”

Sungura kanena, “Naam naiona, nini shauri lako bwana?”

Simba akamwambia, “Nataka uichune uzuri, uitumbue uzuri, uoshe uzuri, ukiisha uniletee moyo, maini na figo, nipate kufungua kinywa, maana tangu asubuhi sijala kitu.”

Sungura akaenda upesi upesi, akatengeneza ile nyama kama alivyoambiwa. Lakini mahali pa kupeleka vitu vile alivyoagizwa na simba, (ndiyo moyo, maini na figo) akavichoma vizuri akala yeye mwenyewe. Akatwaa nyama ya mafuta akachoma akamchukulia mzee simba.

Simba akiangalia aona hivi sivyo vitu alivyotaka.

Akamwambia Sungura, “hivi sivyo vitu nilivyotaka.”

Sungura akasema, “Bwana mkubwa vitu ulivyotaka vimeungua moto vyote.” Simba akanyamaza kimya kwa kuwa mkono unamuuma, akatwaa ile nyama ya mafuta akala, akanywa maji akashukuru. Akisha kula akamwambia sungura, “Sasa huna ruhusa kuondoka, kazi yako ni kunipikia maji ya moto, na chakula, mpaka nijaliwe kupona mkono wangu.”

Sungura akasema, “Ee walah, bwana wangu, mimi mtumishi wako tokeapo nitathubutu wapi kukutupa katika hali hiyo ya ugonjwa?”

Wakakaa siku nyingi. Hata siku moja akapita mzee fisi pale, naye kafanya kupotea njia tu. Sungura akamkaribisha fisi. Fisi alipoangaza macho akaona mifupa imetupwa ovyo hayana mlaji, akayamezea mate. Sungura alipozidi kumwuliza habari, akasema kuwa amepata habari kama mzee simba hajiwezi, basi kapita hapa ili kumtazama.

Basi Sungura akanena, “Ningoje kidogo nikampashe habari mzee simba.”

Akaenda kumpasha habari kama Fisi kaja kumtazama. Simba akamwambia Sungura, “Vema, nakuja sasa hivi.” Akatoka nje, akaamkiana na fisi wakakaa. Simba akamwambia Sungura, “Mtafutie chakula mgeni.” Sungura akaenda akamkusanyia fisi mifupa yote, nyama akampa kidogo. Maana anamjua fisi ulaji wake ni mifupa. Basi mzee fisi akala hata akashiba, akapewa maji akanywa.

Alipokwisha shiba fisi akaaga akasema, “Bwana mkubwa leo nina haraka sina budi kwenda zangu, lakini sitakawia nitarudi kukutazama. Akaenda zake lakini moyoni mwake asema, “Ah! najua huyu Sungura anafaidi, nifanye hila gani hata na mimi nikae Pale nile mifupa pale?”

Hata baada ya siku mbili tatu, Mzee Fisi huyu akaja tena, “Hodi Hodi!”

Sungura akaitikia, “Karibu, nani Wewe?”

Akajibu, “Ah! ni mimi Fisi nimekuja tena kumtazama mgonjwa.”

Akaambiwa, “Karibu.”

“Je, Bwana u hali gani mkono Wako?”

“Ah! Sijambo kidogo.” Wakakaa kitako. Sungura akaenda akapika chakula, akawapakulia kila mtu mbalimbali. Kwa mzee Fisi akatia mifupa mingi. Fisi akafurah sana.

Walipokuwa wakila Sungura akatwaa mtungi akaenda kuteka maji. Huku nyuma simba akamwuliza Fisi, “Je, mzee Fisi hujui dawa?”

Fisi akamwambia, “Hivi bwana Sungura hajakupa dawa?”

Simba akanena, “La, hata sina habari kuwa ajua dawa!”

Fisi akamwambia, “Sungura ni mganga mkubwa bwana, kama hajakupa dawa fahamu kuwa anafanya kusudi.”

Simba akaudhika sana, akasema,

“wajua huyu Sungura si kitu. Yupo hapa sikuzote naye

hanifanyizii dawa!”

Mara sungura akaja na mtungi wake, akamimina maji, akaenda tena kisimani Na huku nyuma maongezi ya Simba na Fisi yameshika juu ya Sungura. Hata Sungura alipokuja tena na mtungi wake Simba hakuweza kustahimili. Akamwita” Sungura!”

Sungura, Akaitika, “Lebeka bwana.”

Akamwambia, “Ati wewe wajua dawa ya vidonda? Mzee fisi ameniambia kuwa wewe unajua dawa. Na wewe upo hapa siku zote hizi hata hunifanyizii nikapona mkono wangu?”

Sungura akanyamaza kwanza akiwaza maana alifahamu kuwa hii ni fitina ya fisi, anamhusudu kwa ile mifupa.

Simba akamuuliza, “Je sungura, mbona kimya?”

Sungura akasem, “nawaza bwana, maana dawa yenyewe ina udhia, ndiyo maana nisikuambie tangu zamani.”

Simba akamwambia, “udhia gani? Sema tu, mimi natak kupona.”

Sungura akasem, “Ee bwana wanfu, mimi nakumbuka wazee wangu waliniambia dawa ya kidonda kam hiki chako, hapana dawa ila ipatikane ngozi ya mgongoni mwa fisi, ufunhiwe jeraha, utapona.”

Simba aliposikia vile hakisaili tena, akamrukia fisi. Akampanda mgongoni na kumrarua ngozi yote ya mgongoni. Fisi akakimbia akaenda zake, simba akapata ngozi kisha akampa sungura, akamwambia, “haya fanya uganga wako.”

Sungura akaitwaa, akaikata sawa na jeraha na kuifunga hodari. Hata muda wa siku mbili tatu, mzee simba akajiona yu hai kabisa. Akajua kweli sungura mganga. Sungura akapata kibali kwa simba. Lakini fisi akapata hasara, ndiyo maana hata sasa ukimtazam fisi utaona manyoya yake mgongoni marefu, maana yaneota katika kovu.

FIKIRINI NA HEMEDI

Hapo kale katika nchi ya Pate palikuwa fundi mmoja mshona cherehani. Alikuwa na kiwanda chake, na wanafunzi hawapungui ishirini. Na katika wanafunzi hawa alikuwako mmoja anaitwa Fikirini. Huyu alikuwa mtu mmoja mzuri sana, tena hodari Wa kazi. Lakini alikuwa na hitilafu moja, alikuwa majinuni kidogo. Kuna wakati hufanyiza kazi sana na kuna wakati hushikwa na bumbuazi, akanyamaza kimya wala hafanyi kazi. Ikawa hali yake namna hii, hata bwana wake akamjua kuwa ndiyo hali yake. Na Huyu Fikirini alikuwa mtu mzima sana kwa sura, tena alikuwa mtu mmoja nadhifu sana. Na akapenda kujiweka katika daraja kubwa kubwa, hata pengine hujishugulisha na mtoto wa Sultani kwa makuu yake.

Hata akitembea njiani huvaa nguo vizuri na kilemba, na watu wakimwamkia huitikia kisultani kwa kichwa na mikono. Hata watu wote wakajua kuwa Fikirini apenda sana fahari ya Usultani. Akawa na mawazo yale hata yakamjaa moyoni. Mwisho akaona dhiki kukaa pale mjini kwa kuwa watu hawampi

heshima ya mwana wa Sultani. Basi akaazimu kutoka katika nchi ile kwenda nchi nyingine watu

watakakomdhani kuwa ni mwana wa Sultani. Lakini kabla hajaondoka, siku moja Sultani wa nchi ile nguo zake anazovaa siku ya rasmi, na siku ya baraza, ziliharibika kidogo, zikahitaji kutengenezwa kwa kushonwa kidogo. Basi zikapelekwa kwa, fundi mshoni. Kwa bahati zikapelekwa katika kiwanda kile kilekile cha fundi wake Fikirini.

Na yule fundi akatwaa zile nguo akampa Fikirini kushona. Hata usiku walipokuwa watu wote wameondoka kiwandani, Fikirini akazitwaa zile nguo akazitazama, akafurahi akacheke moyoni mwake akasema, “Hii ndiyo bahati yangu, nguo hizi nikivaa mimi nitakuwa mwana wa mfalme kwelikweli.”

Basi yalipomjia mawazo haya akaondoka akasafiri kwenda nchi ya Mbali. Na alipofika katika nchi ya ugeni akavaa nguo zile. Na watu walipomuona wakadhani kuwa ni mwana wa mfalme bila shaka. Naye Fikirini mwenyewe hakujitupa, akiwa karibu na mji hupeleka habari kama mtoto wa Sultani anakuja na watu huenda kumlaki kwa sherehe. Lakini watu wakistaajabu kwa kumuona anakwenda kwa miguu.

Basi wengine wakamuuliza kuwa, “kwa nini kwenda kwa miguu naye ni mwana wa mfalme?”

Naye akajibu kuwa anapenda tu. Hata usiku alipolala akawaza akaona kweli amepngua neno maadam hana farasi. Basi asubuhi kulipokucha akafanya shauri kununua farasi. Alikuwa na akiba yake reale miteen, akatoa reale mia akanunua farasi mzee asiyeweza kumwangusha. Akawa anasafiri kwenda mji mwingine, njiani akakutana na mwana wa Sultani kwelikweli, jina lake Hemedi.

Na huyu Hemedi naye hakuwa na mtu alikuwa yeye peke yake na Fikirini naye peke yake. Fikirini akaanza kumuuliza Hemedi, “habari zako, anakwenda wapi?”

Hemedi akajibu, “Ah! bwana wangu, sijui ninakokwenda, napotea na dunia tu.”

Kisha Hemedi akamwuliza, Fikirini, “je, wewe unakwenda wapi?”

Akamwambia, “Na mimi vivy hivyo bwana wangu, sijui niendako.”

Basi wakatoa vyakula vyao wakala, na farasi wao wamewafunga. Kisha wakawa wanazungumza. Fikirini akamwuliza Hemedi, “Je! rafiki yangu ulikuwa unakusudia kwenda wapi?”

Akamwambia, “Mimi natoka Guba kwa Sultani Umeya bin Azuwan, na huyu Sultani Umeya amekufa Na wakati alipokuwa akifa akaniita akaniusia. Akaniambia, ‘Hemedi.’ Nikamwambia, Naam!”

Akaniambia, ‘Njoo karibu yangu.’ Nikaenda karibu yake nikakaa. Akaniambia, ‘Tazama Hemedi! Wewe si mtoto wangu. Wala Si mjukuu

wangu, wewe ni mtoto wa Sultani mkubwa sana Wa nchi ya Baghdad, Na asili ya kuja huku kwangu ni hii. Siku uliyozaliwa wewe baba yako alikwenda Kwa watu wenye elimu kutazamia Akaambiwa, Mtoto wako mtoe katika nchi yao maana wamo maadui waliomkalia mtoto kwa jicho la uhasidi. Mwondoe katika nchi yako mpeleke katika nchi ya Sultani mwingine, Huko kwa Sultani mwingine aende akakae kwa muda wa miaka ishirini na moja. Na siku ya ishirini na mbili ya mwezi wa Ramadhani iwe ndiyo siku ya kufika kwa wazee wako, Na ninakufa, na ile siku iliyoagizwa na baba yako sasa sasa iko karibu. Na baba yako alinipa jambia hili akasema, Siku utakayomleta mwanangu, mlete katika mnara mkubwa katikati ya mbuga chini ya mlima wa Baghdad. Toka hapo mpaka Baghdad ni mwendo wa siku nne.'

”‘Akanipa na jambia hili nikupe ushike mkononi liwe ndiyo alama yako. Basi sasa shika jambia hili ukae nalo hata ukiona zimebaki siku tano ondoka uandame njia, na ukifika mahali ukiona watu wamejaa tele mahali penye mnara toa jambia hili ndani ya ala, mpe mkubwa wa hao watu useme, Mimi ndiye Hemedi bin Sultani. Na watu watakujibu, Alhamdulillah, Mwenyezi Mungu amekulinda hata sasa umefika mkononi mwetu.‘Haya ndiyo tuliyoomba.’”

Wakalala. Na yule Hemedi hakuwa na wasiwasi akajua kama rafiki yake kamuuliza habari kamweleza, basi. Kumbe! Fikirini hakupata usingizi siku ile.

Akawaza mengi. Hata mwishowe akaona hapana njia ila ajifanye yeye kuwa ndiye Hemedi awe mwana wa Sultan kabisa. Basi akafanya hila akamnyang'anya Hemedi jambia lake, wakati huo Hemedi kalala. Akamchukua na farasi wa Hemedi akapanda akaenda zake usiku huo huo.

Hata asubuhi Hemedi alipoamka akaona farasi wake hayupo, na jambia limechukuliwa, na Fikirini hayupo. Hemedi akajua kuwa hii ndiyo kazi ya Fikirini. Fikirini akaenda zake siku ya kwanza, ya pili, ya tatu, akalala karibu na ule mnara wa Baghdad. Asubuhi alipoamka akaona watu wengi sana, wengine wamepanda ngamia, wengine farasi, wamevaa nguo nzuri nzuri. Fikirini naye akavaa zile nguo zake za ufalme, akavaa na lile jambia la Hemedi, amepanda na farasi wa Hemedi. Alipowaona watu akamtoa kasi farasi wake.

Akafika pale walipo watu, akapiga, Salaam aleikum! Watu wakitikia, aleikum salaam. Mara akalitoa jambia akampa mzee aliyesimama sawasawa na lango la mnara Na huyu mzee alikuwa ndiye baba yake Hemedi. Baba mtu alipoona jambia akasema, “Alhamdulillah.”

Mara zikaamrisha ngoma nyingi zikapigwa. Na Sultani akamtwa Fikirini akampakata

Na watu wakashika kusema, “Bwana Hemedi amekuja, amekuja!”

Walipokuwa katika sherehe hii, mara wakamwona mtu amepanda farasi anakuja kasi. Na Fikirini alipomuona akajua kuwa ni Hemedi. Basi akaanza kuwaambia watu ya kuwa yule anayekuja ni mwongo, wala msimsadiki lolote atakalosema, na bado akili zake si barabara, ana wazimu kidogo.

Mara Hemedi akatokea.

Akaja moja kwa moja mpaka mbele ya Sultani akamwangukia, akalia. Akamwanibia, “Mimi ndiye mwanao baba, huyu siye.” Mara Sultani akatoa amri aondolewe mbele yake, akasema, “Mwondoeni, ana wazimu.”

Hata alasiri saa tisa wakafunga safari kurudi mjini Baghdad. Fikirini akapandishwa farasi mwingine mzuri sana mwenye matandiko ya dhahabu. akatangulia mbele pamoja na Sultani. Na Hemedi maskini amefungwa yuko nyuma amepandishwa juu ya ngamia. Safari ikashikana. Njiani kila mji waliopita watu wakampa Fikirini zawadi kama desturi ya masultani.

Walipokuwa karibu na Baghdad, Sultani akatuma watu waende nyumbani kwa Bibi wakampe habari kama mtoto atawasili kesho. Basi mji ukapambwa na nyumba ya Sultani ikapambwa sana. Asubuhi watu wakaingia mjini.

Sultani akatangulia akaenda akakaa katika chumba cha baraza, na mkewe naye akaja akakaa ili amuone mwanawe. Basi wageni wakaingia katika mji kwa sherehe na ngoma. Walipoingia ndani, Sultani akamwambia Fikirini, Nenda ndani kamwamkie mama yako. Akaenda. Mke wa Sultani akamtazama sana Fikirini akasema, “Mimi mtoto wangu namjua sana, ijapokuwa amepata miaka ishirini na moja hawezi kunipotea.” Alipompa

mkono, mke waSultani akaupokea, lakini akasema, “A-a-a, huyu si mtoto wangu kabisa.” Watu wote wakanyamaza kimya. Na Fikirini naye hana la kusema, uso umeanguka chini. Mara Hemedi akatoka mahali alipokuwa akawasukuma watu akaingia mpaka ndani alikokuwa mama yake. Akaanguka chini akalia sana kwa kupiga kelele, “Ee jamani msisikilize huyu, mnyang'anyi huyu!”

Na mke wa Sultani naye akishika vile vile, “Huyu ndiye mtoto wangu Hemedi.” Lakini Sultani hakukubali maneno haya, akaamrisha Hemedi aondolewe, akamchukua mtoto wake Fikirini akapanda juu orofani.

Mke wa Sultani akakasirika sana, akasema, “mimi na mume wangu hatujagombana tangu kuoana, na sasa na yeye pia amekasirika kwa neno hili, lakini haidhuru mimi najua desturi yake, nitamwendea kwa wakati mzuri nikampe shauri langu.”

Mke wa Sultani alikuwa mtu mzima, naye ana akili sana basi akawaita wanawake anaokaa nao nyumbani mwake akawauliza je nini shauri lenu katika habari hii? Akatokea mwanamke anaitwa Tamasha akasema, “Tazama, bibi, katika maneno ya Hemedi alipokuwa akisema nawe, kasema kuwa yule mwenzake ni fundi mshona cherehani, Basi kama ni kweli mtake Sultani apate kuwajaribu vijana hawa maana atajulikana aliyekuwa fundi.”

Mke wa Sultani akaona ni shauri jema. Akaenda kwa mumewe akamwambia, “mume wangu nisamehe kwa maneno niliyosema jana.”

Mumewe akamwambia “nimekusamehe mke wangu.” kisha akamwambia, “bwana naomba kila nitakalokuambia, maadam mimi na wewe tunashindana kwa habari ya hawa vijana napenda kuwajaribu, jana tumesikia yakuwa huyu unayemshika wewe kuwa bin Sultani kazi yake ni kushona cherehani. Basi wape kazi ya kushona niwatazame.” Sultani akakubali. Zikaletwa cherehani mbili na zana za ushonaji zote, zikatiwa katika vyumba mbalimbali Sultani akawaambia wale vijana, “tazameni wanangu, nasikia ya kuwa ninyi mwaelewa kazi ya kushona. Basi napenda mnishonee joho kila mtu kwa ufundi wake.”

Fikirini akawaza moyoni ya kuwa kushona ni kitu gani! Ni mchezo tu kwangu. Nitashona joho hata watu wastaajabu. Lakini yule Hemedi

ameshangaa, maana hajui. Wakapewa vitambaa.

Fikirini akashona joho lake vizuri kwelikweli. Hata Sultani na mkewe walipoliona wakashangaa. Walipokwenda kutazama kazi ya Hemedi wakakuta vitambaa vizima havikukatwa Alipoulizwa, akasema, “Sijui mimi, maana kushona cherehani Si kazi ya mtoto wa mfalme.”

Mkewe akamwambia, “Je! Bwana sikukuambia miye, mtoto ni huyu asiyejua kushona.” Lakini Sultani hakukiri bado. Wakakaa, hata baada ya siku chache Sultani akajaribu vingine.

Katika mji wao kuna mahali watu walipokuwa wakiomba, napo ni makaburini, kwa wazee wao. Basi Sultani akaenda hapa, akasema na babu yake aliyekufa, akamtaka amsaidie katika neno hili ampe mwangaza kidogo.

Akakaa kidogo mara akaona mbele yake visanduku viwili vya lulu, na visanduku hivyo vyote sawasawa. Vyote vimeandikwa juu. Kisanduku cha kwanza kimeandikwa Mali na bahati, na cha pili kimeandikwa. Heshima na dola. Ikatoka sauti ikamwambia. “Chukua visanduku hivi hata nyumbani, ukakusanye watu wengi, uwaite na hao vijana kila mtu achague chake, baada ya hayo utamjua yupi mwanao.”

Siku ya pili Sultani akakusanya watu wakajaa baraza tele, vikaletwa vile visanduku vikawekwa juu ya meza.

Kisha wakitwa wale vijana mmoja mmoja. Akaitwa Fikirini kwanza, akaambiwa, “Baba nimetaka kukupa zawadi ya kisanduku. Basi chagua kimoja katika visanduku hivi.”

Fikirini akasoma kwanza juu na akuchagua kile kilichoandikwa Mali na bahati. Sultani akasema, Marahaba, na kikae hapa kwanza. Kisha akaitwa Hemedi, naye akaambiwa maneno yale yale aliyoambiwa Fikirini. Hemedi naye akasoma kwanza, akachagua kile kilichoandikwa Heshima na dola, maana yeye mtoto wa Sultani mali na bahati hana haja navyo. Halafu akaitwa Fikirini akapewa kisanduku chake, na Hemedi naye akachukua chake. Lakini kabla hawajaondoka vile visanduku vikafunguka vyenyewe. Ndani ya kisanduku cha Fikirini mna zana za ushonaji, na ndani ya

kisanduku cha Hemedi mna taji. Sultani akaitwaa ile taji akamvika Hemedi. Na yule haini akazomewa na kupigwa, mwisho akafukuzwa katika nchi ile.

Akatoka na kile kisanduku chake na farasi wake mzee akarudi kwao kwa aibu. Mwizi wa ajabu huyu, watu huiba vitu, yeye akataka kuiba ufalme! Alipofika katika nchi yake, akarudia tena ufundi wake wa kushona. Wenzake walipomuona wakamcheka sana. Lakini bwana mwenye kiwanda hakupenda kumweka tena kiwandani pake, akamfukuza. Akaenda zake akauza kile kisanduku chake akapata fedha akanunua nyumba mali yake, akanunua na cherehani yake. Akakaa kitako akifanya kazi yake ya kushona.

KISA CHA WADIGO

Hapo zamani palikuwa na wadigo waliokuwa wakija Mvita kutembea, au kuja kuuza vitakataka vyao. Hata siku moja wakupita mahali wakaona wamekusanyika watu wengi. Kumbe ni msikiti, na wale watu wakisali, maana ilikuwa Sikukuu.

Basi wale Wadigo wakasimama kutazama, wakiona ni faraja kubwa vile, watu wakiinama na kuinuilka. Hata ikajiri kuulizana, “pana nini hapa? Amekufa mtu?” Mdigo mmoja akawaambia wenziwe, “Mambo haya si leo tu, lakini kila siku watu hawa hucusanyika hivi wakifanya vivi hivi.”

Karibu yao alikuwako mtu aliyetaalamu akawaambia, “Watu hawa wanasali, wanamwomba Mungu.”

Wale Wadigo wakajibu, “Eee! Ndiyo kuomba Mungu huku?”

Wakatoka wakaenda zao. Wale wengine wakafanya kusahau habari ile, ila mmoja katika yao ikamkaa sana moyoni. Hata jioni akawa anazungumza na wenziwe, asema, “Hawa Wajomba (Waswahili) nikiwaona kila siku wamekusanyika. Pamoja wanainama na kuinuka, mnajua wanachofanya?”

Wenzake wakanena, “Hatujui.”

Asiwaambie neno. Hata siku ya pili wakafunga mizigo yao tena wakaenda mjini kuuza. Majira ya kurudi wenziwe wakarudi, yeye asirudi. Hata jioni akafanya taratibu, akasogea mpaka panapo dirisha, la msikiti akajibanza. Akawaona watu wanaingia, wanatawadha, wanasimama, na kufunga sala na kwenda rakaa. Kisha akamsikia yule Imam aliye mbele kuliko wote anasali. Na watu wanaitikia, Amin. Lakini maneno yanayosemwa hayajui. Hata watu walipokuwa wakitoka, naye akaondoka akaenda kwa nduguye mwanamke aliyekuwa akikaa mle mjini. Akamuuliza akamwambia, “Ndugu yangu, niambie kweli, watu wale wanaokusanyika mle nyumbani hufanyiza nini?”

Akamwambia, “Wanamwabudu Mungu.”

Akalala, asubuhi akaenda zake. Alipofika kwake hakuwahi hata kula chakula kwa wasiwasi mwingi. Akaagiza mtu kumwita mjomba wake. Alipokuja akamwambia, “Mjomba, sisi tunakaa ujingani.

Akamwambia, “Kuna nini baba?”

Akamwambia, “Wewe unapokwenda mjini huwaoni watu wanaokusanyika ndani ya nyumba kila siku?”

Akanena, “Nawaona.” Akamwambia, “Basi watu wale humwomba Mungu, nao wanapata vitu vyote vizuri, vyakula, nguo, ndiyo maana unawaona watu wa mjini hawana kazi. Basi kesho nataka uwahimize watu wote waende mwituni wakakate miti tupate kujenga nyumba ya Mungu.”

Nao wasikasiri, wakaenda kwa umoja wao wakakata miti wakaleta.

Hata alasiri waanza kuchimba mashimo. Siku ya pill na ya tatu kazi ikashikana mkono kwa mikono, hata siku ya nne kazi imekwisha. Wakangoja ifanye kukauka kwanza. Basi katika siku hizi za kungoja msikiti ukauke yule mwenyewe Hamisi Mchinondo haishi kwenda Mvita kutazama watu wanavyofanya.

Tena akamwuliza yule nduguye mwanamke kama watu hawa wanaosali hupata nini hasa. Nduguye akamwambia, “Hupata thawabu na pepo. Na wewe sasa hapo ulipo ii Islamu, yafaa usilimu, ndipo mambo yako yatakwenda vema.”

Basi akakubali kusilimu, akaitwa mtu akamtia maji ya tohara, akamsilimisha akamwita jina lake Salehe bin Oman.

Nduguye akamnunulia kanzu, na kisibao cha kwapa, na kofia, na fimbo ya mtobwe, na viatu. Alipokwisha vaa vitu hivi Salehe bin Oman akarudi. Alipofika kwao akawaita watu akawaambia, yeye si Hamisi Mchinondo sasa ila Salehe bin Omari, maana kasilimu. Akafanyiza karamu akachinja ng'ombe akawakirimu watu.

Kisha akawaambia, “Ndugu, mimi nimeona tunapotea bure, ni heri na sisi tuabudu Mungu. Maana mnawaona wale wenzetu wajomba, wanaabudu Mungu tu, kisha wanapata yote wanayotaka, basi na sisi ni afadhali tufanye kama vile. Na mimi nitakuwa mbele nitakalosema lolote itikieni, Amin.”

Siku ya kwanza akaja Bwana Saleh bin Omari na kanzu yake. Akasimama panapo kibla akaanza kusalisha, na maneno aliyosema ni haya. Nchisali nasalia tumwa, chinuka chibiru china nluma. Maana yake; nikisali nasalia utumwa, nikiinuka kiuno chaniuma. Na watu huitika amin. Ikawa kuinama na kuinuka maneno hayohayo. Msikiti ukasitawi, watu wakazidi kujaa. Wakasali hivi kwa miaka.

Hata mwaka mmoja mvua ikanya kwawingi sana. Hata upande wa kibla wa msikiti ukabomoka kwa ile mvua kukawa wazi. Hata wakati wa kusali sala za Isha Imam akaenda zake panapo kibla akaanza kusalisha kwa maneno yake yale yale. Nchisali nasalia tumwa, chinuka chibiru china nluma. Watu wakaitikia, Amin, kama desturi. Mara ya kwanza wakaenda rakaa moja, hata wakaenda rakaa ya pili. Mara chui akaingilia pale palipobomoka, akaja akamkamata yule Imam. Na penye kibla ni ndani kidogo napo pana giza, nayo imekuwa magharibi, watu wameshughulika na sala hawakumwona chui.

Basi Imam akaanza kupiga kelele, “Alumee!” Watu wakadhani ni maneno ya sala, wakaitikia, amini.

Alumee! Wao wanaitika, “amin.”

Alumee nenda! Amin.

Alumee nenda na tsui(chui)! Amin!

Alumee msihende(msidhani) mzaha! Amin.

Alumee nafa! Amin.

Alumee ndzoni(njoni)! amin.

ya sala wakitikia, Amin Alume, wao Amin. Alume nenda! Amin! Alume nenda na tsui (chui)! Amin! Alume msihende (msidhani) mzaha! Amin! Alume nafa! Amin! Alume ndzoni (njoni) Amin!

Ikawa hivyo, na Imam Saleh bin Oman achukuliwa na chui. Hata watu wakitazama panapo kibla hawaoni mtu, Imam hayupo. Wakaenda kuangalia waona damu tu, wakafuata alimopita, lakini kwa kuwa ni usiku hawakuweza kwenda mbali. Wakalala hata asubuhi. Asubuhi wakafuata wee wakatafuta maiti imebaki kichwa tu, wakakichukua kichwa wakaja nacho mjini, wakakizika.

KISA CHA MTU NA WANAWE

Palikuwa na mtu mmoja akaoa mke, akazaa watoto watatu wanaume. Na yule mtu hakuwa na kitu, rasilimali yake ilikuwa reale thelatha mia nazo kaziweka chini ya maliwato. Akakaa hata akapatwa na ugonjwa wake akafikiri kuwa mimi nina watoto watatu na mke hawa ndio warithi wangu na fedha hii haiwatoshi hawa. Afadhali niwarithishe kwa akili, kila, mtu asijue kuwa nimemrithisha mwenzake. Akamwita mke akamwambia, “Bibi, mimi siwezi, uhai wangu haba kuliko mauti na akiba yangu ni reale thelatha mia, na warithi ni wewe na wanao. Lakini nataka watoto wasirithi, sharti kwanza wakamrithi Sultani wa Mrisi (Mauritius), wakirudi huko ndipo warithi fedha.”

Akakaa, hata hatimaye akamwita mwanawe mkubwa, akamwambia, “Mwanangu, mimi siwezi, naona uhai ni haba, na mauti mengi, lakini nikifa, mimi rasilimali yangu ni reale thelatha mia tu, nazo ziko chini ya maliwato, huo ndio urithi wako, wala usiwaambie nduguzo. Lakini nakutafadhalisha neno moja, usirithi kwanza mpaka uende ukarithi mali ya Sultani wa Mrisi.”

Akakaa, akamwita mwanawe wa pili, akamwambia maneno kama yale aliyomwambia mwanawe mkubwa. Kisha akamwita mwanawe wa tatu, akamwambia maneno kama yale aliyowaambia wengine kwa siri.

Basi tena akawaacha kila mmoja anajishuku kuwa mimi napendwa kuliko wengine. Hatimaye baba yao akafa, wakamzika, wakakaa matanga wakaisha. Walipokwisha, yule mkubwa akaondoka usiku akaenda hata chini ya maliwato akafukua akazona kama aliyosema baba yake, akazichukua. Na yule wa pili akaenda kufukua asizione, akaudhika sana, akasema, Kumbe baba kanihadaa Akarejea nyumbani. Na yule wa tatu vile vile akaenda akafukua asione kitu, akaudhika sana, akasema, Kumbe mze kanihadaa ila kwa hakika fedha ilikuwapo sijui aliyekwiba. Akarejea nyumbani akalala.

Hata asubuhi akawaambia wenziwe, “hamna habari? Baba aliniambia ya kuwa penye maliwato pana fedha reale thelatha mia. Nami nimekwenda tazama, sikuona kitu.”

Na yule wa pili akasema vile vile, na mkubwa naye akasema vivyo hivyo. Yule mdogo akanena, “Lakini baba alisema tena fedha hii isirithiwe mpaka tukamrithi Sultani wa Mrisi. Basi aliyechukua yote ni batali, maana hakushika usia.”

Basi wakapatana wote kutoka kwenda kumrithi Sultani wa Mrisi. Wakatengeneza mikate yao, na bisi, na vibuyu vya maji, walipokuwa tayari wakaondoka, mkubwa mbele, wa pili kati, mdogo nyuma.

Na vijana hawa walikuwa wamesoma vema sana wote watatu. Basi walipokuwa katika kwenda yule mkubwa akaona unyayo wa mnyama. Akasema, “Unyayo wa mnyama huu, na mnyama mwenyewe ngamia.”

Wapili akasema, “Na ngamia huyu katwikwa pau za chuma.” Wa tatu akasema, “Na ngamia mwenyewe amepita zamani yapata saa nzima.”

Wakaenda hata mbele wakakutana na mtu, akawauliza, “Je! wakina bwana, hamkunionea mnyama wangu?” Mkubwa akajibu, “mnyama gani? Ngamia, nini?”

Mtu akajibu, “Naam, ngamia.”

Wa Pill akasema, “Na ngamia mwenyewe ametwikwa pau za chuma?”

Akaambiwa, “Ndiye hasa.”

Wa tatu akasema, “Na ngamia huyo kapita zamani, yapata saa nzima?”

Yule mtu Akajbu, “Naam, ndiye.”

Wakasema, Tumemwona hukoo.

Wakashika njia wakaenda zao.

Hata mbele chini ya mti wakaona alama. Mkubwa akasema, “Kitako hiki, nacho cha mtu.”

Wa Pili akanena, “Na mtu huyu mwanamke.”

Wa tatu akanena, “Naye ana mtoto mgongoni.”

Walipofika mbele wakakutana na mtu.

Akawauliza, “Je, wakina bwana, huko mnakotoka hamkunionea mtu wangu?”

Mkubwa akajibu, “Mtu mke, nini?”

Akaambiwa, “Naam.

Wa pili akasema, “Ana kekee ya dhahabu?”

Akaambiwa, Eh! bwana mdogo.”

Wa tatu akanena, “Ana mtoto mgongoni?”

Akajibu, “Hasa.”

Wakanena, Huyoo! tumemwacha huko. Wakaenda zao.

Hata mbele wakamkuta mtu amechinjwa, hana kichwa, kimebaki kiwiliwili tu.

Mkubwa akasema, “Mtu huyu kachinjwa, naye mwanamume.”

Wa pili akasema, “Naye ana sharafa ya ndevu.”

Wa tatu akasema, “Mtu mwenyewe kizee, umri wake yapata miaka sabini au themanini.”

Wakaenda hata mbele wakakutana na mtu, naye ni mwanawe yule aliyechinjwa. Akawaambia, “Je! Wakina bwana hamkunionea mtu wangu huko mtokako?”

Mkubwa akasema, “Mtu mume, nini?”

Akaambiwa, “Naam.”

Wa pili akasema, “Naye ana sharafa njema ya ndevu?” Akajibu, “Naam, ndiye.”

Wa tatu akasema, “Naye mzee sana, bwana, apata umri wake miaka sabini, themanini hivi?”

Akanena, “Naam, ndiye hasa.”

Wakanena, “Huyoo, anakwenda huko.

Kumbe yule mtu kwenda mbele amkuta mzee wake amechinjwa

Akanena, “kumbe! wale wamemwua mzee wangu.”

Na wale vijana watatu wakashika njia mpaka wakafika kwa Sultani wa Mrisi. Sultani akawakaribisha vizuri, akawapokea kwa mikono miwili Akawapa nyumba wakakaa. Hata kwa Siku ya tatu Sultani akataka kuwakirimu wageni wake. Akatuma mtu kwenda shamba kwa msimamizi kuchukua mpunga, na mbuzi aliye nona.

Ukaja mpunga ukatwangwa, na mbuzi akachinjwa. Ukapikwa wali mwema. Wakaenda wakitwa wageni kwa Sultani. Wakapewa maji wanawe ili wale chakula.

Mkubwa akasema, “Wali huu unawalakini.”

Wa Pili akasema, “Hata kitoweo kina Walakini.”

Wa tatu akasema, “Hata Sultani mwenyewe naye ana Walakini.”

Watwana waliosikia maneno haya wakaudhika, wakaenda wakamwambia bwana wao maneno haya, na ya kuwa hawakula chakula. Sultani akaudhika sana, akaona, vijana hawa hawana adabu. Juu ya kuwakirimu namna hii, bado wananitukana.

Akanena, “Kawaiteni hawa vijana.”

Wakaitwa wakaja akawaambia, “Namna gani hii mliyofanyiza ninyi? Mimi nimewakirimuni na ninyi mwanitukana?”

Wale vijana wakajibu, “Tumekutukanaje, Sultani?” Kabla Sultani hajawajibu mara yakaja mashtaka ya yule mtu mwenye ngamia njiani waliyekutana naye njiani. Akashtaki kwa Sultani ya kuwa watu hawa wamekwiba ngamia wangu. Na Sultani akawaambia, “Kwa nini ninyi mmekwiba ngamia wa huyu?”

Wale vijana wakanena, “Tumemwibaje, Sultani?

Ametuona naye?”

Mwenye ngamia akasema, “kwa sababu waliniambia alama zake zote. Basi wamezijuaje hao kama hawakumwona?”

Sultani akasema, “mmesikia basi jibuni sasa, mmezijuaje alama za ngamia, nanyi hamkumwona?”

Wakajibu hivi:

Mkubwa, “Mimi nilimjua huyu ni ngamia kwa nyayo zake ,nyayo za ngamia hupotea?”

Wa pili akasema, “Mimi nalijua kuwa amechukua pau za chuma kwa kuwa nyayo zake zilikwenda chini sana. Nikajua huyu kachukua kitu kizito, na hapana kizito kama pau ya chuma.”

Wa tatu akasema, “Mimi nalimjua kuwa alipita zamani, kwa kuwa nyayo zake zilikanyagwa, saa nzima, kwa kuwa nyayo zake zilikanyagwa na watu waliokuja nyuma na watu wenyewe tuliwaona njiani, huko nyuma kabisa lakini ngamia hatukumwona.”

Sultani akanena, “Hakika hawa hawakuiba ngamia wako nenda zako.”

Akaja yule mwenye mke naye akashtaki, akasema, “Bwana, hawa wamenichukulia mke wangu.”

Sultani akanena, “Mnasikia ninyi, kwa nini kuchukua mke wa watu?”

Wale wakanena, “Hasha, bwana, sisi hatukumchukua mke wa mtu.”

Mwenye mke akasema, “Mbona basi wameniambia alama zote za mke wangu, ikiwa hawakumwona?”

Mkubwa akasema, “Mimi naliuliza tu mtu mwenyewe mtu mke? Huko ni kuiba, bwana?”

Wa Pili ikasema, “Mimi nalijua kuwa huyu mwanamke, maana naliona kekee ya dhahabu kule alikokaa chini ya mti, lakini sikuigusa.”

Wa tatu akasema, “Mimi nalijua kuwa ana mtoto mgongoni, maana asingeondoka hana kekee yake, ila alimpa mtoto wake uichezea, ikamponyoka, mama yake hana habari.”

Sultani akanena, “Kweli maneno yao, hawakumwona hawa.”

Akaja Kijana aliyechinjiwa baba yake, akanena, “Hawa wamemchinja baba yangu.” Sultani akanena, “Jibuni ninyi, mmemuuaje baba yake huyu?”

Wale vijana wakanena, “Hatukumwua, bwana.”

Yule kijana akanena, “imekuwaje basi kunipa wasifu wake wote?” Mkubwa akasema, “alikuja huyu bwana kututuliza akina bwana mmenionea mtu wangu? Mimi nikamwambia mtu gani, bwana? Mtu mume? Akanena, naam, huko kuuwa bwana?”

Wa pili akasema, “Mimi nalimjua kuwa ana sharafa ya ndevu

kwakuona manyoya mengi kifuani, nikajua kuwa hakosi kuwa n sharafa ya ndevu, maana hii ni maujudi.”

Wa tatu akasema, “Mimi nalimjua kuwa ni mzee wa miaka sabini au themanini kwa kuona damu yake. Ilikuwa haina nuru tena, ina maji nikajua kuwa hii ni damu ya mzee.”

Sultan akasema, “Kweli maneno yao, hawakumwua hawa, nenda zako.”

Sultani akashangaa kwa akili zao wale vijana, lakini bado hawajajitaka. Imebaki habari ya Sultani mwenyewe.

Sultani akawaambia, “Ehe! Sasa nawauliza mimi, Kwa nini mkafanya wali wangu kuwa na Walakini, na mnbuzi kuwa na Walakini, na mimi kuwa na Walakini?”

Mkubwa akasema, “Mimi nimejua kuwa wali una walakini,

kwa kuwa mchele wake mrefu, mnene. Nikajua mpunga huu ulipandwa makaburini, maana ndipo penye rutuba sana. Basi chakula cha makaburini hakina Walakini?”

Wapili akasema, “Nalijua kuwa nyama ina Walakini kwa kuwa nyama yake ilinona sana, nikajua kuwa mbuzi huyu malezi yake si ya mbuzi wengine.”

Wa tatu akasema, “Mimi nimejua kuwa Sultani una Walakini, kwa sura.”

Basi Sultani akakasirika sana. Akamwita nokoa, akamuuliza habari za mpunga. Akanena, “Naam, bwana, mpunga huu ulipandwa makaburini, wala si uongo.”

“Na habari ya mbuzi je?”

Akasema, “Naam, mbuzi yule mama yake alikufa alipokuwa mdogo akanyonya maziwa ya punda!”

Sultani akaona kweli, mbuzi huyu kama punda. Kisha akamwita mama yake akamfunga panapo nguzo akampiga akamwambia, “Sharti uniambie kweli. Hawa wanasema mimi nina Walakini, namna gani? Wewe ndiye unayejua.”

Mama yake akamwambia Kweli, “mwanangu, wewe ni mtoto wa mume wangu wa kwanza aliyekuwa Baniani, si mtoto wa marehemu Sultani.”

Sultani akaona vijana hawa wana akili wala hawana mfano wao. Mahali pa kuwafunga akawapa zawadi nyingi, akawaruhusu kwenda zao. Lakini

pamoja na hayo ndani ya moyo wake hakutaka kuwaacha wale watoto warudi kwao wazima kwa vile walivyomfedhehi kumtambua kuwa yeye si mtoto wa marehemu Sultani.

Alitaka kuwaua, ila hakutaka kuwaua kwa dhahiri. Basi wakati wa kuondoka akatwaa majoho mekundu akawavika wote watatu. Kisha akatwaa majoho meusi akawavika wanawe watatu, akawaambia, “Nendeni muwasindikize wageni.” Akawaacha kwenda zao. Mara nyuma akatuma askari.

Akawaambia, “Nendeni zenu, wafuateni wale wageni, mkiwakuta, waueni vijana watatu wenye majoho mekundu.”

Kumbe! wale vijana walipokwenda mbele wakatambua kuwa pana neno hapa. Wakawaambia watoto wa Sultani wa Mrisi, ya kuwa, “Baba yenu ameharibu. Majoho mekundu ni rangi ya kifalme si majoho ya kuvaa sisi. Majoho meusi ni ishara ya msiba, ndiyo yanayotuelekea sisi tuliofiwa na mzee wetu karibu. Basi yafaa tubadili.”

Wakabadilisha yale majoho. Wale watoto Sultani wakavaa majoho mekundu. Na wale askari waliambiwa kuwa mkiwakuta wale vijana waueni wenye majoho mekundu.

Basi askari walipowakuta wakatimiza amri yao wakawauawenye majoho mekundu. Kumbe! ndio watoto wa Sultani. Na wale vijana watatu, wakawarudisha kwa Sultani. Sultani alipowaona wanakuja wamevaa majoho meusi, akajua kuwa werevu wao.

Akawapa tena malinyingi mno.

Wakatimiza maneno ya baba yao. Wakamrithi Sultani wa Mrisi kwanza, kabla hawajarithi mali ya baba yao. Kisha wakarudi kwenda kurithi mali ya baba yao.

HADITHI YA MTOTO WA SULTANI NA TAJIRI

Aliondoka Sultani, akafanya urafiki mkubwa na Tajiri. Sultani alikuwa na mtoto mume, na tajiri alikuwa na binti. Hata siku moja Sultani akamwambia tajiri, “Mimi naona shauri lililo jema ni kuwaoza watoto wetu, wangu na wako.”

Tajiri akasema, “Maadam unapenda wewe Sultani mimi nina hiari gani?”

Basi wakazatiti arusi. Sultani akamwambia tajiri, “Nataka tufanyize arusi, hata watu wakae wakikumbuka ya

kama hawajaona nyingine.”

Basi tajiri akatoka akaalika watu, walio karibu, Waliowahusu, ndugu, na majirani, na walio mbali, kusi na kaskazi, magharibi na mashariki. Watu wakaja hawana idadi. Akaambiwa Sultani kuwa watu wamekwisha kuwako. Basi ikafanyizwa arusi mwanzo siku ya Jumatano.

Karamu ikawa kubwa ajabu, mji ukawa hausikilizani kwa ngoma na furaha ya arusi. Asiye na mwana akaeleka jiwe.

Watu wakawa huria tena wa ndani nje, na wa nje ndani. Watu hawaoni, hawasikiani. Mizinga ikapigwa haina idadi, hata watu wakaziba masikio. Muda wa siku saba hapana apikaye wala apakuaye, wote chakula kwa Sultani na Tajiri. Baada ya siku saba binti Tajiri akapelekwa kwa mumewe. Wakakaa pamoja kwa miezi saba. Baada ya miezi saba mtoto Sultani akawaita watwana wake, akawaamrisha kuchimba shimo uani katika nyumba yake.

Akaondoka yule kibwana, akamchukua mkewe ili kwenda kutazama ile kazi ya shimo. Walipofika, mume akamwambia mkewe achungulie ndani atazame kama kumekaa vema, yule mume akazunguka kwa nyuma,

akamshika mabega, akamsukuma ndani ya shimo kwa nguvu, kisha akaenda zake.

Hata kwa siku ya pili akaja kumwangalia mkewe mle shimoni Akamwita, “binti tajiri.” Binti tajiri akaitika, “Lebeka.”

Akamwuliza, “Je, hujafa bado?”

Akamjibu, “Mimi sifi, ila nizae watoto wako watatu.”

Yule kibwana akamcheka sana, “akamwambia,

Utazaa wapi watoto wangu, nawe humo shimoni?”

Yule mume akarudi nyumbani.

Akaagiza makanda matatu ya mtama, na moja la mahindi, na kibuyu Cha maji na kumpelekea mle shimoni.

Ikawa kila siku anakwenda asubuhi na jioni, ili kumtazama kama amekufa.

Naye kila akimuuliza, “Je hujafa?”

Naye humjibu majibu yale yale.

Hata zilipotimia siku saba, mtoto wa Sultani akaona ya kuwa hafi huyu, akaaga ruhusa kwa baba yake asafiri. Baba yake akamruhusu. Akafunga safari yake, akachukua watu aliotaka,

na vitu alivyotaka, akaondoka. Alipofika nchi ya mbele, akaacha baadhi ya watu wake pale.

Yeye akaazimu kwenda nchi iitwayo Manga Komamanga. Huku nyuma kwa mkewe akaja buku na panya.

Wakamwuliza yule mwanamke, “Unafanya nini humu shimoni?”

Akawajibu ya kuwa “Haya ni ya uliwengu.” Wakamwambia, “ebu! Tueleze hayo masaibu yako.”

Yule mwanamke akanena, “Mume wangu ni mtoto wa Sultani, naye naliozwa kwa radhi za wazee, Baada ya muda wa miezi saba kupita akanitia humu shimoni ili kutaka kuniua bila sababu.”

Wakamuuliza, “Je kwenu, unakujua?”

Akanena, “nitakujuaje nami nimo ndani ya shimo?” Wakamwambia, “Je! Atokeapo mtu akakupeleka kwenu utampa vyakula hivi? (Yale magunia ya mtama na maindi).”

Yule mwanamke akasema, “atakayenipeleka kwetu, vyakula hivi vyote na atwae yeye.”

Buku na panya wakafanya jitihada ya kuchimba hata uvunguni pa kitanda cha mama yake yule binti tajiri. Walipokwisha wakaja wakamchukua yule mwanamke wakampitisha katika ile njia waliyoichimba mpaka uvunguni pa kitanda cha mama yake.

Hata yule mtoto akamwamsha mama yake. Mama yake akashtuka sana, akamwambia “nani wewe.”

Akanena, “mimi binti yako.” Akamwambia, “umepita wapi na milango yote imefungwa?”

Akamwambia, “mama, waniuliza hivyo, Kwani wadhani natokea nyumbani kwangu? Kaa kitako nikuelezee habari yangu, leo yapata mwezi tangu nimetoka kwa mume wangu. Yule mume amekuwa si mume ila balaa. Aliagiza shimo lichimbwe, kisha akanitumbukiza ndani. Naye akawa anakuja kunitazama ajue kuwa mimi mzima au nimekufa, alipoona nakawia kufa akanikimbia.”

Mama yake akajibu, “ah kumbe Safari ile ni kukukimbia wewe?” Kisha akamwita mumewe akampa habari hii yote.

Wakasikitika sana kwa habari hii, yule mtoto akasema, “sasa nisikilizeni mimi, kitendo nitakachomtenda mimi kitapita hiki alichonitendea mimi. nitafutieni chombo, mnipakilie mali kwa wingi, ila mabaharia nataka wanawake, na mavazi yao meusi, kisha mkipeleke kokoni.”

Yule mtoto mwanamke akapiga kipande, akatambua kuwa nikitoka hapa nitampata mahali kadha wa kadha, basi akaingia chomboni na watu wake, akasafiri muda wa siku kumi na mbili. Akapiga kipande tena, akaona ya kuwa muda wa siku sita atamtia mkononi

Hata siku ya tano Yule mtoto mwanamke akafanyizia mazingaombwe yake ikawa chombo cha mtoto wa Sultani kikapigwa na dhoruba asijue aendako, hata siku ya sita akamtia mkononi, wale mabaharia wa mtoto wa Sultani wakakiona chombo kimewakabili kinakuja kasi.

Wakamwambia bwana wao ya kuwa kuna chombo kinakuja, na yule mtoto wa tajiri kavaa kiume, kajifunga na silaha, kashika na mkuki mkononi, amesimama juu ya staha. Yule mtoto wa Sultani akasema, Loooh masalale! Jitu gani hili mwenda usiku kuamkia mchana! Chombo cha yule mwanamke kikapita kikatatongulia mpaka Manga Komamanga, ndiko alikokuwa akienda Yule mtoto wa sultani.

Yule mtoto mwanamke alipofika Manga Komamanga, chombo chake akakitia kokoni. Akaandika barua kwa sultani wa nchi. Sultani alipoisoma akapeleka watu wakaenda kumchukua Yule mwanamke.

Alipofika kwa sultani akamweleza sultani maneno yake, akamwambia nyuma yangu kunakuja mtu nami nina visa naye. Atakapofika hapa lazima atataka kuposa na mimi nataka unifanye binti yako, akija umwambie ya kuwa huna binti ila huyu, naye kaolewa chuo kimoja. Ukitengeneza habari hii nitakupa reale elfu.

Mara mtoto wa sultani akafika katika nchi ya Manga Komamanga, akatia nanga bandarini akapiga mizinga. Hata siku ya tatu akaenda kumwamkia Sultani wa Manga Komamanga. Akakaribishwa vizuri. Muda wa juma nzima kupita akaenda kwa Sultani kumposa binti yake.

Na Sultan hakukasiri, akamwambia, Mimi nina binti mmoja tu, naye kaolewa chuo kimoja.

Yule kibwana akakubali akanena, “niko tayari.”

Ikatengenezwa arusi akaoa.

Mume akaingia nyumbani. Akakaa muda wa mwaka, mkewe akazaa mtoto mwanamke. Baba yake mtoto akamfulia vyombo vya dhahabu ili pambo la mtoto. Na mwaka huu wote waliokaa pamoja yule mume hakumtambua mkewe, kuwa ndiye yule aliyemtupa shimoni.

Baada ya mwaka mtoto wa Sultani akaomba ruhusa kwa mkwewe, Sultani wa Manga Komamanga ili asafiri. Sultani akamwuliza, “Unataka kwenda wapi?”

Akamwambia, “Nataka kwenda nchi iitwayo Manga Pera.”

Akamkabidhi mkewe na mtoto, akasafiri. Na yule binti Tajiri akamwambia baba yake wa kupanga ya kuwa, “Na mimi nataka kusafiri nifike Manga Pera.”

Akamwambia, “Mume wako akirudi upesi akakukuta haupo je, nisemeje?”

Akamwambia, Haya ni juu yangu. Akatoka naye binti Tajiri katika chombo chake akasafiri. Wakakutana huko nje ya bahari. Binti Tajiri akampiga mtoto wa Sultani kwa mazingaombwe; akampita vile vile kama kwanza, akatangulia yeye kufika Manga Pera.

Alipofika akafanya kama yale aliyoyafanya Manga Komamanga. Na mtoto wa Sultani sababu ya kwenda katika nchi hii, ni kuoa binti Sultani. Basi alipofika hakukawia, akasema haja yake ya kuwa anataka kumposa binti Sultani.

Na Sultani akamwambia ya kuwa ana mtoto mmoja tu, naye kaolewa vyuo viwili.

Akaambiwa kama akihiari ataozwa. Akanena, nimekubali, Aakaozwa

Hata muda wa mwaka mkewe akazaa mtoto mume, akamfulia naye vyombo vyake akampa.

Kisha akaaga kwa yule mkwewe kuwa yeye anasafiri, anataka kwenda nchi iitwayo Manga Ndimu. Na binti tajiri aliposikia ya kuwa mumewe anakwenda Manga Ndimu, akamngoja aondoke naye akafunga safari

akaenda upande ule ule. Akafika yeye kama kawaida yake. Akafanya yale yale maana alifahamu ya kuwa anafanya inadi hii makusudi aje kumbugudhi binti Tajiri akiwa atamkuta hai. Na yule mwanamume alipofika Manga Ndimu akafanya kama yale yale aliyofanya nchi nyingine.

Akamwoa tena yule yule akazaa naye mtoto mwanamume.

Naye pia akamfulia vyombo vyake. Kisha akafunga safari kurudi kwake. Na mkewe na mtoto wake akawaacha kule kule (alivyodhani yeye). Maana anataka mtoto wake mpaka akue. Kumbe binti Tajiri akatoka naye, wakapishana baharini vile vile.

Na yule mwanamke kila nchi aliyopita akamchukua mwanawe.

Akafika mpaka mjini kwao. Punde si punde mtoto wa Sultani akaja. Ikawa furaha kubwa katika mji, mtoto wa Sultani amerudi Ikapigwa mizinga sana. Yule mtoto mwanamume akamweleza baba yake habari zote za safari. Na binti Tajiri naye akawaeleza wazee wake yote aliyotenda. Lakini akawaambia, Sina budi kwenda kukaa kule kule shimoni, mume wangu akija anikute.

Mtoto wa Sultani alipokwisha pumzika akaenda kule shimoni kumtazama mkewe. Akamwita,

“Binti Tajiri! Binti Tajiri!” Akaitikia, “Lebeka.”

Akamwuliza, “Je! u hai bado?”

Akamjibu, “Ni hai

bado, sikukuambia kuwa sifi mpaka nizae Watoto wako watatu?”

Akamwambia, “una wazimu! uzae wapi watoto wangu?Mwenzako huko nitokako nimeoa akina binti Sultani watatu na bado nimezaa nao, wewe utachelewa humohumo shimoni.” Akatoka Akaenda zake.

Yule binti Tajiri naye akatoka akaenda kwa wazee wake. Akawaambia wazee wake, Nataka mnifanyie karamu kubwa, niwaalike watu wengi

kama muezavyo. Nataka Sultani na mwanawe pia wahudhurie.
Wakafanyiza karamu kubwa, wakaalika watu wengi wakaja. Akaja na Sultani na mwanawe.

Wakakaa kila mtu kwa cheo chake. Watu wakala chakula, wakaisha.
Walipokwisha kula watu wakauliza, “Maana yake nini karamu hii?”

Yule binti Tajiri akasema, “Ngojeni nitawaeleza.”

Akaingia ndani, akawatwaa wale watoto wake watatu, kila mtoto amemvika lebasi ya nchi yake, na pambo alilofuliwa na baba yake, na kila pambo mbalimbali.

Akawaleta mbele ya watu.

Akawapitisha kwa watu wote ili wawaone. Kisha akawaambia, Sasa nendeni kwa baba yenu. Watoto wakajinadi wote: Mimi fulani bin fulani au bin fulani. Wakaenda mpaka alipo baba yao. Binti Tajiri akamwuliza mtoto

Sultani, “Je! watoto wa nani hao?” Mtoto wa Sultani akajibu, akanena, “Kwa dalili zote nawaona kuwa wangu.”

Wakaulizwa wale watoto mmoja mmoja walipozaliwa. Wa kwanza akajibu, “Mimi nimezaliwa Manga Komamanga.”

Wapili akajibu, “Mimi nimezaliwa Manga Pera.”

Watatu akajibu, “Mimi nimezaliwa Manga Ndimu.”

Binti Tajiri akawauliza, “Mama yenu nani? Wote wakajibu, Wewe, BintiTajiri.”

Akamwambia mumewe, “Je! sikukuambia, Sifi mimi mpaka nizae Watoto wako watatu?”

Mtoto wa Sultanu akanena, “Naam umenishinda, binti Tajiri.”

Wakakaa pamoja, mtu na mkewe raha mustarehe.

WEZI STADI

Hapo kale palikuwa na wezi wawili, mwizi wa mchana, na mwizi wa usiku. Huyu mwizi wa mchana akiiba Unguja, na huyu wa usiku akiiba Mrima. Wote wawili walikuwa mafundi wa wizi kupindukia. Siku moja yule mwizi wa Mrima akasema, Nitafanya safari niende zangu Unguja nikafanye kazi yangu huko, maana ndiko kwenye matajiri wengi.

Basi akanauli chombo akavuka, Akafanya kazi yake ya kuiba, na kila alichokipata akiweka pangoni. Kumbe! pango hili ni pango aliokuwa akikaa, na kuficha vyombo vyake yule wa Unguja. Lakini kwa kuwa mmoja wa usiku, na mwingine wa mchana hawakujuana, maana hawaonani. Wakakaa hali hii kwa muda wa miaka saba.

Hata siku moja yule mwizi wa mchana akasema, Leo nitapumzika siendi kuiba. Hata alasiri akatoka. Akatembeatembea mle pangoni, akamkuta yule mwizi wa usiku amelala.

Yule mwizi wa mchana akasema. Huyu amekuja kunifelisha mambo yangu, nitamuulia mbali. Akang'oa shembea lake ampige nalo dharuba moja. Lakini akasita. Hata mwisho akamshika mkono, akamwuliza, “Nani wewe?”

Yule mwizi wa usiku akaamka akitetemeka, “Mimi hapa bwana ah! nimetubu, siibi tena.” Akamwambia, “Mwizi wewe eh?” “Eh, bwana, bali sasa siibi tena, basi, nimetubu.”

Akamwuliza, “Tangu lini upo hapa wewe?”

Akanena, “Yapata miaka saba sasa. Akamuuliza, “Vitu ulivyokwiba viko wapi?” Akaenda akamwonyesha anakoweka vitu. Akaviona vitu vingi mno ajabu. Akasadiki kuwa huyu mwizi kweli. Aliposadiki kuwa mwizi kweli, wakashikana mikono, ukawa urafiki mkubwa. Walipokaa kitako kuelezana visa vya uwizi wao, ukaingia ubishi, Nani stadi wa kuiba. Kila mtu akasema, Mimi zaidi. Wakapatana kuonyeshana ustadi wao.

Akaondoka yule mwizi wa mchana akatwaa udongo akauviringa vidonge vidonge, akavipaka rangi ya lulu, akapita akitembeza. Ikawa hii ndiyo kazi yake kwa siku nyingi. Hatima ule udongo akautupa pwani.

Hata siku moja akajipamba sana, akapanda farasi, na kuweka watwana mbele na nyuma. Akaenda hata nyumba ya tajiri mmoja, akapiga hodi, akaitikiwa, Karibu.

Akaingia ndani akakaa kitako.

Akamwuliza yule tajiri, “Unazo lulu nzuri hapa?”

Yule tajiri akajibu, “Ninazo.”

Akamwambia lete, “zikaletwa lulu nzuri nyingi apate kuchagua mwenyewe.” Yule mwizi ikawa kazi kuzigeuza na kuzitazama zile lulu. Hata mwisho mwenye mali akachoka. Akamwambia, “Kama wewe unataka kununua lulu, nunua; la, hutaki, nipe niweke, maana nina kazi nyingine mimi.” Mwizi akamjibu, “Unasemaje? Unasema ukitaka nunua, kwani sasa za nani hizi?”

Wakagombana pale kikomo na kiasi, hatimaye wakachukuana sheriani. Walipofika sheriani, akitazamwa yule mwizi sura yake na lebasi yake, wakaona hakuelekea wizi.

Na zaidi kuliko hayo wakatokea watu walioshuhudia kuwa, Huyu ni mchuuzi wa lulu, siku kadha wa kadha amepita akitembeza lulu. Kadhi akampa haki mwizi, akanena, “Hizi lulu ni zake huyu.” Mwizi akaondoka akaenda zake.

Akamwambia yule mwizi wa usiku, “Unaona kazi hiyo?” Mwizi wa usiku akamwambia mwenziwe, “Unajuaje kuiba wewe ? ngoja nikuonyeshe kuiba.”

Akatafuta misumari yake saba, na nyundo na kenge, akajifanya maskini, Akaondoka akaenda hata mlangoni kwa Sultani,

akawakuta mabawabu wamejaa tele, wakamwuliza, “wataka nini?”

Akawajibu, “Nataka kazi kwa Sultani”

Wakamwambia, “leo hupati kumwona Sultani, labda kesho, maana umekuwa usiku tena Kwa hivi sasa lala hapa barazani mpaka kesho.”

Yule mwizi akatikia. “Ee walah.” Yule Sultani alikuwa na saa kubwa mno ya ajabu, ikipiga mji wote hutetemeka na watu hawasikiani. Yule mwizi akalala hata saa sita ya usiku akampeleka kenge wake kupeleleza. Watu wote wamelala wakati huu.

Basi akaitwaa misumari yake saba akaishika mkononi, na nyundo, akangoja mpaka ipige saa saba. Hata ilipoanza kupiga saa saba, ikipiga Ngool Naye akaukomelea msumari ukutani wakati ule ule ili watu wasisikie.

Ikipiga Ngoo ya pill, akaukomelea msumari wa pili. Akafanya hivyo mpaka yote saba ikaisha. Kisha akatumia misumari hii kuwa ndiyo ngazi ya kupandia. Akapanda hata juu chumbani kwa Sultani, akamkuta amelala yeye na mkewe. Akamvua Sultani

pete yake ya dhahabu, akamvua na Bibi kidani chake cha almasi aliyoivaa shingoni, thamani yake yatosha kununua usultani mzima.

Akatwaa na fedha zilizokuwa ndani ya makasiki azimwagamwaga, kisha akaenda zake. Alipofika kwa mwenzie akanwambia, “Unaona namna ya wizi, wewe unaonea maskini, mimi huiba kwa Sultani, na bado nitatenda zaidi kuliko hivi.”

Sultani alipoamka asubuhi, akaona pete yake haimo kidoleni, na kidani cha Bibi hakimo shingoni, na fedha zimemwagwa chekwachekwa. Akajua kuwa kulikuja mwizi mkubwa

Sultani akatoa amri mwizi huyu atafutwe. Tena mtu asitembee usiku, atakayeonekana anatembea ndiye mwizi. Yule mwizi aliposikia amri hii, akatwaa kikombe chake na rupia zake kumi na tano akaenda hata dukani kwa mshihiri akabisha.

Akaulizwa, “Nani wewe unayetembea usiku, hukusikia amri, Watu hawatembei usiku?”

akanena, “Ah! Nifanyeje nami nataka mafuta, nimeleta rupia zangu kumi na tano nataka kuweka rehani, kesho nitakuja kukomboa. Mshihiri

kusikia rupia kumi na tano roho ikamtoka. Akatoa mikono dirishani iii apokee.

Yule mwizi akaushika mkono akaukata. Akakimbia akaenda zake. Akaenda kwa mwenzie akamwambia, “Unaona? Bado, nitatenda kupita haya.” Akaenda kupika mikate mitatu, akatia kila namna ya kileo. Kisha akavaa kike, akachukua ile mikate akatoka.

Askari wakamuuliza, “Nani wewe?”

Akajibu, “Miye, akina Bwana.”

“Unakwenda wapi?”

Akanena, “Nimechukua mikate, maana naliweka nadhiri, pindi mume wangu arudipo salama, nitapika mikate nipeleke msikitini. Basi sasa nakwenda kuondoa nadhiri yangu. Lakini nadhiri yangu haina haja ya msikitini, hata mkila ninyi hufaa.”

Wale askari wakaitwaa ile mikate wakala, kabla hawajadiriki kwisha wakalewa wote, wakalala usingizi mzito. Yule mwizi akazichukua bunduki zote za askari, na panga zao, akaenda zake. Sultani aliposikia ya kuwa askari wameibiwa bunduki na panga zao zote, akaghadhibika sana. Akanena, “Huyu amekuwa si mwizi tena,

ila stadi. Akikamatwa au akijileta mwenyewe nitampa enzi bora.” Basi Sultani akazidi kuweka watu waulinde mji, na kuvizia ili wamkamate mwizi huyo. Na amri ya kutembea usiku ikazidi kuwa na nguvu.

Hata siku moja jemadari mmoja alipokuwa anazunguka usiku akakutana na huyo mwizi akamkamata. Akamwambia, “Leo Umefika, hutoki hapa. Wewe ndiye mwizi unayesumbua mji mzima.” Akautwaa mkono wake akaufunga pamoja na wake. Wakalala Hata usiku wa manane, watu wamelala akafanya jitihadi akafungua zile pingu. Akatwaa ule mkono wa

yule Mshihiri (maana alikuwa nao mfukoni) akaufunga kwa pingu pamoja na ule wa Jemadari, akaondoka akaenda zake.

Asubuhi yule jemadari alipoamka akaona mwizi hayupo, anaona kipande cha mkono amefungiwa.

Akanena sasa na atafutwe mtu aliyekatika mkono, maana ndiye mwenye mkono huu. Akapatikana yule Mshihiri akabanwa vikubwa. Akachukuliwa kwa kubururwa, na kupigwa, na watu wakimzomea

Yule Mshiriki akajaribu kusema, “Eh! jamaa siye mimi.” Akaambiwa, “Maneno gani hayo, mkono Wako si huu?”

Akanena, “Kweli, lakini

na mimi nimekatwa.”

Sultani akamhoji sana, akaona kweli, Huyu siye, “mwacheni,” nao wakamwacha.

Sultani, akanena, “Leo nitangoja mji mimi mwenyewe peke yangu.” Hata usiku Sultani akatandika farasi wake, akawa anazungukazunguka katika mji.

Yule mwizi anazo habari kama leo Sultani anangoja mji mwenyewe. Basi akaondoka kule pangoni, akavaa magunia akienda zake mpaka kwa Mhindi, akabisha hodi. Yule Mhindi akamwuliza, “Nani wewe?”

Yule mwizi akajibu, akanena, “Mimi hapa maskini, tangu juzi sijui riziki tumboni.”

Mhindi akamwambia, “Hukusikia amri kwamba watu hawatembezi usiku?”

Mwizi akasema, “Nifanyeje, nami hali yangu dhaifu, hata kama ningemwona Sultani mwenyewe ningemwomba anipe chakula tu. Na wewe kama hutaki kunipa chakula bure, nipe kazi nitende nipate chakula.”

Mhindi akamwambia, “Haya, pita ndani. Alipoingia ndani akampa ngano kusaga. Akamwambia, “Saga ngano hii mpaka asubihi, utapata thumuni.”

Akaingia akapewa ngano kuisaga, akawa anasaga ngano, na mlango akaacha wazi yule Sultani akawa anatembea katika mji.

Hata alipopita pale, akaona mlango wazi, na yule kizee anasaga. Sultani akanena, “Nani wewe? Mbona miango wazi hivi?”

Mwizi akasema, Kweli, mjukuu wangu, mbona na wewe unatembea usiku hivi?”

Sultani akasema, “Mimi nakuuliza wewe mbona kuacha mlango wazi?”

Mwizi akasema, “Eh! mjukuu wangu, mimi nakuhofia wewe unayetembea usiku, si uzuri

Baba, hukusikia amri?”

Na Sultani akanena, “Kweli hayo, lakini mbona kuacha mlango wazi na mji umengia wezi siku hizi?”

Mwizi akasema, “Kweli na hivyo, sasa hivi kapita mmoja, kaenda huku.” Mara yule Sultani akashika njia kumfuatia yule mwizi. Akamtafuta asimwone,

Akarudi pale pale akamkuta kizee anasaga ngano vile vile.

“Je? Baba umemwona?”

Sultani akanena, “Sikumuona.

Mwizi akasema, “Nadhani umesikia vishindo vya farasi amekwenda upande huu.”

Basi Sultani akamfuata tena asimwone. Akarudi tena pale pale Yule mwizi akanena, “Wajua Sultani, mwizi huyu atakuudhi.

Ampita hapa sasa hivi amekwenda huku. Lakini sasa nitakupa shauri. Huyu farasi nipe mimi, na hizi nguo nipe mimi. Twaa haya magunia yangu uvae, hatakawia, atakuja sasa hivi, basi akija, mfunge. We kaa kitako usage

hii ngano tu, asikutambue.” Sultani akakubali, akampa nguo zake, na farasi wake, yeye akavaa

gunia, akakaa kitako akisaga ngano.

Yule mwizi akachukua vile vitu akazunguka nyumba akajifanya kama anaenda kukaa upenuni, huyoo akaenda zake. Sultani akabaki akisaga ngano, akangoja hata asubuhi, asimwone mtu yeyote. Hata asubuhi kulipokucha, Mhindi mwenye nyumba akaja akamkaripia sana, maana hakumjua kuwa ndiye Sultani. Akamwambia, Ngano uliyosaga iko wapi? umekaa hapa usiku kucha bure? Akampiga kofi. Akataka kumuongeza la pili, Sultani akanena, “Wanijua mimi?” mhindi akasema, “Sikujui. Akanena, Mimi Sultani.”

Mhindi akamwambia, “Jinsi gani basi, Bwana, kunijia usiku na kutaka kazi kwangu?”

Sultani akanena, “Siye mimi niliyekuja kutaka kazi usiku.”

Sultani akamweleza mambo yote yaliyopita usiku, Mhindi akashangaa. Sultani akaenda nyumbani kwake, wala hakujua namna yakumpata mwizi huyu.

Lakini siku moja walikuwa wamelala wote wawili pangoni wakaja askari wakawakamata. Wakawapeleka kwa Sultani. Sultani akafurahi sana, akawaambia, “Ninyi mlidhani mtaweza kufanya kazi yenu ya kuiba siku zote bila kukamatwa? mlikosea sana.”

“Siku moja kila mwizi hukamatwa, naye hupata adhabu kali. Na ninyi, kwa sababu mu wezi wakubwa, mtapata adhabu kubwa, ndiyo kufa.

Basi akawaita askari wakawaua wale wezi pale pale mbele ya Sultani.

MTEGO WA PANYA HUINGIA WALIOKUWAMO NA WASIOKUWAMO

Palikuwa mtu na mkewe, Ndani ya nyumba yao walikuwamo panya wengi sana wakiharibu vitu, na kutoboa makanda ya

Mtama. Hata yule bwana wa nyumba akatafuta mtego akaenda ghalani akatega. Hatimye akapita panya akauona ale mtego akatambua kuwa mtego huu ametegewa yeye. Akapita jogoo panya akamwambia jogoo, “Wewe mwenzangu mkubwa kuliko, mimi hufanyi jamala ukaupiga teke huu mtego ufyatuke?”

Jogoo akamwambia, “Mtego huu umetegewa wewe, mimi haunihusu kitu.”

Panya akanena, “Kweli, lakini nauona umekaa vibaya wasije wakaingia waliomo na wasiokuwamo.”

Jogoo akanena, “Najuaaje?” akaenda zake.

Mara akapita mbuzi. Panya akamwambia mbuzi, “Bwana mdogo, hufanyi taratibu akaufyatua huu mtego na mimi nikapata riziki?”

Mbuzi akamwambia, “Mimi na mtego tu wapi? Mtego huu umetegewa wewe unayeharibu vitu vya watu, mimi chakula changu majani.”

Panya akanena, “Kweli huu ni mtego wa panya, lakini tena ni mtego wa kuingia waliomo na wasiokuwamo.”

Mbizi akanena, “Mimi sijui hayo, akaondoka akaenda zake.

Hatimaye akapita ng'ombe. Panya akamwambia, “Ee Bwana mkubwa, tafadhali ufyatue huu mtego, na mimi nikapata riziki, tena nauona umekaa vibaya, wasije wakaingia waliomo na wasiokuwamo.”

Ng'ombe akanena, “Hayo ni mambo yako wewe unayetoboa vya watu: mimi nakula majani, na mtama wapendapo kunipa. Sina haja kujishughalisha na mambo yasiyonihusu.” Akaondoka akaenda zake. Na panya naye akaenda zake. Akawahubiria wenziwe kuwa ghalani kuna mtego wa kuwanasa.

Mara akapita nyoka naye anawinda panya, akapita njia ya mtego akanaswa. Yule mwenye nyumba aliposikia ukifyatuka akachukua fimbo akaenda ghalani. Mkewe akamwambia, “Bwana, huchukui taa?”

Akanena, “Kuna kuua panya kukahitaji taa?” Alipoufikia mtego kwa ile fimbo yake yule nyoka akamwuma. Yule bwana akasema, “Ah kaniuma ati!” Mkewe akaleta taa kumulika akasema, “si panya, bwana, ni nyoka.”

Yule bwana akawa hoi, hoi tena maumivu yamemshika.

Huku na huku wakaitwa jamaa zake, wasidiriki kuja wote, akafa. Basi wakaja watu wachache usiku, ili kuwaliwaza wafiwa. Akachukuliwa jogoo akachinjwa kitoweo cha wale watu waliolala. Siku ya pili wakaja watu wengi kulala matangani. Akachukuliwa mbuzi akachinjwa kitoweo cha watu wa matangani. Hata siku ya kusoma hitma akachukuliwa ng'ombe akachinjwa, maneno ya panya yakatimia, ni mtego wa panya lakini wakaingia waliokuwamo na wasiokuwamo.

MGANGA NA MWANAFUNZI BUBU

Paliondokea mganga stadi mno wa ajabu. Ikawa katika nchi ile hakuwapo mganga kama yeye. Akafanya mali sana. Na watu kadha wa kadha wakataka wajifunze kazi yake, ila huyu mganga hakutaka mwanafunzi anayesema, ila bubu. Maana yake alijua awezi kueleza neno, na ufundi wake hautakwenda mbali, maana hakutaka ufundi wake uenee, wasije wakafaidika watu wengi kwa chumo. Watu walijaribu kumuomba awafundishe hata kwa mali hakutak. Akaondoka mwanamke mmoja aliyekuwa na mtoto wake mmoja tu. Akamwambia, “Mwanangu, wewe ni mwana yatima, baba yako amekufa, na mimi mwanamke siwezi kukufundisha kazi. Nataka usikilize shauri langu. Ipo kazi kwa yule mganga ukiipata utastarehe wewe na mimi. Lakini ina tofauti moja, hatakiwi mtoto ila bubu. Basi mwanangu nataka ujifanye bubu uende kwa fundi ukanyamaze kimya, ukastahimili yote atakayokutenda.”

Mtoto akakubali. Mama yake akamchukua akampeleka mpaka kwa mganga akamwambia, “Nimekuletea mwanafunzi.”

Akamuuliza, “Huyu mtoto ni bubu?”

Akanena, “Bubu tangu kuzaliwa.”

Akamwambia, “Unaona! Hivyo ndivyo nilivyotaka.”

Akampokea yule mtoto, mama yake akaenda zake. Yule mganga akamtwaa yule mtoto akamtandika vema kwa bakora, na mtoto kimya. Maana mganga alijua kuwa kama huyu mtoto ni mwongo, akipigwa atalia, “Mama wee! nakufa.”

Alipoona hakulia kwa bakora, akatafuta upupu akamtia. Na mtoto akalia kwa kutoa machozi tu, na kujikuna, lakini neno hakutoa. Mganga akaisha mizungu yote ya kutaka kumsemesha. Hakuweza. Hata mganga akayakini kuwa huyu kweli bubu. Akakaa naye.

Akamsabilia kazi zake zote. Kila anapomfanyizia mgonjwa dawa huyu mtoto sharti awepo. Akimtuma hutumika, akimwuliza neno hajibu ila kwa kichwa na mkono.

Wakakaa katika hali hii siku kadha wa kadha. Siku moja akaja mtu hawezi kichwa, kutaka kuaguliwa. Mganga akamtazama, akamwambia, Kichwa chako kimepungua, na ukizidi kukaa katika hali hii utafanya wazimu. Na mimi naweza kukufanyizia dawa lakini sharti nitoboe kichwa chako, nitazame yule mgonjwa akakubali. Mganga akatoboa kichwa, akatazama ndani akaona yuko funza mkubwa mweupe kati ya ubongo.

Akafahamu kuwa huyu ndiye anayeharibu ubongo wake, ikawa fundi kutafuta njia ya kumtoa yule funza. Akatufuta kulabu ili aingize katika ubongo ili akamkamate yule funza amtote. Yule mwanafunzi akatazama akaona ya kuwa Leo mganga anakosea. Ubongo utiwe kulabu mpaka ndani utaharibika. Lakini kusema hapati maana yeye bubu. Lakini tena akawaza kuwa mimi nikinyamaza hata huyu mtu atiwe kulabu atakufa, Basi akangoja hata mganga alipokuwa karibu kutia kulabu, Akasema, “Fundu unakosea! Huyu funza ukimto kwa namna hiyo, huo ubongo utazidi kuharibika. Twaa moto uweke karibu na kichwa huyo funza atoke mwenyewe kwa joto!”

Yule mganga alipomsikia mwanafunzi wake kusema, alishangaa, “Ah! Kumbe wewe unasema.” Akakasirika sana akataka kumfukuza kabisa. Lakini yule mwanafunzi akasema, “tafadhali ufikiri zaidi. Naliweza kukaa kimya kabisa na kukudanganya siku zote ili nipate faida kwa hila, lakini sikupenda mtu huyu afe, wala sikutaka wewe uadhibiwe kwa kosa lako. Kwa hiyo naliacha hila yangu nikasema.”

Mganga akasema, “kweli unayosema,” Akamsamehe.

Akazidi kumfundisha uganga wake. Wakawa rafiki tokea siku ile wakafanya kazi pamoja wakasaidiana.

KIBURI SI MAUNGWANA

Aliondokea fundi mhunzi nae akawa hodari sana kwa kazi ya uhunzi. Akapata mwanafunzi mmoja naye akaondoka kuwa hodari sana, hata wakamsifu sana huyu mwanafunzi kuliko fundi wake

Hata yule mwanafunzi akafanya kichwa kikubwa akafanya kiwanda chake, na fundi wake asimjue, ila hupata siku kwa nadra kwenda kumtazama fundi wake napo kwa vishindo na makeke. Hata siku moja alipokwenda mtazama fundi wake, akamkuta kazini anafua. Akamwamkia fundi wake

kwa hivyo tu, maana sasa anajiona bora yeye. Fundi wake akamwitikia akamwambia, “Je, baba umekuja kututazama.” Akamwambia, “Naam.” Hata alipokwisha pumzika, fundi akamwambia mwanafunzi wake, “Baba, njoo mara moja utusaidie kufukuta.”

Mwanafunzi akashika mifuo kwa ghasia tupu, akafukuta. Na katika kufukuta akailiza ile mifuo kwa mlio huu:

Hapana jingine, fundi.

Hapana jingine, fundi.

Fundi akaona mwanafunzi wake ametakabari sasa, anathubutu kuja mbele yake, na kunena hakuna fundi mwingine. Akaona mwanafunzi wake anakuja kwa meno ya juu. Hatimaye yule fundi akamwambia mwanafunzi wake, “Sasa njoo wewe unipokee, shika nyundo utengeneze hili fuawe.” Basi yule mwanafunzi akatwaa nyundo, akashika kufua lile fuawe. Fundi akashika mifuo. Akafukuta kwa taratibu. Naye akailiza mifuo yake hivi:

Jingi liko wee, fundi.

Jingi liko wee, fundi.

Maana yake usiseme hapana fundi jingine, liko fundi jingine.

Wakafanya kazi yao wakaisha. Yule mwanafunzi akaenda zake. Sifa zake yule mwanafunzi zikawa zinavuma kama ngoma, hata zikafika kwa Sultani. Sultani akamwita akamwambia, “Nasikia wewe fundi mkubwa wala hapana kazi inayokushinda katika uhunzi.”

Akamwambia, “Naam.”

Basi Sultani akamwambia, “Nataka unifulie mtu, umtie na roho Yake, na kama huwezi si fundi kitu, nitakuua.”

Yule fundi akashughulika, akili zikamduru. ikatazamwa katika ramli, ikaonekana ya kuwa ametendewa na fundi wake. Yule mwanafunzi akaondoka akaenda kwa fundi wake, akamuangukia. Fundi wake akampokea. Akamweleza ile habari iliyompata. Fundi akamfundisha maarifa mwanafunzi wake. Akamwambia, “Nenda kwa Sultani ukamwambie kazi yake uliyonituma, Maulana, nimesikia, nimeimekubali, lakini nimetindikia kitu kimoja. Haiwi ila unipatie makaa ya mgomba.

Sultani akaagiza watu wakusanye migomba wakaichoma moto wasipate makaa. Sultani akashindwa. Yule fundi akapona asiuawe.

Kisha fundi akamwambia mwanafunzi wake, “Je baba fundi jingine lipo halipo?”

Akanena, “Lipo. Akakaa kwa heshima na adabu.”

KISA CHA MASKINI AU HADHI BORA KULIKO MALI

Palikuwa na mtu mmoja maskini hohehahe, hana mbele wala nyuma siku moja ikamjia fikira akanena, “Nitakwenda kwa Sultani nitake kazi.”

Akaondoka

akaenda kwa Sultani. Akamkuta Sultani amebarizi yeye na mawaziri wake. Akamwamkia, “Subalheri maulana.”

Sultani, akaitikia, “marahaba.”

Yule maskini akanena, “Mtumwa wako ataka kuonana nawe

kwa faragha, maulana.”

Sultani akakubali akaenda faragani.

Maskini akanena, “Seyidina nimekuja kwako kuja kutaka kazi. Na mimi kazi yangu haina mshahara wala chakula, wala nguo, nataka neno moja kwako Seyidina.”

Sultani akanena, “kama lipi?” Akanena, “wakati unapobarizi pamoja na mawaziri wako, nataka ufanye kawaida ya kuniita Mbele yao ukininong’oneza-nong’oneza.” Sultani akanena, “Nikuambiaje?”

Maskini akanena, “Upendavyo wewe, Maulana, hata kama utanitukana, utaniita mjinga, baradhuli, kelb, yatosha. Ila napenda watu waliopo wasisikie ila mimi mwenyewe.”

Sultani akanena, “Vema.”

Hata siku ya pili, yule maskini akaja, na baraza imejaa watu. Sultani alipomwona akamwita, “Hamadi!”

Akaitika, “Lebeka Hababi.” Akaenda akamnong'oneza, asimwambie neno ila maneno kama yale, mjinga, baradhuli, kelb, kalil il adab. Na yule maskini, kazi yake ni kuitikia tu, “Naam, Ee Wallah, Inshallah, Bwana.” Kisha hutoka huenda zake.

Waziri mkubwa yakamuudhi mambo yale. Akaona ya kuwa huyu Hamadi sasa ana hadhi kwa Seyid kuliko sisi wote. Hata siku moja yule maskini akaitwa nyumbani kwa Waziri, akamfanyia chakula, akamkaribisha vizuri. Kisha akamuuliza, “Hivi Hamadi kila siku ukija barazani Seyid hukuita akakunong'oneza, anakuambia nini?”

Yule maskini akanena, “Sultani huniuliza mambo mengi juu yenu ninyi mawaziri, na mashehe. Kama siku lile ya awali, aliniuliza habari zako wewe, yaani ataka kukutoa kazini. Lakini mimi nikamwambia, Maulana, huyu waziri mtu mwema sana, akitoka huyu hupati mwingine kama huyu.”

Waziri akanena, Ndivyo.

Shika papo. Akatwaa fedha nyingi, na zawadi nyingine akampa, akaenda zake. Hata siku ya pill akaitwa na Shehe mmoja, naye akamuuliza maneno kama yale, na maskini akajibu kama yale na kuzidi. Naye akatwaa mali akampa. Ikawa watu wakubwa wa baraza wote wakamwita na kumhoji kama yale na yeye kila mtu akamsifia kwa yake. Na wote wakampa mali.

Hata siku moja Sultani alikuwa amekasirika kidogo, na kwa bahati alisahau kutumia sauti ndogo aliposema naye akamwambia kwa wazi, “Mjinga, baradhuli, keib, kalil il adab!” Watu wote waliokuwako wakasikia wakafikiri Sultani amemkasirikia, tena amechukizwa naye. Basi wote wakamdharau wakamfukuza.

HADITHIYA BIBI MNG'INDO

Walikuwapo wazee wawili wa King'indo wakazaa mtoto wao mmoja mwanamke, akawa mzuri sana. Baba mtu akafa, akabaki mama mtu na binti yake. Habari ya yule mtoto ikaenea katika mji kuwa mtaa fulani kuna mtoto mwanamke mzuri. Ikawa watu wengi kutaka kwenda kuposa.

Yule mama mtu kamweleza mwanawe ya kuwa asimkubali mtu mpaka atakayemwambia yeye mwenyewe. Mama hakutaka mume wa kumfaa mwanawe tu, alitaka mume wa kumfaa na yeye, maana sasa yeye mzee, hali yake fupi

Akatoka kijana wa kwanza kwenda posa, pamoja na kikundi cha wenzake mpaka mlangoni kwa Bibi Mng'indo, wakamkuta Binti Mng'indo. Mwenyewe Bibi Mng'indo yuko kondeni analima. Naye kamwagizia mwanawe akija mgeni aje kumwita.

Basi walipokuja wale wageni Binti Mng'indo akawakaribisha vlzuri, akawaambia,

Ningojeni niende nikamwite bibi mkubwa wangu. Akaondoka yule mtoto kwenda kumwita mama yake. Akawambia mama, Nyumbani kuna wageni, vijana wanaume.

Bibi Mng'indo akatambua kuwa wamekuja posa. Akamwambia mwanawe Tangulia. Bibi Mng'indo akatwaa matambara akajifunga mguuni, akajifanya ana kidonda kikubwa, na wakati wa kwenda akawa anakwenda pecha. Alipofika karibu na nyumba yake akaanza kulia na kuugua, na kuanguka chini Na kila akianguka, huimba;

Pindingu chali Nikalole wageni Wa mwanangu kukaya.

Maana yake, Naanguka chali. Nakwenda tazama wageni wa mwanangu mjini au nyumbani. Basi yule kijana aliyekuwa posa pamoja na wenzake walipomwona huyu mama anakwenda pecha, anapita akianguka, na

kuimba, wakaangua vicheko wakacheke, wakasema, “Mtazameni mama ya King'indo anavyokwenda.”

Ikawa kumcheke mpaka yule mama alipoingia ndani.

Halafu akajikakamua akakaa mlangoni, akawauliza habari wageni. Wakasema haja yao. Akakataa akasema, “La, binti yangu hatakufaa bwana. Huyu maskini, samli ataiweza wapi,” wakarudi.

Mara ya pili akaenda mtoto wa Sultani na wenzake kumposa Binti Mng'indo. Walipofika hawakumkuta Bibi mkubwa, walimkuta Bibi mdogo tu. Naye kama desturi yake akawakaribisha. Kisha akaenda kumwita Bibi mkubwa wake kondeni. Yule Bibi mkubwa wakati wa kuja hali yake ile ile na wimbo wake

ule ule :-

Pindingu chali Nikalole wageni Wa mwanangu kukaya.

Alipofika karibu ya nyumba mtoto wa Sultani hakuweza kujizuia, akacheke sana, akasema, “Mwajua mzee huyu, ana mambo? Vile ndiyo nini?

Basi Wote wenye vidonda huanguka vile?”

Wote wakacheke mpaka alipoingia ndani. Kisha akawauliza haja yao. Mtoto wa Sultani akasema, Mimi nimekuja posa binti yako. Bibi Mng'indo akasema, “La, hatakufaa bwana, huyu amezoea Ugali

kwa panya, nyama ataiweza wapi?” Mtoto wa Sultani akaenda zake. Ikawa watu wote waliokuja namna yao hii. Naye akawakataa wote. Hata siku moja akaja mtoto

wa Waziri pamoja na vijana wenziwe. Yule mtoto akawakaribisha, kisha akaenda kumwita mama yake. Na Bibi Mng'indo naye namna yake ya kuja ikawa ile ile. Akapita akianguka, na kwenda pecha, na kuimba. Alipofika karibu ya nyumba akaanguka makusudi kama ilivyo desturi yake.

Mara yule mtoto wa waziri akaruka, akamwinua, akamwuliza. “Una nini Bibi mkubwa? Pole, Mama!” Na wenzake waliotaka kucheka akawakataza.

Akanena, “Mna haja gani kumcheka huyu kizee.” Akamwokota akampangusa-pangusa udongo.

Kisha akaingia ndani. Halafu akawauliza haja yao. Mtoto wa Waziri akasema, “Nimekuja posa Binti Mng'indo.”

Yule kizee akanena, “Hii ndiyo namna ya kijana nimtakaye. Amenionea huruma leo hajakuoa, akikuambia atakuoa atakutazama, wewe macho mawili, na mimi kadhalika atanitazama vema.”

Basi huyu akapata ruhusa kumposa Binti Mng'indo,

Akamposa. Yule mama asifanye kisirani akampa mtoto wake amwoe, akanena, “nakupa mwanangu, maana nimekuona kuwa moyo wako thabiti, utaweza kukaa vema na mwanangu na kunitunza mimi mkweo.”

KWA NINI WATU WEUPE HUITWA WAZUNGU?

Zamani wazungu walipoanza kuingia katika nchi ya afrika watu wengi hawakuwapenda.

Basi ikawa mji wanaokaa wazungu watu huhama kutafuta mahali pasipo wazungu. Alikuwako mzee mmoja hapa Unguja alipoona bendera za Wazungu zinazidi, akaazimu kuondoka kwenda bara. Akaenda hata akafika mji mmoja mahali pazuri akataka kufanya maskani.

Hata jioni akasikia kengele akauliza, “Nini hicho?”

Akaambiwa, “Nyumbani kwa Mzungu huko, pana Mzungu mwalimu anasomesha watu.”

Akanena, “Haya ndiyo niliyoyakataa tangu kwetu.”

Akapumzika siku kidogo, akaondoka akaenda mbele. Akafika mji mmoja, akakaribishwa akakaa. Akauliza habari za Wazungu, akaambiwa, “La, hapa hawapo, akafurahi sana.

Akafanya maskani, akaanza kufanyiza biashara kidogo, akaanza kustawi. Hata baada ya miezi sita, siku moja wamekaa kitako wakasikia mganda unapigwa. Watu wakasema, “msafara huo!” Punde si punde wakaona msafara unaingia, wakaauliza, “msafara wa nani?”

Wakaambiwa, “wa Mzungu, mwenyewe yuko nyuma anakuja.”

Mzungu alipofika, akamwita jumbe wa mji akamwambia, “Nimetumwa na serikali yangu kuja kutia bendera hapa, maana hii nchi yake!” Yule mgeni akafahamu kuwa ndio mwanzo wa kuja kukaa pale. Akaondoka akaenda zake mpaka Nyasa.

Alipofika huko akakuta Wazungu wa Serikali, wa biashara, walimu, wawindaji wamekuwako tangu zamani. Akaona udhia mkubwa, kusimweke. Akaifanya safari akarudi Unguja. Aliporudi akawaeleza watu kisa chake.

Lakini akanena, “Mimi sijashindwa maana Afrika kubwa. Sasa nitafanya safari nitakwenda ndani huko mpaka Uganda nikae.”

Wenzake wakamwambia, “Baba, Uganda kuna Wazungu kuliko huku kwetu.”

Yule mzee akasema, “kweli sasa najua hawa sio Wazungu lakini Wazungukeni, hii Wazungu ni mkato wake tu, wamekwisha tuzunguka.”

KISA CHA ALI NA WATOTO WA NDUGUYE

Zamani moja palikuwa na ndugu wawili, mmoja jina lake Lus, wa pili jina lake Kedhab. Baba yao akafa, watoto wakabaki na mama yao. Hawa watoto walirithi mali nyingi sana kwa baba yao lakini wakaiharibu yote, wakabakiwa na kitu kidogo. Kedhab akamwambia nduguye Twende tukamuulize mama yetu atuambie kazi ya baba yetu. Wakaenda wakamwuliza mama yao, mama yao akawaambia ya kuwa, “Kazi ya baba yenu ilikuwa ni kufua majembe.”

Wakaenda wakajifunza kazi hiyo lakini hawakuijua, wakaharibu vyuma vya watu tu, wakafukuzwa. Basi ikawa kila kazi waliyopelekwa wakashindwa. Hata walipoona pesa zao zinakwisha, wakaenda kwa mama yao wakamwambia, “Mama afadhali tukuuze tupate pesa.”

Mama yao akakubali wakaenda kumuuzwa kwa Sultani, wakapata mifuko miwili ya fedha, wakatumia. Yule mdogo akamwambia mwenziwe, “Twende kwa mama yetu tena tukamuulize kazi ya baba, naye lazima atuambie, akituficha tumuue.”

Wakaenda hata shamba alikokuwa anafanya kazi. Wakaomba ruhusa kwa nokoa ili waseme naye. Nokoa akawaambia, “Mama yenu sasakazi kwa ana kazi, ngojeni amalize kazi kwanza.”

Yule mkubwa akasema, “Mimi nitakwenda kumshikia kazi yake huyu mwenzangu akaseme naye.”

Nokoa akakubali. Yule mtoto akaomba dua, mara wakaja watu wengi wakapokea ile kazi yake. Wakalima ngwe yote na zaidi.

Nokoa alipoona vile akakimbia akaenda akampasha Sultani habari. Sultani aliposikia akawaacha wamchukue mama yao, akawaongeza na fedha. Walipofika nyumbani mama yao akawaambia, “Kazi ya baba yenu ilikuwa wizi.”

Basi wale watoto wakanena, “tumesikia.” “Wakafanya shauri wakanena, “twende tukaanze kuiba kwa baba mdogo.” Maana na baba yao mdogo kazi yake ni hii hii.

Yule baba yao mdogo alipowaona hawa watoto wanakuja kafahamu mambo yao, maana ajua kuwa mwana wa nyoka ni nyoka. Akamwambia mkewe, “Huyo kondoo mfiche mbali, maana wale watoto watamwiba.” Mkewe akaenda akamficha katika chumba cha kuni. Usiku wale watoto wakaamka. Kedhab akaondoka akapapasa huko na huko hakuona kitu. Akaenda hata chumba cha baba yake mdogo, akafanya taratibu akafungua mlango. Akajigeuza sauti, akaiga sauti ya baba yake mdogo akasema, “Bibi, yule kondoo umemficha wapi?”

Mama yake mdogo akamwambia, “Kondoo nimemficha katika chumba cha kuni.”

Kedhab akaenda chumba cha kuni akamchukua, akamwamsha nduguye wakaenda zao.

Walipokuwa wakienda zao hawakuenda wote pamoja.

Ilikuwa yule anayechukua kondoo hupita mwituni, na asiye kitu hupita njiani. Ikawa wanakwenda huku wanapokezana mara huyu mwituni huyu njiani. Asubuhi yule Ali(baba yao mdogo) akamwuliza mkewe, “yule kondoo umemficha wapi?” Mkewe akamwambia, “nimekuambia tangu usiku kama nimemficha chumba cha kuni.” Wakaenda kutazama wakaona kondoo hayupo.

Ali akatambua kuwa wale watoto ndio waliokwiba kondoo. Akawafuata kungali giza giza bado. Akawakuta njiani katika kazi yao ile ile ya kupokezana, mara Kedhab njiani, mara Kedhab mwituni, Lus njiani.

Yule babayao naye fundi wa wizi. Basi akajificha mahali mwituni. Alipotokea mwenye kondoo akampokea, naye akadhani mi mwenziwe, akamwachia. Ali akachukua kondoo akaenda zake Hata wale watoto walipokutana wakaulizana, “Kondoo anaye nani?” Wakatambua kuwa baba yao mdogo ndiye aliyemchukua kondoo mara Kedhab akarudi mbio

kwenda nyumbani kwa Ali, akatangulia yeye kufika kabla Ali hajafika. Akabadili nguo, akavaa kanga akakaa mlangoni.

Alipokuja baba yake akampokea kondoo, akamfunga. Akaenda akamwambia aende akaoge. Naye akamdhani ni mkewe, akaenda kuoga. Huku nyuma Kedhab akamfungua kondoo akaenda zake. Alipomfikia nduguye wakamchinja yule kondoo, wakachukua nyama. Baba yao alipokuja kuwatazama, wakamfanyizia chakula, kitoweo chake ile nyama ya kondoo.

Yule mzee Ali alipoona mambo yale akaenda akamwambia Sultani. “Bwana mjini mna wezi humu, yafaa uagize mabedui waje wawakamate.”

Sultani akaagiza mabedui wakaja.

Nao chakuia chao wakataka mbuzi na asali. Akatumwa Ali kwenda kutafuta asali na mbuzi. Marejeo ya Ali wale watoto wakajificha njiani. Kedhab akakaa njiani akajifanya maskini kipofu.

Alipotokea Ali, Kedhab akaanza, “Ya Allah maskini!”

Ali akamwambia, “shika kamba ya mbuzi twende zetu mjini.” Wakaenda zao, Ali mbele, maskini nyuma. Kila wakati Ali humuuliza Kedhab, “Mbuzi unaye?”

Naye hunena, “Ninaye.”

Hata walipofika pale alipojificha Lus, akatoka akakata ile kamba, ya mbuzi, akamchukua mbuzi akaenda zake. Ali akamwuliza maskini, “Mbuzi unaye?”

Akasema, “sijui, naona kamba imelegea.”

Ali alipotazama akaona mbuzi hayupo. Akamwambia, “Kaa hapa. Mimi nakwenda kufuatia mbuzi.” Yule maskini akaachiwa kitungi cha asali. Na alipoona kuwa Ali amerudi nyuma, akakimbia na kile kitungi hata kwa nduguye.

Na Ali kule alikokwenda hakumpata mbuzi, akarudi kwenye asali, asiikute asali wala maskini. Akaenda kwa Sultani Akamwambia, “Wezi wamenishinda wameninyang’anya mbuzi na asali pia.”

Sultani akasema, Mimi ninayo asali. Wakaitwa mabedui wakapewa ile asali, wakaenda zao mahali mahali pasipo watu, maana wakila hula uchi nguo huvua. Basi na wao wakaziacha nguo zao pamoja na mlinzi mmoja. Kedhab akaja akamuuliza yule mlinzi, “Wenzangu wako wapi?”

Akamwambia, “Wako kule, wanakula chakula.” Akamwambia, “na kitu cha kutowelea?”

Akanena, “Hawana.”

Basi akatoa reale ya Sham moja akamwambia yule mlinzi wa nguo, akamwambia, “Nenda kanunue mofa kwa pesa moja.” Yule mlinzi wa nguo akamwona mjinga huyu, akaenda upesi kununua ili amuibie ile reale. Huku nyuma Kedhab kachukua nguo zote za mabedui akaenda zake.

Yule mlinzi aliporudi akakuta nguo hazipo, na yule mtu naye hayupo. Akaenda kuwaambia wenye nguo mambo yaliyompata. Nao wakaenda kumwambia Sultani ya kama wezi hawa wanatushinda. Sultani akapiga mbiu kuwa, baada ya saa nne za usiku hapana ruhusa kutembea. Kisha akaweka askari sita wa zamu. Kedhab akaenda akafanya mikate miwili, mmoja akautia kila namna ya kileo, mmoja akautia manukato tu. Usiku akatoka askari wakamkamata.

Akasema, “Msinipeleke gerezani, nipelekeni kwetu kwanza nikale chakula, halafu mnipeleke gerezani.” Wale askari wakakubali.

Wakampeleka kwake kula chakula. Walipofika nyumbani akatwaa ule mkate wenye vileo akawapa askari. Akawaambia, “karibuni,” na yeye akala ule mwingine. Wale askari wakalewa

Kedhab akawanyang'anya bunduki zao na nguo akaenda zake. Asubuhi walipoamka wakajiona hawana nguo wala

silaha. Sultani alipopata habari akatoa askari wengine washike zamu, mambo yakawa yale yale.

Hata Sultani ikampasa kushika zamu mwenyewe. Usiku akaja kedhab. Akamhadaa Sultani hata akamfunga pingu, kisha akampiga sana akamtia gerezani. Asubuhi waziri akaenda kutazama gerezani akamuona Sultani amefungwa, tena amepigwa. Sultani akamweleza habari yote. Kisha Sultani akapiga mbiu, akasema mwizi huyu anayekwiba mjini akipatikana nitampa binti yangu amwoe.

Kila mtu akajitapa kuwa mwizi ni yeye. Kedhab akanena, maneno tu hayafai Sultani aandike kwa hati ya mkono wake kama kweli atamwoza binti yake.

Sultani akakubali, akaandika.

Kedhab akaenda kuleta nguo za mabedui, na nguo za askari Tena akasema, “Mimi ndiye niliyekufunga pingu na kukutia gerezani.”

Sultani akanena, “Kweli, lakini kabla sijakupa binti yangu nataka uniambie. Je, unaweza kuiba kitu chochote?”

Yule mwiziakajivuna, akasema, “Ndiyo Bwana.”

Sultani akasema, “Nitakuambia kitu kimoja ambacho nataka ukiibe. Kama ukikiiba, nitakupa binti yangu na nusu ya ufalme wangu lakini kama usipoweza nitakuua.”

Akasema, “Vema, nimekubali.” Sultani akamwambia, “Nataka uibe ukaidi wa mke wangu. Ukauchukulie mbali, maana napenda asiwe mkaidi.”

Kedhab akasema, “Ah! siwezi bwana, umenishinda. Basi akafa.”

KISA CHA SUNGURA NA CHECHE

Aliondoka cheche akamwambia Sungura, “Yahe! Mimi ni mmojawapo sina mke,

na wewe mwenzangu nakuona hali kadhalika. Basi si afadhali tukakae pamoja mimi nawe tutakakachopata tule, tukikosa tumshukuru Mungu!”

Sungura akasema, “hayo ndiyo maneno.” Wakakaa mahali pamoja kazi yao ilikuwa kutega ndege, wakipata wakila, hata siku moja walikwenda tembea mahali wakakuta mayai ya kanga. sungura akasema, “Na tumtege huyu kanga.”

Kicheche akasema, “Vema.”

Sungura akaenda akafanya mtego, akatega. Akaja kanga akanaswa, wakamchukua nyumbani. Sungura akamwambia cheche,

“Somo! Huyu kanga mchome, na mayai pia, mimi nimechoka kidogo nataka kusinzia.”

Cheche akasema, “Vema.” Akachoma. Hata kanga alipokwisha iva, cheche akapigwa na ile harufu nzuri ya kanga asiweze kustahimili kungoja Sungura, akamla kanga na mayai pia. Kisha akatwaa ganda moja la yai akalitengeneza akalificha mahali. Akatwaa manyoya akayatia motoni na yeye akajifanya kalala. Yale manyoya yalipoanza kunuka Sungura akazindukana, akamwuliza kicheche, “Kanga yuko wapi somo?”

Cheche akasema, “Nalimwacha papa hapa motoni, mimi nalishikwa na usingizi kidogo, hakosi kaungua.”

Sungura akasema, “Vema. Fumbo mfumbe mjinga, mwerevu hung'amua.”

Sungura amekwisha fahamu kama rafiki yake kamtafuna yule kanga, moto kafanya kisingizio. Sungura akasema, twende tukatafute chakula kingine, wakaenda. Kila mtu akaingilia upande wake. Wakapata

walivyopata. Cheche akashiba sana akalala. Akaja Sungura akamkuta cheche kalala.

Akatwaa majani ya mgomba, akamnyemelea kwa taratibu, akamfunika yale majani ya mgomba, akamfunga vema. Kisha akatwaa ufito akampiga sana. Cheche akalalamika sana. Sungura akakimbla. Cheche akalia akanyamaza. Mara mzee Sungura atokea akamsukuma cheche kwa miguu, akasema. “Kitu gani hiki?”

Cheche akamwambia, “Ni mimi rafiki yako.”

” Una nini?”

Cheche akasema, “Kaja mtu hapa kanifunga, tena kanipiga sana kisha akaenda zake.”

Sungura akasikitika sana. Akasema, “Unamjua mtu huyotumpige?”

Cheche akasemaa, “Simjui.”

Wakakaa kitako. Hata siku moja kikawako sherehe hapo mtaani. Cheche akamwambia Sungura, “Twende tukacheze ngoma leo.”

Sungura akasema, “Vema, lakini nataka nifike kwetu kwanza nikatazame jamaa, kisha nitakuja.”

Cheche akakoga, akavaa nguo zake nzuri. Akatwaa unyoya wa kanga na gamba la yai akachomeka kichwani akaenda kucheza ngoma. Hata alasiri akatokea sungura, akamwona rafiki yake uwanjani anawaka kwa unyoya na yai la kanga. Mara Cheche alipomwona Sungura akaenda akashika zumari akapiga:

Kanga pia!

Singizia moto!

Ti! Ti! Ti!

Maana yake, kanga nimemla wote nikasingizia moto. Sungura aliposikia,
akaamka akashika ngoma kubwa akapiga

Nikalimkamata, Nikalifungafunga, Kwa majani ya mgomba.

Nikalipiga

pu! pu! pu!

Cheche hakujua kwanza ni nani, aliposikia ngoma akahamaki akashika
fimbo wakapigana. Hata mwisho wakaamuliwa. Na urafiki wao ukavunjika

WAJINGA NDIO WALIWAO

Paliondokea mtu katika Kisiwa cha Unguja, enzi ya Seyid

Majid Said, naye akikaa mjini. Na mtu huyo alikuwa hana kazi maalum, yake ililikuwa kuwafuata Waarabu wakubwawakubwa

na kupata manufaa yake kwao. Na kazi za zamani hizo ilikuwa watu kufunga bidhaa na kwenda bara kufanya biashara, au kulima vyakula na kuuza.

Na yeye alikuwa mtu mmoja asiyetaka kazi ya namna hii.

Hata hatimaye akaonelea mji hauemweki. Akatafuta kanzu yake njema akavaa, na kilemba chake cheupe, na msahafu wake kwapani, akashika njia kwenda pande za mashambani kutarazaki. Na kazi aliyochagua ni kazi ya ualimu kusalisha watu.

Lakini yeye mwenyewe hajui kusoma hata herufi moja. Alichagua kwenda shamba kwa wahadimu, huko ndiko walikokuwa wajinga wasiojua kusoma, na hata dini ya kislamu ilikuwa haijaingia kwao bado. Basi mwalimu akawasili Unguja Ukuu. Wahadimu walipomwona mgeni wakamkaribisha sana.

Hata waliposikia kuwa yeye ni mwalimu wakazidi kumkaribisha na kumheshimu. Na yeye mwenyewe ikawa mchana kutwa kufunua msahafu, na kutazama tu, watu wakadhani anasoma, Akapewa nyumba bure na chakula kwao. Hatimaye akawaambia, “jengeni msikiti nikusalisheni.”

Wahadimu wakajenga msikiti.

Hata wakati wa kusali ulipojiri mwadhini hapana, maana wale wenyeji hawajui. Basi ikawa kazi ya mwenyewe Mwalimu kuadhini. Lakini naye ni vile vile hajui kitu. Akasimama akaadhini hivi :-

“Allah akbar! Allah akbar! Wajinga ndio waliwao, Wajinga ndio waliwao. Allah akbar. Watu wakajaa msikitini.

Huyu mwalimu kama nilivyosema hajui kusoma, si kukuambia kusalisha! Lakini watu wamekwisha kuwamo msikitini, ikawa hana hila ila kusalisha. Akaenda panapo kibla, akasalisha hivi:

“m, m, m, m, Wajinga ndio waliwao, Amin.”

Ikawa kila akisema, “M, m, m, m, wajinga ndiyo waliwao, wajinga ndiyo waliwao.”

Wahadimu huitikia, “amin.”

Kila akiinama na kuinuka maneno ni hayo hayo. Na Wahadimu wakidhani asema Kiarabu, wakawa wamekazana tu, “Amini!”

Zilipokwisha sala wakatoka nje. Wahadimu wakamsifu mwalimu wao jinsi anavyosalisha vizuri. Ikawa hivi hali ya mambo kwa siku nyingi kupita. Wakamfanyia. mshahara mwema

Siku moja akatoka Mwalimu wa kweli mjini anayejua kusoma na kusalisha ili kwenda kutembea shamba. Akafika Unguja Ukuu. Akapata habari kama mjini pana Mwalimu mmoja arifu sana, ndiye anayesalisha msikitini. Na huyu mwalimu mgeni asiende kumtazama, akangoja mpaka wakati wa sala. Wakati wa sala ulipojiri akamsikia mwadhini anaadhini. Lakini maneno yake yakamshtusha sana.

“Allah akbar! Allah akbar! Wajinga ndio waliwao, Wajinga ndio waliwao. Allah akbar!”

Yule mgeni asiseme neno, akaenda msikitini, akakuta watu wamejaa. Na mbele yao panapo kibla yuko mtu anayemjua tangu mjini, naye anamjua hajui kitu. Basi akamsogelea kule kule mbele ili amsikilize vema. Na mwalimu alipomuona huyu mgeni akashtuka sana maana naye amjua tangu mjini.

Akawaza kuwa leo uongo wangu utabainika. Lakini mara akili ikamjia.akageuza namna ya kusalisha, akasalisha hivi :-

“M, m, m,m, mwalimu usinibaini, nikipata sita, tatu zangu, tatu zako wajinga ndio waliwao Amin!”

Na maneno haya walisikiana wao wawili tu, maana walikaa karibu karibu. Akashika kusalisha kwa maneno yale yale.

“M, m,m, m, Mwalimu usinibaini,Wajinga ndio waliwao, nikipata nane, nne zangu, na nne zako, Amin.”

Akasalisha hivi mpaka mwisho, wakatoka. Walipotoka nje wale walimu wakaamkiana Kwa vicheko sana.

Watu walipowaona wanacheka, walidhani wanacheka yao ya huku nje, maana wanajuana. Kumbe wanacheka yale yale ya msikitini: “Mwalimu usinibaini, wajinga ndio waliwao, nikipata nane, nne zangu, nne zako. Wakakaa katika hali hii wakiwala mpaka walipochoka, wakaja zao mjini na wingi wa mapesa.

MBWA NA PAKA

Hapo kale maarifa ya kufuata vitu na kunusa yalikuwa ya paka. Mbwa akaona haya ni maarifa makubwa ya kufuata vitu na kunusa, na kujua njia kwa harufu.

Basi mbwa akatolea akaenda kwa paka akamwambia, “nifundishe na mimi kazi hii ya kunusa harufu, maana naona ni njia njema ya kupata chakula.”

Paka akamwambia, “vema.”

Mbwa akakaa kwa paka, na paka akamfundisha kazi aliyotaka kama desturi. Mbwa alipoona siku nyingi zimepita, naye kazi anajua, akaomba ruhusa kwa fundi wake paka kwenda zake. Akanena, “siku zimekuwa nyingi na mimi nataka nikatafute riziki.”

Paka akamwambia, “bado hujajua yote, subiri kidogo.”

Mbwa akanena, “la, sharti niende zangu.”

Paka akanena, “vema, nitakupa ruhusa, lakini si leo. Njoo kesho.”

Asubuhi paka akamwambia mkewe, “akija mwanafunzi wangu mbwa kuniulizia mwambie bwana hayupo, kaenda huko.”

Mbawa akaja, akauliza, “bwana yuko wapi?”

Mke wa paka akanena, “amekwenda huko.” Naye aliagiza hivi kusudi apime akili zake, na kadiri alivyojua.

Mbwa akauliza tena, “wapi?”

Akajibiwa, “hukoo!”

Basi mbwa akaanza kunusa harufu ya paka na kutafuta alimopita.

Akaipata harufu yake akaifuata. Na paka kajificha kipande makusudi. Mbwa akaifuata harufu tu kwa saa nyingi. Hata akafika mahali alipo paka. Kumbé paka alipofika mahali pale alifanya kuruka toka jiwe hili hata jiwe jingine. Kisha akaingia pangoni akatokea upande wa pili. Alipotokea upande wa pili akarukia juu ya mbuyu, akapanda juu. Mbwa akafuata harufu hata mle alimorukia, akaingia pangoni naye akatokea upande wa pili wa pango. Lakini alipofika pale aliporukia juu ya mbuyu akili za mbwa zikaisha. Akabaki ananusa chini, Akazunguka huko na huko asimwone paka.

Paka yuko juu anamwona. Hata paka akaanza kupiga kelele, “Na huu! Na huu!” Maana yake, Umefanya haraka kutaka kwenda zako, na wewe ulidhani unajua mizungu yote, na huu je? Ndiyo maana hata sasa mbwa hodari wa kufuata harufu ya chini kwa chini, lakini kitu kikipanda mti huwa basi, hawezi kukifuata. Ndiyo maana mbwa hawezi kupanda mti.

NJIA YA KUVUKIA MWENYE DENI

Palikuwa na mtu mmoja mkopi sana, akakopa mali kadha wa kadha za watu mbalimbali. Ikawa kila aliyemkopesha fedha fedha yake, naye hana cha kuwalipa. Hata mwisho wale wenye mali wakachoka, wakapatana wote wamshtaki.

Akatokea mmoja katika wale wanaotaka kumshtaki akamwambia, “Mimi nitakufundisha njia ya kuvukia katika madeni yako lakini kwa sharti moja.”

Akamwambia, “Sharti gani?” Akanena, “Ukivuka katika mashtaka haya kwa akili nitakayokufundisha tafuta pesa unilipe mimi tu.”

Mkopi akanena, “nimekubali.” Akamwambia, “Ukienda kunako hukumu ukiulizwa neno jibu, Ng'o!”

Yule mtu akakubali.

Wakamshitaki, akaitwa katika hukumu. Wale watu wanaomuwia wakaleta mashtaka yao, wakasema, “huyu tunamuwia naye hataki kutulipa.”

Kadhi akamuuliza, “Je, hawa wanakuwia kweli?”

akanena, “ng'o!”

“Umekopa fedha kwa hawa? Akanena, “ng'o.”

“Utalipa fedha hii?”

Akanena, “ng'o.”

Kadhi akakasirika sana, akasema, “Jinsi gani ninyi mkaniletea mtu mwenye wazimu. Ana Wazimu dhahiri huyu. Haya tokenii, hana hata deni kitu huyu. Amekopaje naye ana wazimu,”

Akawafukuza katika hukumu. Hukumu ilipokwisha yule aliyemfundisha njia hii ya kuvukia, akamwambia, “Unaona, akili yangu imekufaa, sasa nipe haki yangu.”

Akamwambia, “Ng'o!” Akamwambia, “Umenigeukia hata mimi?”

Akamjibu, “Ng'o!”

Akavuka, hakumlipa mtu.

KAMA PUNDA

Alikuwako mtu mmoja aliyekuwa kipofu tokea kuzaliwa kwake. Siku moja ikapita hekaya, macho yake yakafumbuliwa hivi tu kwa ghafula. Na mbele yake kulikuwa na punda amesimama. Akamuona huyu punda asione kitu zaidi. Mara macho yake yakafumbwa tena. Basi ikawa ulimwengu wake wote punda!

Ikawa akikaa mahali akaja mtu “akisema fulani kajenga nyumba nzuri!”

Yule kipofu husema, “uzuri wake kama punda?”

Na akija mwingine akisema “bandarini kumekuja merikebu kubwa!”

Yule kipofu hujibu, “ukubwa wake kama punda?”

Basi ikawa hivi sikuzote. Mtu atakayekuja mbele yake akasifu kitu basi yeye huuliza kitu hicho namna yake kama punda? Hata tena watu Wakastaajabu, Mwisho wakamwuliza, “Jinsi gani bwana wewe, mbona kila kitu kama punda!”

Akawapa kisa chake kilichompata, ya kuwa ailifumbuliwa macho yake, naye asione kitu ila punda. Basi, ulimwengu wote ukawa huyu punda. Kitu kizuri kama punda! Kikubwa, kama Punda! Kirefu kama punda! Na vingine vyote kama punda.

NYOKA NA JONGOO

Hapo kwanza Nyoka alikuwa ana miguu ila macho hana. Na Jongoo alikuwa na macho ila miguu hana. Wakafanyiza urafiki hata wakaahidiana kila mmoja katika wao akitaka kitu kwa mwenziye apate.

Hata siku moja Nyoka akamwambia Jongoo, “Sahihi,

leo kuna ngoma upande wa Nitakuja. Napenda uniazime macho yako nikatazame ngoma, na mimi nitakupa karadha miguu yangu.”

Jongoo akakubali akamwazima macho yake, naye akapewa miguu ya Nyoka.

Basi Nyoka akatoka akaenda kutazama ngoma. Na Jongoo akawa amekaa pale pale asiende mahali maana haoni. Ngoma ilipokwisha, Nyoka akawa anarudi. Alipofika nusu ya njia akatazama huko na huko, akaona faraja kubwa kuona vitu vizuri Akawaza moyoni mwake, “Wajua jongoo anafaidi, anaona vitu vizuri, tena aweza kuwaona adui wakiwa mbali. Basi ya nini nimrudishie? Yeye na atwae miguu, mimi nitatwaa haya macho.”

Akageuza njia akaenda upande mwingine. Mzee Jongoo akabakiwa na miguu mingi na macho hana. Nyoka akakaa na macho yake. Tangu wakati huo Nyoka na Jongoo hawakupatana tena.

KWELI TATU

HAPO kale palikuwa na mfalme mmoja, akatoa amri katika ufalme wake ya kuwa mtu atakayetenda neno kubwa la kustahili kufa, ataweza kusamehewa asiuawe akitoa maneno ya kweli matatu yasiyoweza kukanika. Ikatukia mmoja katika askari zake akahalifu amri ya kustahili kuuawa, akakimbilia mwituni. Na kule mwituni alikokwenda akazidisha ubaya wake wa kumwua kila mtu aliyepita upande huo. Mfalme akaagiza askari waende wakamkamate. Wakaenda wakamkamata wakamleta mbele ya Kadhi. Kadhi akamuuliza, “unajua amri ya nchi?”

Yule mtu akajibu, “Naam.”

Akamwambia, “ipi?”

Akanena, “Nikitaka salama yangu sharti niseme maneno matatu ya kweli asiyoweza mtu kuyakanusha kabisa. Nisipoweza kusema nitauawa.”

Kadhi akanena, “Ndivyo, Basi unayo maneno matatu ya kweli?”

Akanena, “Ninayo.”

Akamwambia, “Taja.”

Akanena,

1. “Mtu akikuambia mimi nimekuwa mbaya tangu kuzaliwa usimsadiki.”

Kadhi akaangalia akaona kweli, hapana mbaya tangu kuzaliwa, upo wakati alipoanza kuwa mbaya.

2. “Mtu akikuambia hali hii niliyo nayo sasa naipenda usimsadiki (ya kusimamiwa na mtu mwenye upanga mkononi tayari kuniua).

Kadhi akaona kweli, hapana mtu anayependa hali kama hii

3. “Mtu akikuambia mimi nikiachiliwa hapa nitarudia tena siku nyingme papa hapa usimsadiki.

Kadhi akaona kweli. Hapana mtu atakayekuwa mpumbavu atoke katika kinywa cha mauti halafu arudie tena.

Akamwambia, “Kweli, maneno yako thabiti wala hayakaniki, Akaachiwa wala hakuuawa.”

NDOTO

Hapo kale palikuwa na rafiki watatu wakisafiri. Baada ya siku kupita chakula chao kikawaisha ukabaki mkate mmoja wakafanya shauri wakanena, “Mkate huu ikiwa tutagawana wote hautatutosha. Basi na tufanye shauri.”

Wakapatana ya kuwa tulale wote, mtu atakaye ota ndoto ya ajabu, na atwae yeye mkate, na sisi wote tutakuwa radhi. Wakalala, lakini mmoja wao hakupata usingizi upesi. Basi huyu akatwaa ule mkate akaula wote. Hata wale wenzake wakaamka, naye akajifanya kama anatoka usingizini. Akawaambia, “Semeni ndoto zenu.”

Akajibu wa kwanza akasema, “Mimi nimeota ndoto ya ajabu.

Nimeona ngazi ya dhahabu imesimamishwa toka ardhi mpaka mbinguni. Wakaja malaika wakaichukua roho yangu wakaipandisha katika ngazi wakaipeleka mbinguni, nikaona fahari yote ya huko.

Nami nikafurahi mno kuona fahari ya mbinguni. Hii ndiyo ndoto yangu.”

Wa pili akasema, “Mimi nimeota nimejiwa na mashetani, wakitwaa roho yangu. wakaifunga kwa pingu za chuma wakaikokota mpaka Jehanam. Huko wakaiadhibu sana. Wakaniambia, ‘Hutatoka huku.’ Hii ndoto yangu.”

Wa tatu (yule aliyekula mkate) akasema, “Mimi nimeota nimejiwa na malaika, akaniambia, ‘Umeona yaliyowapata wenzako?’”

Nikanena, “La.”

akaniambia, ‘Nifuate.’

“Nikamfuata. Akanichukua mpaka panapo mlango wa mbingu nikakuona wewe umeketi juu ya kiti cha dhahabu, umezungukwa na fahari ya huko. Malaika akaniambia, ‘Unamwona mwenzako, basi hatoki huku maana wanaoingia huku hawatoki. ’”

“Tena akanichukua mpaka mlango wa Jehanam, nikakuona Wewe umo ndani, unaadhibiwa vibaya. Nikasikia kuwa na wewe hutoki kule maana imekuwajibu kukaa daima. Basi niliposikia kuwa ninyi wote wawili hamrudi tena, ndipo nikala mkate wote.”

MVIVU KUPITA WOTE NDIYE ATAKAYEKUWA MFALME

Palikuwa na mfalme alikuwa na wana watatu. Akawa anawapenda wote, hata hakutaka kumchagua mmoja kumpa Ufalme wake. Akawaambia wanawe, “Mtoto aliye mvivu kuliko wote ndiye atakayekuwa mfalme baada yangu.”

Basi wale watoto wakaja kwa baba yao ili kila mmoja aeleze uvivu wake.

Wa kwanza akasema, “Waama katika watu wavivu, kama mimi hajatokea.”

Akaaimbiwa, “Umekuwaje uvivu wako?”

Akanena, “Siku moja nalikuwa nimeketi karibu na moto, hata miguu yangu ikawa inaungua moto, nami nikaona uvivu kuiondoa!”

Wa pili akanena, “Mimi nimezidi. Maana kama angenifunga kamba shingoni akanining'iniza juu ya mti, akanipa na upanga mkononi niikate ile kamba, ningeona uvivu kusogeza mkono kuikata!”

Wa tatu akasema, “Mimi wangu si uvivu ila ni kuapizwa. Siku moja nimelala kitandani natazama juu, na juu yangu palikuwa na maji yanadondoka, na maji hayo asili yake ni mabaya yakimpata machoni, macho yatapofuka. Lakini mimi hulala tu, nikaona uvivu kugeuza uso wangu kwa kuume wala kwa kushoto.”

Mfalme aliposikia, akaona huyu wa mwisho kawashinda wote, akamwandikia ufalme uwe wake. Lakini siku moja akaja adui akataka kumnyang'anya ufalme wake, akaona uvivu kumzuia. Basi mwishowe akapoteza vyote alivyo navyo kwa uvivu

KISA CHA BINTI MATLAI SHEMS

Alikuwako mfalme mmoja, katika milki yake ana watoto sita walio wakubwa na mmoja mdogo. Ikawa siku moja mfalme na watoto wake wamekaa bustanini, akatokea ndege akatua juu ya mti. Na ndege huyu alikuwa mzuri san. Mbawa

zake za dhahabu, na miguu yake rangi ya lulu, Si mrefu, wala si mfupi, si mnene wala si mwembamba. Yule mfalme akampenda sana yule ndege.

Akawaambia wanawe, “tafadhalini wanangu, anipendaye mimi sharti akanipatie ndege yule.” Wakaondoka wale watoto wakubwa wakasema, “Sisi tutakupatia baba.”

Akasema, “Vema wanangu.” Na yule mdogo asiseme neno. Baba yao akawafanyia safari, kila mtoto akapewa farasi mmoja na watumwa mia.

Na yule mdogo akamwambia baba yake. “Baba na mimi nataka nisafiri pamoja na ndugu zangu nikakutafutie ndege huyu.”

Baba yake akamwambia, “Mwanangu, wewe kijana bado hutaweza kwenda mbali.”

Mtoto akajibu, “La, baba, hali ya wenzangu ndiyo hali yangu, nikipata huyo ndege, vema, sikupata huwa basi.”

Baba yake akakubali, akamfanyizia safari kama wenziwe, akampa farasi na watumwa mia, na fedha, maana yeye ndiye aliyempenda kuliko wenzake.

Basi wakaondoka wakaenda zao kutafuta ndege. Wakaenda mwendo wa siku tano. Wale wakubwa wakafanya mashauri kumuua ndugu yao. Wakamwambia, “Tupe mali yako yote, watumwa na farasi, ama tutakuua.”

Akawaambia, “Hamna haja ya kuniua, chukueni hii mali mniachie roho yangu.”

Wakamnyang'anya mali yote, wakamwacha yeye na nguo zake na kitabu chake, basi.

Walipokwisha mnyang'anya wakasema, “Baba huyu ana Wazimu, ametuambia tumtafutie mnyama mwenye mbawa, tutampataje sisi? Yeye anaruka, sisi tunakwenda chini. Afadhali sisi tufanye maskani hapa, tujenge mji wetu, watu tulio nao wanatutosha. Sisi tunao watu sita mia, na mia tuliomnyang'anya yule mjinga, jumla saba mia basi wanatosha Tuanze maskani hapa urefu wa umri wetu tutakaoishi katika dunia.”

Yule kijana alipokwisha nyang'anywa akaenda zake msituni na nyika, hata akapata mwendo wa siku mbili. Akatokea mahali pana jangwa kubwa upeo wa macho. Na katikati ya jangwa hili Pana mti mkubwa. Yule kijana akaenda kukaa chini ya ule mti pumzika.

Mara akasikia kishindo kwa mbali katika mwitu. Punde si punde akatokea zimwi mkubwa mno. Likaja likasimama pale alipo yule kijana, akamuuliza, “Wewe mtoto unatoka wapi?” akamjibu, “Sijui nitokako wala niendako.”

Akamwambia, “Umedhulumu roho yako basi, wewe hunitoshi mimi kwa chakula changu cha saa moja. Nitatwaa damu yako nifanye maji ya kusukutua, na mifupa yako nifanye mswaki, na nyama yako nifungulie kinywa.

Halafu niingie mwituni nitafute tembo wawili nifanye chakula.”

Yule kijana akanena, “Lile atakalokuamuru Mungu fanyiza, maana amri yote ina yeye.”

Zaidi ya haya yule kijana akampa habari yote tangu kutoka kwao, na habari iliyompata, hata kufika hapa. Yule zimwi akamwambia, “Nimesikia hayo lakini kama unataka salama ya roho yako nipatie chakula nile.”

Yule kijana akamwambia, “Mimi mwenyewe natafuta chakula, nitapata wapi chakula cha kukupa wewe?”

Akamwambia, “Sijui, kama hukunipa nitakuua.” Akamwambia, “Nipe muda wa saa mbili.”

Zimwi akanena, “Nimekupa.”

Yule kijana akatwaa kile kitabu chake akasoma, akaomba Mungu. Mara yakaja masufuria arobaini ya vyakula mbele yake. Zimwi akasema, “Sasa ndivyo.” Akayaingilia masufuria yale yote akayala. Yule kijana akastaajabu sana. Yule zimwi alipokwisha kula akasema, “Sasa na tuulizane hali, maana akili yangu imetulia.” Akamwambia, “Niambie unachotafuta.”

Kijana akamwambia, “Natafuta ndege mwenye mbawa za dhahabu, na miguu ya lulu.”

Zimwi akasema, “Namjua anakokaa, lakini mbali sana.” Kijana akamwambia, “Haidhuru, twende.”

Wakaondoka Wakaenda mwendo wa siku tatu. Wakafika mahali pana majumba yanaonekana kwa mbali. Zimwi akamwambia, “Unazona nyumba zileee?”

Akajibu, “Naam.”

Akamwambia, “Basi ukifika pale utaona watu, na huyo unayemtaka yupo katikati, ndani ya tundu. Lakini kuna ibra moja, ukisikia watu wanazungumza, basi wamelala hadi na ukisikia, wamenyamaza, basi wa macho.”

Yule kijana asiogope, akaenda hata pale. Akasogea mpaka panapo lile tundu, akataka kukamata, mara mazimwi wakamwona, wakamkamata. Wengine wakasema, “Tumle,” wengine wakasema, “Tumpeleke kwa Sultani.”

Mwisho wakampeleka kwa Sultani wao. Sultani akamuuliza, “Jambo gani lililokuleta huku wewe?”

Akanena, “Hapana zaidi ya ndege mliye naye.”

Akamwambia, “Vema, kama unataka ndege, nenda kanitafutie upanga wa radi, ukileta huo nitakupa ndege.”

Yule kijana akanena, “Inshallah.” Akarudi hata pale alipo rafiki yake zimwi. Yule zimwi akanena, “Je! Mbona hukupata?”

Akanena, “Nimeambiwa nikatafute upanga wa radi ndipo nimpate ndege, licha ya mmoja, hata wote.”

Yule zimwi akamwambia, “Vema rafiki yangu. Lakini nipe chakula kwanza nile tupate kufanya safari hata kunako upanga wa radi.”

Yule kijana akasoma vile vile kitabu chake, akaletewa masufuria arobaini vile vile kama kwanza. Yule zimwi akala. Kisha wakaondoka wakaenda mwendo wa siku mbili. Wakaona majumba kwa mbali, zimwi akamwambia mtoto, “Majumba yale ndiko kwenye upanga wa radi.”

Akaondoka mtoto akaenda, akaona mambo kama aliyoyaona kwenye ndege. Akaona panga zimetundikwa Na yule kijana hakuogopa, akaenda zake moja kwa moja akanyosha mkono azichukue zile panga, mara wenyewe wakamwona wakamkamata. Wengine wakasema, Tumble, na wengine wakasema, Tumpeleke kwa Sultani. Wakampeleka

kwa Sultani Sultani akanena “Unatafuta nini huku?”

Yule kijana akanena, “Natafuta upanga wa radi.”

Akaambiwa, “kama unataka, nenda ukanitafutie Binti Matlai Shems; ukimleta huyo utapata

upanga licha ya mmoja hata zote tatu.”

Kijana akamwambia, “Inshallah.” Zimwi akamuuliza, “Je! Mbona hukuleta upanga?”

Akamwambia, “Nimeambiwa mpaka nimlete Binti Matlai Shems ndipo nipate upanga.”

Wakafanya safari kwenda kumtafuta Binti Matlai Shems wakaenda hata wakafika pwani, mbele yao kuna bahari kubwa Zimwi akang'oa miti mikubwa akaunda merikebu nzuri akaitia baharini, wakaingia wakaenda

zao hata wakafika katika nchi ya Matlai Shems, baba yake Binti Matlai Shems.

Walipokwisha fika yule kijana akamwambia rafiki yake, “Je?

Sasa tumekwisha fika, nini shauri lako, hata tumpate Binti Matlai Shems?”

Yule zimwi akamwambia “Nyamaza kimya utampata.

Lakini inatakiwa hila kubwa sana hata umpate.”

Akamwambia, “hila gani?”

Zimwi akajibu, “Sharti wewe ujigeuze mganga, ujifanye unajua dawa sana, tena dawa yako ukimfanyizia mtu hafi.”

Yule kijana kanena, “Basi hayo kazi?”

Akamwambia, “Basi kesho shuka mjini hata kwa Sultani ukamweleze habari ya dawa yako. Lakini fahamu akikuambia mfanyizie dawa binti yangu, sema kama dawa ya binti yako haifai kufanyizia nchi kavu ila baharini. Basi akija huku utamchukua.”

Akanena, “Vema.”

Asubuhi kulipokucha yule kijana akaondoka akaenda zake mjini. Akafanya taratibu akafika hata kwa Sultani, akamweleza habari za dawa yake. Sultani aliposikia kuwa dawa yake mtu hafi akanena, “Mimi naitaka sana dawa hiyo, nataka unifanyizie mimi, mke wangu na binti yangu.”

yule kijana akamjibu, “Ewallah Seyidina.”

Akarudi merikebuni akampa habari rafiki yake.

Kisha akachukua madawa yake ya uongo-uongo akashuka pwani tena.

Akawafanyizia dawa wote, Sultani, na mkewe. Lakini kufikia Binti Matlai Shems akanena, “Huyu dawa yake haifai nchi kavu ila baharini tena asije na watu wengi ila mjakazi mmoja tu.”

Sultani akanena, “Vema.”

Yule kijana aondoka akaenda zake merikebuni kwa rafiki yake akampa habari kama Binti Matlai Shems atakuja kesho. Naye akamwambia, “Vema, nitakuwa tayari.”

Sultani akampa habari mwanawe, kuwa itamlazimu kufanyiza safari kwenda merikebuni kufanyiziwa dawa, lakini sharti aende yeye na kijakazi mmoja tu. Binti Matlai Shems akaitika, “Ewallah Baba.” Asubuhi akaja yule kijana kuja mchukua Binti Matlai Shems kumpeleka merikebuni.

Walipofika wakashuka vyumba vya chini kwenda kufanyiza uganga wa uongo-uongo. Kumbe! huku nyuma yule rafiki yake anaendesha merikebu. Hata Binti Matlai Shems alipotanabahi merikebu iko mwendo wa kutwa.

Bibi akashtuka, “wapi huku?”

Yule kijana akamwambia, “Huku ndiyo kwetu. Lakini wewe usitie hofu, Inshallah utarejea kwenu.” Na kule nyuma Sultani alipotazama, bandarini merikebu haipo, akafanya wazimu jinsi alivyompenda binti yake. Akatoa merikebu zake ziende katika dunia yote kumtafuta binti yake; hazikumwona, zikarudi. Na yule Sultani akalia, akamshukuru Mungu.

Na yule kijana na rafiki yake wakaja mpaka karibu na pale penye upanga wa radi. Akamwambia, “Je! rafiki yangu sasa tumefika penye upanga wa radi, na Binti Matlai Shems tunaye nini shauri lako?”

yule rafiki yake akamwambia, “Shauri hapana, ila mwombe Binti Matlai Shems akupe mjakazi wake, ukawaambie kuwa Binti Matlai Shems ni huyu.”

Yule kijana akanena, “Vema.”

Basi akamwambia Binti Matlai Shems ya kuwa, “tafadhali nipe mjakazi.”

Binti Matlai Shems akamwambia, “Vema.”

Akampokea yule mjakazi, akampamba kwanza lebasi za kiungwana, akawa mzuri kama vilivyo. Basi rafiki yake akamwambia, ‘Sasa mpeleke

mwambie huyu ndiye Binti Matlai Shems.”

Akasema, “Inshallah.”

Akaenda naye hata akafika

kwa yule Sultani wa mji ule, akamwambia, “Seyidina, Nimemleta Binti Matlai

Shems uliyemtaka.”

Sultani akafurahi sana, akamwambia chukua panga zote tatu. Yule kijana akanena, “La,

mimi matlaba yangu ni upanga mmoja tu.”

Akamwambia, “Basi hiari yako.”

Akanyanyua mkono akachukua upanga mmoja. Akaja nao hata kwa rafiki yake, akamwambia, “Huu upanga wa radi nimeupata.” Akamwambia, “Sasa twende zetu kwenye tundu la ndege.”

Wakaenda zao hata walipopata karibu. Yule kijana akasema,

“Nini shauri lako, rafiki yangu?”

Yule zimwi akamwambia, “Hapana shauri ila tufanye upanga mwingine tusipeleke huu.”

Basi yule zimwi akachonga upanga mwingine wa mti, akaupaka dawa ukageuka kuwa wa chuma, akamwambia, “Chukua huu ukampe Sultani, mwambie ndiyo upanga wa radi.”

Yule kijana akauchukua akaenda nao hata kwa Sultani, Akanena, “Huu upanga wa radi nimekuletea.”

Yule Sultani akafurahi sana, “akamwambia Chukua ndege Wote Watatu.” Yule kijana akasema Matlaba yangu ni ndege mmoja.”

Akamwambia, “hiari yako.” Basi akamchukua ndege mmoja na tundu lake. Akaja kwa rafiki yake akamwambia, “Sasa tumepata haja zetu, sasa twende moja kwa moja kwa baba yako au twende kwa ndugu zako?”

Kijana akasema, “Twende kwa ndugu zangu.”

Zimwi akamwambia, “Nenda, lakini nitakupa akiba ya neno. Chukua nyoya hili, ukipatikana na neno tia nyoya hili motoni. Nami nitakutokea kukidhi haja yako.”

Yule kijana akapokea unyoya, akaondoka akaenda kwa ndugu zake. Akawakuta wamestarehe wanalima mashamba. Akafika yule kijana akawaeleza mambo yote. Na wale ndugu zake wakamuuliza, “ndugu yetu, na huyu mwanamke ni nani?”

Yule kijana asiseme jina lake yule mwanamke, akasema, “nimemuokota njiani tu, na upanga huu nimemkuta anao huyu mwanamke. Na huyu ndege ndiye anayemtaka baba. Basi twendeni kwa baba kwa umoja wetu, tutasema kuwa huyu ndege tumepata sote.”

Wale ndugu wake wakalala, hata usiku wakamkamata ndugu yao. Wakamkaba roho hata akazimia, wao wakadhani amekufa. Wakaenda wakamtupa mbali. Na yule binti Matlai Shems alipoona vile, moyo wake ulaudhika, akawa hali wala hanywi, wala hasemi. Wakaondoka ndugu wale sita. Wakamchukua yule bibi, na upanga na ndege. Wakaenda hata kwa baba yao.

Baba yao alipowaona watoto alifurahi, akapokea na yule ndege. Akawauliza, “ndugu yenu yuko wapi?”

Wakasema, “hatujui, alikwenda njia ya peke yake.”

Baba yake akasema, “Na apotelee mbali sababu alishika shauri la peke yake.”

Baba yao akawauliza tena, “mwanamke huyu jina lake nani?”

Wakasema, “hatumjui, tumemuokota njiani na upanga wake.”

Tena akawauliza, “kwanini basi hasemi mwanamke huyu, wala hali wala hanywi?”

Wakasema, “labda anawaza kwao.”

Na yule kijana kule alikotupwa, baada ya saa nyingi kupita ukampiga upepo wa alfajiri akaja juu, akapata fahamu. Mara akatafuta moto akatwaa ule unyoya aliopewa na arafiki yake, akautia motoni. Mara rafiki yake akatokea.

Akatokea akamwambia, “je rafiki yangu una nini?”

Akampa habari yote ya ndugu zake jinsi walivyomtenda. Akamwambia, “haidhuru rafiki yangu mimi nitakupeleka kwa baba yako.”

Akampa nguo nzuri akavaa, akampa na farasi akampanda, akamchukua mpaka kwa baba yake.

Akamkuta baba yake yuko barazani na watu wamejaa tele na wale ndugu zake wapo. Akaanguka mbele ya baba yake akamwadithia habari zake zote, tangu mwanzo hata mwisho. Akasema, “Na mwanamke huyu ndiye Binti Matlai Shems upanga huu ni upanga wa radi. Na habari hizi akieleza rafiki yake zimwi yupo anatia sahihi.

Kisha akaja Binti Matlai Shems akajinadi akasema naye habari zake, hata watu wakastaajabu,

Mara Sultani akaamrisha watoto wake sita wauawe. Wakashonewa mafumba wakatoswa baharini. Na yule kijana akapata heshima kubwa kwa babaye akamwoza yule Binti Matlai Shems. Baada ya Siku kupita. Kijana akamchukua Binti Matlai Shems akampeleka kwa babaye. Na baba yake alipomwona binti yake akafurah akamshukuru yule kijana. Akawafanyizia arusi mara ya pili na Wakakaa raha mustarehe.

MWAMINI MUNGU SI MTOVU

Alikuwako mtu mmoja na mkewe, hawakuwa na kitu, rasilimali yao ni kondoo na jogoo. Siku moja wakapata habari kuwa rafiki yao anakuja kuwatazama. Mke akamwambia mumewe, “Mume wangu kesho anakuja mgeni wetu na sisi hatuna kitu.

Ila huyu kondoo na jogoo. Na mimi kumchinja kondoo wangu sitaki na kumchinja jogoo wangu sitaki.”

Mumewe akamwambia, “ikiwa hapana budi labda tutamchinja kondoo.”

Na maneno haya kondoo na jogoo wanasikia. Hata usiku jogoo akaanza kuwika kwa furaha, na maneno aliyosema akiwika ni haya:

“Usiku na uche tumchinje kondoo!”

Na kondoo hujibu, “Allah! Allah!”(maana yake mambo kwa Mungu).

Usiku na uche tumchinje kondoo.”

Na kondoo hujibu, “Allah! Allah!.” Tu.

Hata kulipokucha wakaanza kuzaa mashauri mengine. Mke akasema, “bwana, huyu mgeni anayekuja ni mgeni wa siku moja. Pana haja gani kumchinja kondoo kitoweo cha siku tatu? Afadhali tumchinje jogoo.” Akakamatwa jogoo akachinjwa, yule aliyemtumaini mwenyezi Mungu akasalimika.

KASA NA KITATANGE

Zamani moja, wanyama wote wa baharini walifanya shauri wafanye baraza ili waepuka hila za kiumbe aitwaye binadamu. Maana huyu ni kiumbe anayewaudhi sana. Huwatega kwa ndoano na nyavu.

Basi wakakutana ili wafanye shauri la kuepuka hila zake. Basi ikapigwa mbiu ya mgambo asiye mwana aeleke jiwe, wote wakutane kwa Sultani Nyangumi kufanya mashauri haya. Hata siku ya mkutano ilipowadia wanyama wote wa baharini wakakutana. Wakatazama wakaona ya kuwa kasa hakuja katika mkutano huu. Basi wanyama wote wakakasirika, wakasema, “hii ni namna gani, sisi tuliokuja si kitu, yeye bora kama nini?” Na tufanye mashauri yetu. Tukiisha tumwendee tukamhoji atupe hoja za kuacha kuja.”

Na katika mkutano huu yupo bwana Kitatange, na huyu ni sahibu yake sana kasa. Basi. Aliposikia maneno haya, akamtuma mtoto mpaka kwa Kasa akampa habari iliyopo. Mtoto wa kitatange alipofika akamwambia Kasa, “Baba kanituma anena kimbia, jamaa

wote wakiisha mashauri yao wanakuja kwako, maana wameudhika kwa kuwa hukuhudhuria katika mkutano.”

Kasa akauliza, “Je Mwenyezi Mungu yupo pamoja nao?”

Yule mtoto akasema, “Sikumwona, wala simjui. Amekaaje?”

Kasa akasema, “Sijui namna yake, mimi nauliza hivyo tu.”

Yule mtoto akaenda zake.

Halafu Kitatange akampeleka mtoto mwingine akazidi kumtafadhalisha akimbie. Kasa akauliza maneno yale yale, Mwenyezi Mungu yupo pamoja nao? Akanena, Sikumwona wala simjui, akasema, basi sikimbii.

Kitatange alipoona wanyama wote wanaondoka kumwendea,

Kasa, akampeleka mkewe, akamwambia, “Tafadhali nenda upesi kamwambie sahibu yangu ajifiche, jamaa wote wanakuja kwake.”

Mke wa Kitatange akaenda, akampa habari yote. Kasa akamwuliza swali lile lile, “Mwenyezi Mungu yupo pamoja nao au wao tu?”

Akanena huyo, “Sijui, wala Sikumwona. Amekaaje?”

Kasa akasema, “Hata mimi simjui namna yake.”

Hata wanyama wote walipokuwa karibu, Kitatange mwenyewe akakimbia akamwambia, “Sahibu usiwe na haja kukaa hapa, jifiche, maana wamekukamia sana.”

Kasa akaimwambia Kitatange, “Mwenyezi Mungu yumo pamoja nao.”

Kitatange akashangaa akasema, “Huyo sikumwona waama jamaa Wote wapo.”

Kasa akasema, “Basi sijifichi.”

Punde si punde wakaja wote wa baharini pale pale alipokuwapo Kasa. Mwenyezi Mungu akamjaza imani yake akatwaa lile gamba alilo nalo akamfunika, miguu na kichwa akatia ndani. Basi wao wakatafuta wasimwone, naye yupo pale pale, lakini Wakadhani ya kuwa ni jiwe. Mwisho

wakasema, “ameombewa huyu amejua kujificha, tungemtia adabu leo kwa ukaidi wake.” Wakatawanyika, kila mmoja akaenda kwake.

Mwamini Mungu si mtovu.

YALIYOMO

kisa cha kwanza

Kisa cha pili

Kisa cha tatu

Kisa cha nne

Kisa cha tano

Kisa cha sita

Kisa cha saba

Kisa cha nane

Kisa cha tisa

Kisa cha kumi

Kisa cha kumi na moja

Kisa cha kumi na mbili

Sultani na mvuvi

Sultani na mkwewe

Mvuvi na jini

Kisa cha majuha wawili wanawake

Jogoo na sungura

Kisa cha paka kupenda mekoni

Kisa cha kuku na mwewe

Kisa cha majuha watatu

Simba na sungura

Fikirini na Hemedi

Kisa cha Wadigo

Kisa cha mtu na wanawe

Hadithi ya mtoto wa sultani na wa tajiri

Wezi stadi

Mtego wa panya huingia waliomo na wasiokuwamo

Mganga na mwanafunzi bubu

Kiburi si maungwana

Kisa cha maskini

Hadithi ya bibi mg'indo

Kwanini watu weupe huitwa wazungu

Kisa cha Ali na watoto wa nduguye

Kisa cha sungura na cheche

Wajinga ndiyo waliwao

Mbwa na paka

Njia ya kuvukia mwenye deni

Kama Punda

Nyoka na jongoo

Kweli tatu

Ndoto

Mvivu kupita wote ndiye atakayekuwa mfalme

Kisa cha binti Matlai Shems

Muamini Mungu si mtovu

Kasa na kitatange

Hadithi ya chewa

Kisa cha kuku na kanga

Mtoto wa maskini

Mtu aliyesikia lugha za wanyama

Binti Hamadi

HADITHI YA CHEWA

Asili ya Chewa kuwa na kinywa kipana ni hii. Chewa alikuwa na wazee wake na ndugu zake na mkewe. Akasafiri kwenda nchi ya mbali. Hata alipokuwa huko akaja mtu anayetoka kwao akampasha habari ya kuwa baba yake amekufa. Chewa akanena, “Hiyo ni kazi ya Mungu.” Asifanye msiba, wala asione uchungu katika moyo wake. Hata siku nyingine akaja mtu mwingine akamwambia, “Mama yako kafa.”

Chewa akasema vile vile. Hata siku nyingine akaja mtu akamwambia, “Nduguyo kafa.”

Chewa akasema vile vile. Wakaisha jamaa zake wote naye husema maneno hayo hayo. Hata siku moja akaja mtu anayetoka kwao vile vile, akamwambia, “Unazo habari?”

Akanena, “La, sina habari.”

Akamwambia, “Mkeo kafa.” Chewa akanena, “A-a-a-a.” Akapanua kinywa kwa kustaajabu.

Ndiyo asili Chewa kuwa na kinywa kipana.

KISA CHA KUKU NA KANGA

Hapo zamani Kuku na jogoo hawakuwa wanyama wa mjini.

Walikuwa wanyama wa mweituni, wakikaa wote pamoja kuku na kanga na ndege wengine. Basi ikawa siku moja ikanya mvua moja kubwa huko mweituni.

Kanga akamwambia kuku, “Nenda mjini kwa watu waitwao Binadamu, wenye miguu miwili, mikono miwili, na macho mawili, ukaombe moto, tuje tuote maana baridi imezidi.”

Kuku akaondoka akaenda hata mjini kwa Binadamu. Alipofika akakaribishwa vizuri. Wakaulizwa haja yake akasema, “Mimi mtu wa mweituni naja kuomba moto, maana kwetu hakuna moto.”

Wale Binadamu wasimpe moto, wakazidi kumkaribisha kwa kumpa vyakula. Tena akawaona Binadamu wamestarehe sana, wengine wamelala usingizi wa mchana, na wengine hivi. Binadamu wakazidi kumpa vyakula, hata mwisho akasahau aliyotumwa. Na kule mweituni kanga alipoona kuku anakawia akamtuma jogoo aende kumhimiza. Jogoo akaenda. Alipofika kwa Binadamu naye akakaribishwa vizuri kama kuku. Alipoingia ndani akamkuta kuku kaupiga usingizi hana habari.

Akaamshwa. Jogoo akamuuliza, “jinsi gani kuku, mbona kimya?”

Akamwambia, “mimi sirudi tena mweituni, maana tangu kuja Binadamu wamenitendea mema matupu, basi nirudi mweituni nikafanye nini?” kisha akamwambia jogoo, “Ela njoo ule chakuja nilichobakiza mimi.”

Jogoo akala, kikampata. Na yeye akaingia ngomani, akapanga akasema, “Na mimi sirudi mweituni.”

Na asili kuku wanapokunywa hutazama juu.

Yaani Wanamshukuru Muumba aliyewajalia kupata riziki kwa binadamu.

Lakini wema wa Binadamu hauna kuendelea sana. Siku moja Walikuja wageni kule nyumbani kwa Binadamu. Wakatazama Wakaona wana chakula tu, hawana kitoweo. Basi Wakafanyiza mashauri wakanena, “Hatuna haja kusumbuka kimfaacho mtu chake, tumkamate kuku tumwue tumfanye kitoweo cha wageni wetu.”

Mara wakamkamata. Akalia, “Si mimi Si mimiii!” Lakini wapi?

Binadamu wakamchinja.

Jogoo kuona, akapiga kelele naye, akalia, “Koko! Likoo!” Maana yake, Kuku umenidanganya.

Kanga akawa amechoka kungoja. Basi naye akaja hata karibu na mji wa Binadamu akapiga kelele, “Kuku wee! Kuku wee! Nimekuambia kapae moto! Kimya! hakisikia sauti?”

Alipozidi kuita jogoo akamjibu, “Ya kale hayakooo! Usiingie ujinganiii?”

Kanga aliposikia hivyo akajua kuwa hawa hawarudi tena, akarudi kwenda mwituni.

MTOTO WA MASKINI

Walikuwako watoto wengi wa kimaskini wanakutana kucheza mahali pamoja, na mchezo wao mkubwa ulikuwa kutafuna katu na tambuu.

Hata siku moja akapita mtoto wa Sultani, akamwona mtoto mmoja mwanamke katika wale watoto wa kimaskini mzuri kupita wenzake. Akawauliza wafuasi wake, “watoto hawa wanafanyiza nini hapa?”

Wakamwambia, “Hawa ni watoto wa kimaskini. Hukutanika hapa kucheza, basi hii ndiyo kazi yao.”

Akamwona yule mtoto mzuri, akauliza, “Na yule pia?” Wakamwambia, “Ndiyo.”

Mtoto wa Sultani akasema, “Mimi nataka kumwoa mtoto yule.” Wakampasha habari baba yake. Baba yake akakubali. Basi mtoto wa Sultani naye akamwarifu baba yake.

Baba yake akakubali, akawaoza.

Yule mtoto wa maskini hakupenda kuachana na wenzake, lakini ni mambo ya wazee wake ndio waliomshurutisha aolewe. Akakubali kwa shingo upande. Hata alipokuwa katika nyumba ya mtoto wa Sultani hakuwa na furaha. Akapewa chakula kizuri na starehe zote, lakini yule mtoto hakuwa na furaha. Ikawa wakati mumewe anapokwenda barazani yule mtoto hubaki peke yake chumbani. Na kule chumbani akisimama dirishani huwaona wale wenzake wanacheza chini ya mti.

Na yeye mara hukumbuka akicheza pamoja nao.

Basi tena hulia, akiimba hivi;

Wale wenzangu wale

Wale wenzangu

Wale Wanakula katu zao

Mimi wali wa samli

Wanisonga moyo!

Huimba hivi mpaka mumewe arudi. Akija humkuta macho yamevimba. Naye humwuliza, “Una nini bibi?”

Naye husema, “Sina kitu.”

Ikawa kila siku kazi ni kama hiyo. Mwanamke hali ila kidogo tu, maana wali wa samli unamsonga mayo. Hata siku moja watwana

wa mle nyumbani wakamwambia bwana wao ya kuwa, “Bwana unapoondoka, huku nyuma hulia na huku akiimba, na maneno anayoimba ni haya:

Wale wenzangu wale

Wale Wenzangu

Wanakula katu zao

Mimi Wali wa samli

Wanisonga moyo!

Basi mtoto wa Sultani akasema, “kesho nitayapeleleza mambo haya. Akaaga kuwa anakwenda barazani kama desturi yake. Akamfungia bibi chumbani akaenda zake.

Alipopata njiani akarudi akaja akasimama mlangoni. Akamsikia mkewe ndani analia na kuimba kwa maneno kama yale. Na zaidi kuliko haya asema, “Mambo gani haya yaliyompata binadamu, kuolewa kwa nguvu! Mambo ya wazee haya!”

Mara mtoto wa Sultani akafungua mlango. Akamwambia, “Ah! Mke wangu, kumbe! hayo ndiyo yanayokuliza siku zote? Unakumbuka wenzako

na katu zao? Na raha hii huitaki? Basi bibi, mimi nalidhani ulikubali kwa ridhaa yako. Na sasa hapana haja, nenda zako kwenye katu zako.”

Akamwacha aende zake, Mtoto mwanamke akafurahi sana. akatoka, akarudia pale pale panapo mti kucheza na wenzake.

MTU ALIYESIKIA LUGHA ZA WANYAMA

Alikuwako mtu mmoja amepata bahati ya kusikia lugha zote za wanyama. Na ndani ya nyumba yake alifuga ng'ombe, punda, mbwa, paka na kuku. Ikawa siku moja yule mtu anatembea upande wa uani walikowaweka wale wanyama.

Akamsikia punda akimwambia ng'ombe ya kuwa yeye atajitia ugonjwa kesho maana kazi zimezidi.

Asubuhi ng'ombe peke yake akaenda kazini.

Na alipofika kazini akakuta kazi moto mmoja, akapewa kazi mara mbili kuliko siku zote. Lakini alipofika bandani alikokuwako punda, ng'ombe hakusema habari za kazi. Akasema, “Mimi leo sikupewa kazi, nalifungwa panapo majani nikila tu, hunioni nilivyoshiba?”

Punda akasadiki. Hata asubuhi punda akaondoka akaenda kazini alipofika akakuta kazi zaidi kuliko siku zote. Akafanyiza mpaka Jioni. Aliporudi bandani akamwambia ngo'mbe, “Umenitendaje wewe, umeniambia hakuna kazi kumbe kazi imezidi?”

Ng'ombe akamwambia, “Ndiyo, mimi nalikuambia vile kusudi usizidi kulala ningekuambia kama kuna kazi ngumu ungezidi kujitia mgonjwa.”

Basi yule bwana aliposikia maneno yale alicheka sana maana ameyasikia maneno yao tangu mwanzo.

Alipokuwa anacheka mkewe akamwona, akastaajabu kumwona anacheka na wanyama. Akamwuliza, “Mume wangu, unacheka nini?” Akamwambia, “Nacheka tu.” Akamwambia, “La, sharti utaniambia unachochea.”

Huku na huku, mwisho yule bwana akamwambia. “Mke wangu, mimi nimepata bahati ya kusikia lugha za hawa wanyama. lakini nina mwiko

mkubwa, nikisikia maneno nisiseme nikisema nitakufa.”

Akamwambia, “sharti utaniambia.”

Akamwambia, “Huachi mke Wangu unanitakia kufa?”

Akanena, “Mimi sijui hayo.”

Akawaita jamaa zake na mke wake akawaeleza habari hii, na wao wakasema naye lakini hakukubali.

akasema, “Sharti utaniambia.” Hatimaye yule bwana akanena vema, “kesho nitakuambia. Lakini fahamu kuwa mimi ndiyo mauti yangu.”

Alipokuwa akisema na mkewe paka alikuwako, akasikia. Akaenda mbio akamweleza mbwa akamwambia, “kesho bwana atakufa.”

Mbwa akasema, “imekuwaje?”

Paka akaeleza habari zote za ng’ombe na punda na jinsi bwana alivyochekea kisha paka na mbwa wakaenda kwa ng’ombe na punda wakawaambia, “mmefanyaje ninyi?”

Wakamwambia, “kulikoni?”

Wakasema, “kesho bwana atakufa na sababu ya kufa ni maneno yenu ninyi mliyosema kwa sababu habari za kazi bwana alikusikieni akachekea. Basi mkewe alipomwona anachekea akataka kujua anachochekea.

Naye akasema atakufa lakini kwa kuwa amemshikilia sana amesema kesho atamwambia.” Basi wale wanyama wanne. wakakaa kwa kujiinamia wakikumbuka kuwa bwana wao atakufa kesho. Mara akaingia jogoo, yeye hana habari ile iliyopita. Akaja kwa vishindo, na kuwika, na kuruka! Wenzake wakamwambia, “wewe jogoo namna gani bwana anakufa kesho na wewe umo katika furaha?”

Jogoo akasema, “Bwana atakufa?”

Kuna nini?”

Wakamueleza mambo yale yote. Jogoo akasema, “Ah! Hayo anapenda mwenyewe. Mbona mimi nina wake wengi na mimi hawanitadii, wakinifanyia jeuri kidogo huwapiga kwa mabakora wote, nao wanashika adabu zao. Lakini yeye bwana anapenda mwenyewe.”

Kumbe bwana akawa anasikia yale maneno. “Akasema, Ajua kweli, nitajaribu dawa ya jogoo.”

Asubuhi kulipokucha akamwita mkewe ndani, akamwambia, “Nalikuambia, Kesho nitakuambia nilichocheka basi sasa nitakuambia.”

Akatwaa mkwaju, akamchapa vema. Kisha akasema, “Haya ndiyo maneno niliyosikia kwa jogoo, amesema tangu nimekuoa hajaona nikikupiga, ndiyo niliyocheka.”

Mwanamke akatoka akaenda kwa wazee wake na fimbo zimemwota maungoni.

Wazee wakamwambia, “Je! hatukukuambia? Sasa yote yaliyokupata stahili yako, na hivyo rudi kwa mumeo.” Akarudishwa kwa mumewe akakaa kwa heshima na adabu.

BINTI HAMADI

Palikuwa na mtu jina lake Hamadi, akazaa binti saba. Na wote walikuwa wazuri sana. Na katika mji alikuwako mtoto mmoja wa tajiri akamposa Binti Hamadi mmoja akamwoa.

Lakini yule mtoto wa tajiri hakutaka kumwoa kwa kuwa Alimpenda, la! Ila alimhusudu yule Hamadi akataka kumuulia watoto wake. Basi alipomuoa yule binti Hamadi wa kwanza akamweka ndani ya nyumba ya watumishi, na vyakula lakini wasipike. Yeye mwenyewe alikua akila nyumbani kwa baba yake na nyumbani kwake hapikiwi kitu. Watumishi wakitoka kwenda kula nje, ila bibi hapati kutoka. Na wakija watu kumtazama hawamwoni maana bibi anatawa. Kusudi yule mwanamke asipeleke habari kwa baba yake ikawa mambo ni kama hayo mchana kutwa humletea kitu kidogo mkononi basi.

Yule mwanamke akadhii kwa kutwa hapati kula, mwisho akafa. Na wazee wake hawakujua kwa sababu ya kufa kwake wakadhani ni ajali tu. Baada ya kufa yule wa kwanza mtoto wa tajiri akataka kuoa Binti Hamadi wa pili na wazee wake hawakukasiri wakampa. Akamtenda kama yule mtoto wa kwanza naye akafa,

Akawaoa watoto sita na wote wakafa kwa dhiki ya njaa. Akabaki kitinda mimba na yeye pia akaolewa na yule yule alipofika nyumbani akaona namna yake akatambua kuwa nduguze wamekufa kwa dhiki ya njaa. Basi akafanya shauri kuwa yeye hakubali atakula.

Basi ikawa bwana anapoondoka kwenda kwa baba yeke, bibi naye anakwenda ghalani anatwaa vyakula anawapa wajakazi kupika. Hata bwana akiya anakuta nyumba imejaa harufu ya vyakula. Akiisha pakua anampa bwana chake, lakini bwana hukataa. Bibi anakula chake mpaka kushiba. Mambo yale bwana yanamuudhi lakini hana la kufanya.

Hata ikawa anaporudi kutoka kwa baba yake neno lake la kwanza kumwita mkewe. “Binti Hamadi!”

Naye humwitikia, “Labeka bwana.”

“Na leo umepika?”

Naye hujibu, “na leo pia.”

Basi akafanyiza namna hii ata akawa mgonjwa kwa simanzi maana yale yanamuudhi. Na katika ugonjwa huu binti Hamadi hakuacha kupika, hupika akala kama desturi. Na bwana kila siku akirudi humwita vile vile, “Binti Hamadi!”

“Labeka bwana Pia, na pia Bwana.”

Hata ugonjwa ukazidi maana yeye alikuwa hali na kuwambia wazee wake hapati anaona haya. Wazee wake wakaja kumtazama pamoja na watu wengine. Na yeye katika katika kuugua kwake neno lake lili hili, “Binti Hamadi!”

“Labeka bwana, Pia, na pia bwana.” Watu hawafahamu maana yake wanajua wao wenyewe tu! Hata karibu na kukata roho akaita tena “Binti Hamadi!”

“Labeka bwana Pia, na pia bwana.”

Akafa .Alipkufa wazee wake na watu waliokuwapo wakauliza, “nini maana yake maneno waliyosema?”

Akawaambia, “maana yake mali yangu yote yako pia usimpe mtu, nami humjibu, vema yote yangu. Basi wazee wakampa mali yote ya munewe. Na siri ile ya pia, na pia bwana hawakuijua.